Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini na Moja - Tarehe 8 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa Mwaka 2004/2005.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 198

**Upatikanaji wa Hati za Vijiji**

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wananchi wa Mtwara Vijijini wameleta maombi ya kutaka wapatiwe hati za Vijiji tangu mwaka 1999, lakini Serikali imekuwa inawapatia namba za Vijiji bila hati na kueleza kuwa waendelee kusubiri hati zinaandaliwa, kwa mfano, mwaka 1999/2001, zilitolewa namba za Vijiji vya Niyumba, Kiwenguro na Mnivata ambavyo vinaendeshwa kwa namba tu hadi leo na mwaka 2003 zilitolewa tena namba za Vijiji 27 bila hati na kuahidi kuwa hati zinaandaliwa na kwamba zitapatikana kabla ya Novemba, 2004 wakati wa uchaguzi ujao wa Vijiji/Vitongoji huku Serikali ikituhimiza tuwafikishie ujumbe Wananchi kuwa wawe na moyo wa subira na imani kwamba hati zao zitapatikana:-

(a) Je, Serikali inaweza kuharakisha kuwapatia wananchi hati hizo mapema ili Vijiji husika vipate muda mzuri wa maandalizi ya kufikiria kuwapata viongozi bora wa Vijiji na Vitongoji?

(b) Kwa kuwa imefahamika kuwa huenda zikatolewa hati za Vijiji vichache kati ya hayo maombi yaliyopelekwa, je, Serikali inasema nini juu ya jambo hilo na kama ni kweli, vile Vijiji vitakavyokosa hati wakati wamepewa namba si kuwakosesha haki wahusika na kuwafanya waichukie Serikali yao?

(c) Kwa kuwa inasemekana kuwa maombi yasiyoambatana na Vitongoji kuanzia vinne au vitano hawapati hati ya Kijiji, je, hivi sasa tafsiri sahihi ya Vitongoji ni nini na Serikali inayo hakika kuwa tafsiri hiyo inafahamika hivyo kwa Wilaya, Kata na Vijiji au ni Wizara peke yake ndiyo wanaoijua tafsiri hiyo na je, tafsiri hiyo imepelekwa hadi ngazi za chini za Vijiji na kama haijapelekwa kuna haki gani kuwaadhibu Wananchi wa Vijiji vingine kwa kutowapa hati?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilipokea maombi ya Wananchi wa Halmashauri ya Mtwara ya kutaka kupatiwa hati za Vijiji ambayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Mbunge mwenyewe mwaka 2003. Maombi ya awali kuhusu usajili wa Vijiji vitatu vya Niyumba, Kiwenguro na Mnivita, hati zake zipo tayari na zitawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara kwa utaratibu uliowekwa. Aidha, Vijiji 27 vya Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara vilivyowasilishiwa maombi ya usajili, hati zake zinashughulikiwa pamoja na maombi ya Vijiji vingine nchi nzima. Usajili wa Vijiji hivyo utakamilika kama nilivyosema wakati wa hotuba yangu ya bajeti kabla ya mwisho wa mwezi Agosti, 2004.

(b) Mheshimiwa Spika, sifa mojawapo katika kusajili Kijiji ni kila Kijiji kuwa na vitongoji vitatu au vitano. Aidha, mwongozo wa jinsi ya kusajili vijiji kulingana na sifa zinazotakiwa unafahamika vizuri kwa Halmashauri zote. Mwongozo huu unaelekeza kwamba ni sharti kwanza yatolewe maombi rasmi yanayotokana na Mkutano Mkuu wa Kijiji husika, maamuzi ya Kamati ya Maendeleo ya Kata na uamuzi wa Baraza la Madiwani.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, maombi yanayoletwa yanatakiwa kutimiza sifa nilizozitaja ili yaweze kushughulikiwa na kupatiwa hati za usajili.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba amepokea maombi yale kutoka kwangu na atashughulikia haraka iwezekano na kwa vile nilishampa pia na maombi ya Mji Mdogo. Je, Mheshimiwa Waziri tukimwalika kwenye sherehe kubwa ambayo inaandaliwa Mtwara Vijijini ya kupatiwa Mji Mdogo na Vijiji, yuko tayari kufika kwenye sherehe hiyo? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Yuko tayari, hilo siyo swali. *(Kicheko)*

Na. 199

**Madai ya Walimu**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA (k.n.y. MHE. HASSAN C. KIGWALILO)** aliuliza:-

Kwa kuwa walimu wengi wa shule za msingi na za sekondari wakiwemo wale wa Wilaya ya Liwale wana malimbikizo ya madai yao mbalimbali yatokanayo na uhamisho, matibabu na kadhalika na kwa kuwa hali hiyo imekuwa kero kubwa kwa walimu nchini kote:-

(a) Je, Serikali inadaiwa kiasi gani cha fedha na walimu hao na ina mikakati gani ya kumaliza kero hiyo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuchelewesha kuwalipa walimu madai yao mbalimbali kutazorotesha elimu na mahusiano mazuri kati ya walimu na Halmashauri zao?

(c) Je, ili kupunguza kero hiyo kwa walimu kwa nini Serikali haisitishi kwa muda uhamisho mpaka hapo fedha itakapopatikana?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika miaka hii mitatu jumla ya madai ya walimu walio chini ya Wizara yangu yalikuwa Sh. 1,246,395,576.50/=. Jumla ya madai yaliyolipwa ni Sh. 1,209,910,587.50/=, kwa hiyo, bakaa ni Sh. 36,484,989/=. Madai yaliyobaki ni kwa sababu ya wahusika kutowasilisha nyaraka na fomu mbalimbali zinazotakiwa kwa malipo husika.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kuchelewesha kulipa madai halali ya walimu hao, kunachangia katika kuzorotesha elimu na uhusiano mzuri wa kikazi. Ndiyo maana Wizara yangu inalipatia uzito suala la kulipa madai yote ya walimu yaliyohakikiwa yakiwemo ya uhamisho, matibabu na likizo kila wakati fedha zinapokuwepo katika bajeti. Kwa kuzingatia ukweli huo, Wizara yangu kufikia tarehe 30 Juni, 2004, ilikuwa imekwishafanya malipo ya madai ambayo nimekwishayaeleza katika (a) hadi kufikia hiyo albaki ya Sh. 36,484,289/= ambayo hayajakamilika kutokana na sababu nilizozitaja katika sehemu (a).

(c) Mheshimiwa Spika, uhamisho wowote unaofanywa ni ule unaozingatia mpangilio sahihi na ikama ya walimu katika kila shule. Aidha, uhamisho unafanywa kutokana na kufunguliwa kwa shule za sekondari mpya nyingi zinazojengwa kila mwaka kwa nguvu za wananchi. Kwa sababu hiyo, uhamisho hauwezi kukwepeka, kinachohitajika ni kuendelea kujitahidi kutafuta fedha za uhamisho na wahusika wa uhamisho huo kulipwa stahili zao mapema.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukanusha kabisa madai yaliyotolewa na Rais wa Chama cha Walimu Tanzania kuwa wafanyakazi wa Makao Makuu wanakula fedha za walimu. Kinachofanyika Makao Makuu ni kujitahidi kuhakiki madai yote kwa uangalifu kuepukana na madai hewa. Mwenyekiti wa CWT yeye mwenyewe amenukuliwa akisema na ninanukuu: "Mwaka 1998 CWT ilipeleka madai ya malimbikizo yaliyofikia Sh. 9.1 bilioni na baada ya uhakiki wa Serikali zililipwa Sh. 4.2 bilioni". Maneno hayo yanadhihirisha umuhimu wa kuhakiki madai yote kwa uangalifu.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri. Kwa vile Mkoa wa Lindi na hususan Wilaya ya Liwale, maendeleo ya elimu ni duni na pia matokeo ya darasa la saba kwa shule za msingi pamoja na ya sekondari ni mabaya zaidi na pia kuna matatizo mengi ya walimu. Je, sasa hivi sio wakati muafaka baada ya bajeti hii Mheshimiwa Waziri kutembelea sehemu kama hiyo?

**SPIKA:** Maswali ya aina hiyo kwa kweli hayakubaliki na kanuni zetu za Bunge. Kwa hiyo, Waziri usihangaike kulijibu.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na kutupiana mpira wa madai ya walimu kati ya Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Elimu na kwa kuwa walimu wengi wa shule za misingi wanadai pesa nyingi sana na Mheshimiwa Waziri anasema ni shilingi bilioni moja tu wakati takwimu zilizoko zinaonyesha ni zaidi ya Sh.

18 bilioni.  Je, si wakati muafaka sasa madai ya walimu yote yakashughulikiwa na Wizara moja ya Elimu ili ijulikane nani mhusika hasa?  *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kufafanua kwamba, hakuna lolote la kutupiana mpira katika jambo hili. Waheshimiwa Wabunge, wanafahamu namna mgawanyo wa fedha unavyofanywa na Bunge hili kwa kupitia *Votes.*  Sasa Wizara yangu inasimamia *Vote 46* ambayo ina mishahara ya walimu wa sekondari, walimu wa vyuo vya ualimu na walimu walio katika idara ya ukaguzi wa shule.  Hiyo ni *Vote 46.*  Kwa hiyo, Wizara yangu inajibu maswali yote yanayoendana na *Vote* hiyo na walimu wa shule za msingi kwa utaratibu wa mageuzi ya Serikali za Mitaa, Walimu hao mishahara yao inapita katika *Vote 56.*  Jambo hili mimi nachukulia Waheshimiwa Wabunge wanajua namna ya kufuatilia *Vote,* ila inapojitokeza kwamba mtu unapeleka masuala kule kusikohusika, Serikali tunakabidhiana ndani ya utaratibu.

Serikali haikatai kuwajibika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ndiye anayeongoza kusimamia Wizara zote, ameshatoa kauli hapa Bungeni kwamba inaundwa Tume maalum kuweza kuchunguza suala hili.  Kwa hiyo, uchunguzi ule utafanywa kuhusiana na *Vote* zote mbili.  Kwa hiyo, Serikali inawajibika na jambo hili kwa ukamilifu kwa kufuata taratibu za fedha za Serikali zinazopitishwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Na. 200

**Vijana wanaozurura bila kazi mijini kupelekwa JKT/JKU**

**MHE. ISMAIL J. R. IWAVATTA (k.n.y.  MHE. MGANA I. MSINDAI)** aliuliza:-

Kwa kuwa mpaka sasa wapo watoto wengi sana wanaokaa Mijini bila kazi ambao wamezaliwa na wazazi ambao ni ombaomba na kwa kuwa wakiwa wadogo baadhi yao huwaongoza wazazi wao wasioona kuzunguka Mijini wakiomba, lakini watoto hao wakishafikia umri mkubwa huacha kazi hiyo na kujiingiza kwenye vitendo vya ukahaba, ujambazi na kadhalika, kutokana kukosa kazi.

Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati wa kuwachukua vijana hao na kuwapeleka kwenye Kambi za JKT/JKU ili wakafundishwe Kilimo, Ufundi na Ulinzi, hatimaye wapewe maeneo ili waanzishe shughuli za uzalishaji mali, wajitegemee na kusaidia kukuza uchumi kwa mambo mema watakayokuwa wakifanya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI (k.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana, Sera ambayo lengo lake kuu ni kuwaendeleza vijana wote wa Taifa hili. Sera hiyo ni pana na inajumuisha sekta na taasisi mbalimbali za binafsi na Serikali ikiwemo Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, baada ya JKT kurejeshwa upya mwaka 2001, imeanza kutekeleza jukumu lake la kuwaandaa vijana kufuatana na sera ya maendeleo ya vijana kwa kutoa malezi mazuri kwa vijana na kuwaandaa wawe raia wema, wazalendo na wanaoithamini na kuipenda nchi yao. Malengo mengine ya JKT ni kuwawezesha kujitegemea, kuwapa vijana mbinu za kijeshi ili wawe tayari kulihami Taifa kwa kuwa walinzi wa wananchi, mali zao na mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utaratibu wa uchukuaji wa vijana wa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati za Ulinzi na Usalama ngazi za Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya na Mikoa, ndizo huhusika moja kwa moja katika kupokea maombi ya wanaotaka kujiunga na JKT, kuchuja maombi hayo na uteuzi wa vijana hao. Jeshi la Kujenga Taifa halihusiki moja kwa moja na uchukuaji vijana kutoka Vijijini wala Mitaani. Kuhusu watoto wa mitaani, kimsingi huhudumiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa kushirikiana na mashirika kadhaa yasiyokuwa ya Kiserikali, wameweza kuwachukua baadhi ya vijana hao wa mitaani na kuwapa mafunzo mbalimbali ambayo yamewezesha baadhi ya vijana hao kupata elimu ya sekondari na vyuo mbalimbali na hatimaye wamekuwa raia wema wanaoishi kwa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, itashirikiana na Wizara mbalimbali zinazohusika na malezi ya watoto wa mitaani ili kuweka utaratibu unaofaa wa namna ya kuchukua baadhi ya vijana na hasa wale wenye sifa za kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kulingana na taratibu, kanuni na Sheria za JKT zinazohusu kuwachukua vijana kujiunga na Jeshi hilo.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Msindai. Lakini vile vile naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Kwa kuwa vijana wanaokwenda JKT huwa lazima wawe na elimu na huwa maombi yanapokaribishwa wanapanga kabisa darasa la saba wanatakiwa kiasi gani, kidato cha nne wanatakiwa kiasi gani na kidato cha sita kiasi gani na kwa mujibu wa swali la mwuliza swali ni kwamba, hawa vijana anaowazungumzia Mheshimiwa Msindai ni wale ambao bahati mbaya shuleni hawakwenda, walikuwa wanasaidia wazazi wao ambao hawaoni, kupita mitaani na kuomba. Lakini vile vile namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake...

**SPIKA:** Sasa uliza swali la nyongeza.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu huu utaratibu wa kuwachukua hawa vijana ambao ni wa mitaani unafanywa na Serikali katika baadhi ya Miji tu, sasa je, Serikali inaweza ikafanya ukawa ni utaratibu katika Wilaya zote ili vijana wote wa namna hii waweze kufaidika kupata elimu na baadaye waweze kulisaidia Taifa hili kwa kuwa raia wema? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ni mzuri na Wizara inayoshughulika na hawa watoto wa mitaani, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ina lengo la kuratibu vituo vya kulea watoto hawa ambavyo vimesambaa karibu katika Mikoa yote. Kwa hiyo, kwa utaratibu huo tuna imani kabisa Wizara inayohusika, itatusaidia kuratibu wale vijana ambao wana sifa na sifa za JKT zaidi ya uraia tunachukua mpaka darasa la saba, Majeshi mengine yanachukua kuanzia *form four,* lakini JKT ili iweze kuwachukua vijana wote wa aina mbalimbali inachukua hata darasa la saba. Kwa hiyo, nina imani kabisa ushauri wa Mheshimiwa Mbunge utazingatiwa kwa sababu vituo hivyo vipo kwenye Mikoa yote na Wizara inayohusika itaratibu Mkoa gani, kuna vijana gani wenye sifa hizo, tuko tayari kuwachukua kama tulivyosema katika jibu letu la msingi. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni kweli Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, wanashughulikia suala la watoto wasio na uwezo au hawana mahali pa kutunzwa. Lakini lipo tatizo kwamba watoto hawa kama ilivyoelezwa katika swali la msingi, wanatembea na wazazi wao na bahati mbaya hakuna anayewajibika kusema kwamba labda huyu achukuliwe aende shuleni. Je, sasa ni jukumu la nani kwamba watoto hawa wakusanywe na wapelekwe shuleni, tatizo ni kuwakusanya na kuwapeleka shuleni, ni jukumu la nani, Serikali inaweza kujibu hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hao watoto wanaotembea na wazazi wao, jukumu la kuhakikisha kwamba wanakwenda shule, kusema kweli ni jukumu la Serikali za Vijiji na Mitaa na ipo sheria ya *Compulsory Enrolment,* ipo sheria ya kulazimisha kila mtoto aliyefikia umri wa kwenda shule aende shule na Serikali za Vijiji, Serikali za Kata, pamoja na sisi Wabunge, kusema ukweli tushirikiane kutekeleza hii sheria ili hawa watoto waende shule na wale ambao wana mazingira magumu hizi Wizara nilizozitaja zinawahudumia. Kwa hiyo, kusema kweli utaratibu upo mzuri tu wa kuwashughulikia watoto hawa, tushirikiane kuutekeleza huo utaratibu tuliojiwekea.

Na. 201

**Aina ya Bunduki na Matumizi Yake**

**MHE. MARIA D. WATONDOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa kila mwananchi anayo haki ya ulinzi na kujilinda na kwa kuwa bunduki ni moja kati ya silaha muhimu za ulinzi na kwa kuwa zipo bunduki za aina mbalimbali:-

(a) Je, ni bunduki za risasi ngapi na ni za kiraia au kivita anazoruhusiwa mwananchi kuwa nazo?

(b) Je, ni chombo gani kina mamlaka ya kuamua aina ya bunduki ambayo mtu au shirika wanastahili kununua?

*(Mwuliza swali tajwa hapo juu alilifanyia marekebisho swali lake kwenye kipengele (a)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu kama lilivyoletwa kwako.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujbu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, kila raia anayo haki ya ulinzi na kujilinda na kwamba bunduki ni moja ya aina ya silaha ambazo mwananchi anaruhusiwa kuzimiliki. Aina ya bunduki ambazo mwananchi anaruhusiwa kuzimiliki ni bastola, *rifle* na *shotgun.* Silaha hizi hazimo katika kundi la silaha za kivita. Silaha hizo huruhusiwa kumilikiwa na raia kwa ajili ya kujilinda binafsi, mali zake pamoja na uwindaji wanyama wa porini. Bunduki hizo pamoja na risasi zake hutolewa kama ifuatavyo:-

- Mwananchi anaruhusiwa kumiliki bastola moja na kwa mwaka inaruhusiwa kuwa na risasi 25 kwa ajili ya kujilinda binafsi, *Shotgun* moja na kwa mwaka mmiliki anaruhusiwa kuwa na risasi kati ya 200 na 500 kwa ajili ya kulinda mali zake na mazao na *Rifle* moja, mmiliki huyo anaruhusiwa kuwa na risasi 50 na zisizidi 200 kwa mwaka kwa ajili ya kuwindia.

Mheshimiwa Spika, aidha, raia anaruhusiwa kumiliki silaha moja au zaidi kulingana na matumizi yaliyoainishwa hapo juu. Jeshi la Polisi ndicho chombo chenye mamlaka kisheria ya kuamua aina ya bunduki ambayo mtu binafsi au shirika linaweza kumiliki.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongeza kidogo juu ya yaliyojibiwa hasa kutokana na marekebisho ya swali lake ambayo kidogo yalikuwa ni marekebisho ya msingi. Kimsingi bunduki inayoruhusiwa kwa raia ni ile ambayo inapiga risasi moja moja inaweza ikawa na risasi tano, kumi au ishirini lakini inapiga moja moja siyo automatic. Nadhani hapo hasa ndipo ilipo tofauti kati ya zinazoruhusiwa kwa raia na za kijeshi. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza na nashukuru kwa majibu ya nyongeza ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na majibu mazuri, je, Shirika la Umma kama Shirika la Wanyamapori ambao wafanyakazi wake wanafanya kazi misituni wanahitaji kujilinda na wanyamapori na kupambana na majambazi, hawana haki ya kupata silaha *automatic* ili waweze kulinda maliasili za Taifa hili na kujilinda wao wenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa vita vya kisasa vimebadilika kabisa na silaha kama *AK 47* si silaha ya kivita, Serikali haioni kwamba katika kuendelea kusema silaha *automatic* ndiyo silaha za kivita inawanyima haki ya kujilinda raia hasa wanaofanya kazi misituni? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, wale Askari wa *Game* kimsingi kazi wanayoifanya siyo kazi ya kivita ni kazi ya ulinzi kule porini. Kwa hiyo, mpaka sasa hatuwapi silaha za kivita, lakini inapotokea hali ya huko porini ikageuka kuwa ya kivita kama ilivyowahi kutokea kule Ngorongoro ambapo kule msituni kulikuwa na watu wenye silaha kali, katika mazingira hayo ndipo Askari wa *Game* wanapewa silaha kama hizi na tunaongezea nguvu. Mtakumbuka kule Ngorongoro tulipeleka Jeshi la Wananchi na Polisi kuungana na wale Askari wa *Game* katika kupambana. Hiyo ilikuwa ni hali maalum, kwa hiyo, katika hali maalum, tunaruhusu silaha za kivita, lakini katika hali ya kawaida, wana silaha za kawaida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *AK 47,* hii ni silaha ambayo inapiga risasi za mfululizo. Kwa hiyo, hii mpaka sasa bado ipo katika kundi la silaha za kivita na haturuhusu raia wa kawaida aipate. *(Makofi)*

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa raia wengine wanaomiliki bunduki na bastola wanapatwa wakati mwingine na hasira ya kuweza kuua wake zao au wanapatwa wazimu na kuweza kuua watu na wenzangu wananiambia pia na kuua waume zao. Pamoja na hivyo, je, Serikali imetoa nafasi gani kwa watu kama hao wanaomiliki kabla hawajanunua kuweza kupewa elimu thabiti kabisa ya kuwaelekeza ili waachane na kufanya matatizo kama hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mara chache inatokea mume akatumia bastola kumuua mke au mke akatumia bastola kumuua mume. Nasema haya ni matukio ya nadra sana na ya bahati mbaya sana. Lakini kimsingi kabla Mtanzania yeyote hajamilikishwa silaha kwa upande wa bara maana yake kule upande wa Tanzania Zanzibar, hiyo ruhusa mpaka sasa bado haipo. Huku bara ambako ipo hiyo ruhusa huyu mtu anayeomba lazima kwanza ajadiliwe kuanzia kwenye Kijiji chake, watamjadili tabia yake, kiwango chake cha hasira, ulevi, wanamjadili kwa undani baadaye atakwenda kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kata, baadaye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, baadaye kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa. Sasa huku akigundulika huyu mtu ana hasira za karibu karibu hapewi. Yaani moja ya kigezo ni je, hasira zake ni za kiwango gani, wale wenye hasira za karibu karibu hawamilikishwi silaha. Kwa hiyo na hata baada ya kupewa silaha

hizo vilevile hao wamilikaji tunawapa maelezo ya kutosha kwa matumizi ya silaha zile, jinsi ya kuzitunza na sheria zake. Kwa kweli sheria ya kumiliki ni kali sana na mmliki akikosea kidogo adhabu yake ni kali vilevile. *(Makofi)*

Na. 202

**Kupanda kwa Bei ya Mafuta**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Machi - Mei, 2004 bei ya bidhaa za mafuta zimepanda kwa kiasi kikubwa kutoka wastani wa fedha za Kitanzania Sh.650/= hadi Sh.850/= kwa lita:-

(a) Je, huko kupanda kwa bei ya mafuta kumeleta madhara gani katika uchumi?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kupunguza makali ya madhara yanayotokana na kupanda kwa bei ya mafuta?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida ya uchumi wa soko uliopo nchini, bei ni matokeo ya hali halisi ya mahitaji na upatikanaji wa bidhaa, yaani *demand and supply.* Hata hivyo, hali halisi siyo pekee inayochangia mwenendo wa soko mbali pia mtazamo na imani na mazingira ya kisiasa.

Mwenendo wa biashara ya Kimataifa unaambatana sana na hali ya kisiasa duniani hususan mazingira ya amani au vita. Amani huzaa imani na vita siyo tu huleta maafa, uharibifu wa mali na kupoteza nafasi ya kufanya kazi nyingine, bali pia huzusha hofu na kutoweka kwa imani na hii ndiyo hali ya biashara ya mafuta duniani kwa hivi sasa. Vita inayoendelea nchini Iraq na hali ya mashambulizi nchini Saudi Arabia na wale wanaoipinga Serikali ya nchi hiyo kumepoteza imani juu ya upatikanaji mafuta katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya mgogoro ama wa ndani au wa Kimataifa, wafanyabiashara wanaotoa huduma au bidhaa, hupata changamoto ya namna ya kugawa gharama zinazotokana na hali hiyo ya kivita. Kuna mbinu mbili, ama kupunguza faida ya wenye mali na hivyo kushusha imani ya uwekezaji katika biashara husika au kuongeza bei kwa mlaji ambayo inaweza kukimbiza wanunuzi kama kuna bidhaa mbadala. Kwa kuwa bidhaa ya mafuta haina mbadala, wafanyabiashara hukimbilia kuongeza bei ili kukabiliana na gharama za kupanda kwa huduma kama vile Bima. Hali hii imejitokeza

sambamba na *OPEC* kupunguza uzalishaji kuanzia mwezi Aprili, 2004 kwa asilimia 4.25 na matumizi ya mafuta kuongezeka kwa asilimia 9 katika nchi zenye uchumi unaokua kwa kasi kama vile Uchina.

Mheshimiwa Spika, bei ya mafuta katika soko la dunia imepanda kutoka dola za Kimarekani 32 kwa pipa miezi minne iliyopita hadi kufikia dola 42 hivi karibuni. Kupanda kwa bei duniani kumesababisha ongezeko kubwa la bei ya mafuta hapa nchini. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Desemba, 2003 hadi Aprili 30, 2004, bei zilipanda kwa asilimia 14.67 kwa dizeli, asilimia 25.54 kwa petroli na asilimia 18.44 kwa mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafuatilia kwa karibu athari za kupanda kwa bei ya mafuta katika uchumi. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa madhara ambayo yamejitokeza ni pamoja na mfumko wa bei za chakula, ongezeko la gharama za uendeshaji katika sekta mbalimbali ikiwemo uzalishaji umeme kwa kutumia mafuta.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa mujibu wa taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania, mfumko wa bei ya chakula ulipanda kutoka asilimia 4.3 mwezi Juni, 2003 hadi kufikia asilimia 8.8 mwezi Aprili, 2004, mfumko huu ulichangiwa na kupanda kwa bei ya usafirishaji na kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Mei, 2004, Wizara ya Nishati na Madini, ilitoa taarifa rasmi kwa wananchi juu ya sababu za kupanda bei ya mafuta na kuwashauri wawe makini katika matumizi ya mafuta. Aidha, Serikali imekuwa ikifuatilia kwa makini kupitia Kamisheni ya Ushindani wa Haki *(Fair Competition Commission),* kuhakikisha kuwa Makampuni ya mafuta yanafuata taratibu za biashara huru na kwamba makampuni hayo hayachukui mwanya wa kuongezeka kwa bei katika soko la dunia kujinufaisha. Kwa mfano, tarehe 21 Mei, 2004, tuliarifiwa kuwa wafanyabiashara wa mafuta wa Mkoa wa Mwanza walikutana na kupanga bei. Kutokana na taarifa hizo, Wizara iliwasiliana na Kamishna wa Ushindani, ambaye naye baada ya uchunguzi alichukua hatua.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwataka wananchi waifahamishe Serikali pale wanapoona kuwa wafanyabiashara wa mafuta wanakiuka maadili ya kanuni za uchumi wa soko. Aidha, napenda kutoa onyo kwa wafanyabiashara wa mafuta kuwa ni marufuku kupanga bei kwa pamoja na Serikali itachukua hatua kali kwa yeyote atakayethibitika kutumia mwanya wa hali ya kupanda kwa bei ya mafuta duniani kujinufaisha isivyo halali.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa nchi zote duniani huhakikisha zinadhibiti kwa karibu mwenendo wa bei ya mafuta; na kwa kuwa baadhi ya nchi tumeshuhudia zikienda vitani ili kuhakikisha zinalinda maslahi yake kuhusiana na mafuta; kwa nini sasa Serikali yetu

imeamua kuondoa mikono yake moja kwa moja na kuachia soko la mafuta kuwa soko holela badala ya kuwa soko huria?

La pili, kwa kuwa Serikali wakati fulani ilisema inaandaa sheria itakayodhibiti biashara ya mafuta na kwa kuwa Bunge hili tayari lilishatunga sheria mbalimbali za kudhibiti biashara kwa ujumla. Je, sheria mpya itakayokuja inayolenga mafuta, ina tofauti gani na hizi sheria zilizopo zinazotakiwa kudhibiti hali na mwenendo wa biashara? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali haijaachia biashara ya mafuta iwe biashara holela. Kama nilivyotoa mfano wakati najibu swali la msingi, nimetoa mfano wa wafanyabiashara ambao wamekuwa wakikutana na kupanga bei, nikatoa mfano wa wafanyabiashara wa Mkoa wa Mwanza. Lakini pia pametokea mifano mingine katika Mkoa wa Dar es Salaam ambapo Mkuu wa Mkoa baada ya kugundua kwamba wafanyabiashara wamekaa na kupanga bei akatoa katazo kuhusu upangaji wa bei.

Mheshimiwa Spika, pia hapa Bungeni pamepitishwa Sheria ya kuunda chombo maalum chenye jina la *EWURA* na tunatarajia kwamba chombo hiki kitakapoanza kufanya kazi, suala la udhibiti wa Sekta hii utakuwa kamilifu zaidi. Lakini kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge yeye mwenyewe amesema, Serikali inaandaa sheria ya mafuta na nadhani ningemwomba tusubiri mpaka wakati sheria hiyo itakapokuwa tayari na kuletwa Bungeni kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge kuipitisha tuone kuna tofauti gani baina ya sheria hiyo na vyombo vingine hivi ambavyo vimeundwa kwa ajili ya udhibiti wa sekta hii ya mafuta.

Na. 203

**Ukosefu wa Umeme Mkoa wa Mtwara**

**MHE. LYDIA T. BOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa jambo kubwa linalowakera Wananchi wa Mkoa wa Mtwara Mjini/Vijijini pamoja na Mji Mdogo wa Nanyamba na Vijiji vya Wilaya hizo na Shule za Sekondari ni la ukosefu wa umeme:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi za kutoyapatia maeneo hayo umeme tangu tupate uhuru hadi sasa?

(b) Je, ni vigezo/mbinu gani zinazotumika katika karne hii ambapo baadhi ya Mikoa iko kwenye hatua za kufikisha umeme kwenye Kata wakati kuna Mikoa/Wilaya nyingine bado hazijapata umeme kama ilivyo kwa Mkoa wa Mtwara?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lydia Boma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara unapata huduma ya nishati ya umeme itolewayo na Shirika la Umeme Tanzania kwa kutumia mashine zinazoendeshwa kwa kutumia mafuta ambapo Wilaya ya Mtwara, Tandahimba, Newala na Masasi, zote zimekwishapata umeme.

Kwa kuwa suala la kufikisha huduma ya umeme kwa wananchi wote kwa mara moja haliwezekani kutokana na ukosefu wa fedha, Serikali inalenga kusambaza umeme hatua kwa hatua na lengo kuu kwa sasa kama ambavyo tumesema mara nyingi ni kufikisha umeme katika Makao Makuu ya Wilaya na sehemu nyingine ambazo ziko karibu karibu na miundombinu ya umeme. Kwa kuzingatia lengo hilo, Mkoa wa Mtwara ni miongoni mwa Mikoa ambayo Makao Makuu ya Wilaya zake zote yamepata umeme, wakati ambapo bado tuna Wilaya 18 katika Mikoa mingine ambazo bado hazijapata umeme.

Mheshimiwa Spika, sababu za msingi za kutoyapatia umeme maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge kwa kweli ni ukosefu wa fedha. Serikali inafanya kila jitihada ya kuona kwamba inafikisha huduma ya umeme kwa wananchi hatua kwa hatua fedha zinapopatikana. Napenda kutoa taarifa kwamba, kazi ya awali ya kupima njia ya umeme kutoka Tandahimba ambako kuna umeme hadi Nanyamba ilikwishafanywa na *TANESCO.* Inakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi milioni 353 zitahitajika kufikisha umeme katika Mji Mdogo wa Nanyamba uliopo kama kilomita 23 kutoka Tandahimba.

Kama nilivyoeleza hapo awali, vigezo vinavyotumika ni kufikisha umeme katika Makao Makuu ya Wilaya na maeneo mengine kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, huo umeme anaosema kwamba tayari wanaandaa utapatikana lini? *(Makofi)*

La pili, kwa kuwa tulipewa semina na Ofisi ya Waziri Mkuu ikieleza jinsi ya kufunga Tovuti na hizi Tovuti mimi kwa uelewa wangu mdogo ni kwamba huwezi kuzifunga bila kuwa na umeme. Sasa wananchi wema wa Mkoa wa Mtwara, zikiwemo shule za sekondari ambazo zinakosa umeme kama Nanyamba niliyoanza kuitaja, Kitangari, Mnyambe na sekondari nyingine wanatumia vibatari na kandili, ni lini hawa sasa watapata umeme ili waweze kufunga *Internet? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu lini umeme utafika huko jibu nilishalitoa katika jibu la msingi kwamba, tutakapopata fedha tutafikisha umeme huko.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Serikali ina nia thabiti ya kuhakikisha kwamba, maeneo mengi ya vijijini na maeneo mengine yanapatiwa umeme. Ndiyo maana basi

kuna huu mpango wa kuanzisha Taasisi ya kusambaza umeme vijijini *(Rural Energy Agency)* na pia *Fund* maalum ya kusambaza umeme vijijini yaani *Rural Energy Fund.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo pia kama ambavyo tumeshawahi kutoa taarifa hapa Bungeni, nina imani wananchi wa Mkoa Mtwara na Mkoa wa Lindi watakuwa na umeme wa kuaminika zaidi na unaoenda katika maeneo mengi baada ya mradi wa umeme wa Gesi ya *Mnazi Bay* kukamilika.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri amesema tatizo ni ukosefu wa fedha. Kwa nini basi Serikali isijiwekee utaratibu mwingine wa kuandaa angalau bajeti au makisio ya kila mwaka angalau kuweka vifaa kidogo kidogo ili wananchi wa maeneo tajwa na swali la msingi wawe na matumaini na Serikali yao kwamba na wao siku moja watapatiwa umeme? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali yenyewe huwa inaandaa mpango wa kusambaza umeme katika Makao Makuu ya Wilaya na vijijini na pia kupitia Shirika la Ugavi wa Umeme Nchini *(TANESCO)*. Ndiyo maana mwaka hadi mwaka huwa tunakuja hapa Bungeni wakati wa hotuba za bajeti kuelezea katika mwaka fulani ni maeneo gani yamepatiwa umeme, hii isingewezekana kama kungekuwa hakuna mpango mahsusi.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa MheshimiwaWaziri aliahidi mwenyewe kwamba, umeme ukiwaka Tandahimba utawaka pia na Nanyamba. Je, leo anawaeleza nini watu wa Nanyamba juu ya hili maana umeme umewaka Tandahimba na Nanyamba haujawaka? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Tumieni mkaa!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba, katika miaka ya nyuma, Serikali iliwahi kuahidi kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge na iliahidi kwa matarajio kwamba, upatikanaji wa fedha ungeweza ukakamilisha kazi hiyo kama taarifa ilivyotolewa wakati ule.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwafahamisha Wananchi wa Nanyamba, kwanza, ni kwamba Mbunge wao Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, ameshafanya ile kazi ya ushenga na waswahili wanasema mshenga hauawi. Amefanya kazi ya kufuatilia suala hili Serikalini mara kwa mara na si kosa lake yeye ndiyo sababu mpaka sasa hakuna umeme pale Nanyamba, lakini ukosefu wa umeme unatokana na hali ya kifedha na kama ambavyo tumeahidi mara tu fedha zitakapopatikana basi umeme utafika Nanyamba. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 204

**Uendelezaji wa Michezo Nchini na Viwanja vya Michezo**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO (k.n.y. MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inayo mipango mizuri ya kukuza michezo katika nchi hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa viwanja vizuri na vya kisasa vya michezo vyenye vipimo sahihi vinavyokubalika Kitaifa/Kimataifa, kuwa na wachezaji wenye vipaji vinavyoendelezwa kwenye michezo mbalimbali watakaohimili ushindani wa Kitaifa/Kimataifa pamoja na kuwa na vyama mbalimbali vya michezo katika ngazi za Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa hadi Taifa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuviendeleza viwanja vya michezo vilivyopo hapa nchini ambavyo vingi vilijengwa kwa lengo la kukidhi tu sherehe bila kujali vinamilikiwa na nani kwa manufaa ya wanamichezo wa Tanzania?

(b) Ili kuwa na vyama vya michezo kwenye ngazi nilizozitaja, je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na Maafisa Michezo wa Wilaya na Mkoa?

(c) Kwa kuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni haihusiki tena na michezo; je, Serikali ina mpango gani wa kukuza vipaji vya michezo kwa watoto walioko katika shule za msingi, sekondari na vyuo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa na itaendelea kuendesha na kutoa mafunzo kwa waendeshaji wa Viwanja vya Michezo kuhusu namna bora ya kutunza viwanja hivyo. Mafunzo hayo ikiwa ni pamoja na ushauri wa kitaalamu, yamekuwa yakitolewa na yataendelea kutolewa kwa mameneja na wamiliki wa Viwanja vya Michezo mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Serikali haina mpango wa kuwa na Maafisa Michezo wa Mikoa. Hata hivyo, nafasi za Maofisa Michezo za Wilaya zipo katika Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa. Aidha, Serikali imeshatoa mwongozo wa kufuata katika kuajiri Maofisa Michezo katika Wilaya. Hata hivyo, kutokuwepo kwa Maofisa Michezo wa Mikoa au Wilaya siyo kigezo cha uanzishwaji au kutoanzishwa Vyama vya Michezo katika ngazi hizo. Uanzishwaji wa Vyama vya

Michezo katika ngazi hizo kunategemea zaidi utashi wa wadau wenyewe wanaotaka kuanzisha chama katika ngazi husika na siyo utashi wa Afisa Michezo Wilaya au Mkoa.

(c) Mheshimiwa Spika, siafiki maelezo ya Mheshimiwa Hashim Saggaf kuwa, Wizara ya Elimu na Utamaduni haihusiki na michezo. Wizara hiyo, inayo mitaala ya kufundishia somo la michezo na pia wanaruhusiwa kucheza katika ngazi ya shule ili mradi tu isiingilie muda wa vipindi vya masomo mengine.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imejikita zaidi katika uendeshaji wa michezo nje ya shule hususan ile inayosimamiwa na Vyama vya Michezo vya Kitaifa.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Pamoja na majibu haya mazuri ningependa kujua kwa nini Serikali hadi hivi sasa ina kigugumizi cha kushiriki kikamilifu katika masuala ya michezo kama zinavyofanya nchi nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba, Serikali ina kigugumizi katika kushiriki kwenye michezo. Tunaendelea kushirikiana na ratiba za vyama vya michezo ambazo zinatufikia. Ndiyo maana hata vijana ambao wanakwenda kwenye Olimpiki mwezi Agosti, 2004, wanasafirishwa na Serikali hii ambayo haina kigugumizi. Kwa hiyo, sielewi kigezo cha kigugumizi anachokizungumza Mheshimiwa Mbunge ni kipi. Lakini kwa chama ambacho hakipo tayari kushirikiana na Serikali, Serikali haiwezi ikakilazimisha kwa sababu Chama kina wenyewe kwa mujibu wa Katiba zao.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri ya kutoa mafunzo kwa waendeshaji wa viwanja, lakini pamoja na mafunzo hayo hakuna kitu kizuri kilichoonekana. Je, sasa Serikali iko tayari kukaa na hao waendeshaji wa viwanja ili viwanja hivyo vibinafsishwe?

**SPIKA:** Ni swali jipya. Mheshimiwa Naibu Waziri hana majibu.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka kujua kwa kuwa sisi wote ni mashahidi, michezo ni moja ya ajira kubwa kabisa zinazowapatia wananchi hasa wanamichezo wanaojua kucheza mpira wa miguu, kipato kikubwa kabisa cha kujiendeleza wao wenyewe. Sasa Serikali kwa nini isisaidie katika kuboresha michezo hii katika shule zetu kwa kuweka kipindi maalum cha michezo kikarejeshwa kama zamani katika vile vipindi vya *P.E.* ili vijana wetu kuanzia shule za msingi hadi kuendelea Chuo Kikuu waweze kuielewa michezo hiyo ili hata watakapokosa ajira nyingine basi michezo iwe moja ya ajira zao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, mpaka hivi sasa Serikali haijaondoa vipindi vya michezo katika shule zetu za msingi, sekondari mpaka vyuoni. Mabadiliko haya yametokea tu baada ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kutoa maagizo kwamba, michezo iendeshwe bila kuvuruga ratiba ya masomo mengine. Sasa mkanganyiko huu unapelekea watu kuamini kwamba, michezo katika shule zetu imeondolewa, bado michezo ipo siyo ndani ya shule tu, hata shule na shule kukutana katika Kata, katika Kijiji ilimradi michezo ifanyike bila kuingilia vipindi vingine wanaweza wakatumia siku ya Jumamosi na Jumapili. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuwasisitize walimu wetu waendeleze michezo wasitafute visingizio juu ya hili. *(Makofi)*

Na. 205

**Ujenzi wa Uwanja wa Taifa**

**MHE. HADIJA K. KUSAGA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2003/2004 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kuanza Ujenzi wa Uwanja wa Taifa wa kisasa na kwa kuwa Serikali iliahidi kwamba ujenzi huo ungeanza rasmi mwezi Novemba, 2003 lakini jambo la kusikitisha ni kwamba hadi sasa bado ujenzi huo haujaanza na hakuna dalili zozote za kuonyesha kuanza kwa ujenzi huo:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa ililidanganya Bunge pamoja na Taifa kwa ujumla?

(b) Kama jibu kwenye sehemu (a) ya swali hili ni 'sivyo' je, Serikali inasema nini kuhusu kuanza kwa ujenzi huo?

(c) Kutokana na kusuasua kwa kuanza ujenzi wa uwanja huo; je, Serikali haioni kuwa itakuwa imekwamisha uamuzi mzuri na azma ya Mheshimiwa Rais ya kuukabidhi uwanja huo ukiwa tayari umekamilika ifikapo tarehe 25 Mei, 2004?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mbunge wa Temeke, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sikubaliani na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ililidanganya Bunge na wananchi kuhusu suala la ujenzi wa uwanja. Ujenzi wa uwanja upo pale pale.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa uwanja wa kisasa utaanza mara tu Bunge lako hili Tukufu litakapoidhinisha fedha za ujenzi huo.

(c) Azma ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na uwanja wa kisasa wa michezo iko pale pale. Kinachofanyika sasa ni kuwa na mpango madhubuti na endelevu wa kuweka msingi wa upatikanaji wa fedha na mgawanyo wake kulingana na mahitaji ya ujenzi bila ya kusimama, kuwa na michoro ya ujenzi tarajiwa, yenye kiwango chenye ithibati ya Kimataifa .na kukamilisha shughuli za utafiti wa kijiologia, upimaji na upembuzi yakinifu wa udongo katika kuhimili ujenzi na uzito wa jengo linalokusudiwa pamoja na athari za ujenzi huo katika eneo husika. Ni mategemeo yangu kwamba, maandalizi ya kisayansi ya aina hii Serikali inayofanya ndiyo yanayohitajika yakiwa sehemu muhimu sana ya awali ya ujenzi unaokusudiwa kujengwa, ili uendelee kujengwa bila kusimama kwa mujibu wa ratiba iliyopo.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa hivi karibuni Serikali imewekeana Mkataba wa ujenzi wa Uwanja wa Taifa na Serikali ya China. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akaliambia nini Bunge hili Tukufu pamoja na Taifa kwa ujumla Mkataba huo unasemaje?

(b) Kwa vile imekubalika kuwa uwanja huo wa Taifa wa kisasa utajengwa Wilayani Temeke. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atawasaidiaje vijana wa Temeke wakati uwanja huo utakapokuwa unajengwa waweze kupata ajira za muda ili waweze kujikwamua na tatizo la ajira?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, Mkataba ni mrefu lakini kwa ujumla umebeba mambo makubwa yafuatayo: Mkataba unaeleza tutajenga kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na ya Uchina uwanja wa kisasa utakaokuwa na uwezo wa kuchukua watu 60,000. Kati ya gharama za ujenzi huo wa dola za Kimarekani milioni 56. 4, Serikali ya Tanzania italipa dola za Kimarekani milioni 23, China itagharamia vifaa vya ujenzi, mitambo, wataalamu na ujenzi wa uwanja wenyewe. Tanzania itahusika na uchunguzi wa kijiologia, kutoa taarifa za msingi za ujenzi, ramani, eneo la ujenzi, maji, umeme, mahitaji ya msingi ya kila siku kwa wataalam wa Kichina watakapokuwepo hapa, kutoa *Visa* na kibali cha kufanyia kazi nchini pamoja na kushughulikia suala la kodi kwa vifaa na mitambo vitakavyoingizwa nchini kutoka China. Mwisho, tunatarajia ujenzi huu utaanza mwezi Septemba, 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli uwanja utajengwa katika Wilaya ya Temeke, lakini si jambo linalowezekana kwamba vijana wa Temeke pekee ndiyo watahusika katika kujenga. Tutakuwa tunawafikiria vilevile na uwezo wao na utaalamu walionao, lakini ni vijana wetu watatumika kwa sababu idadi ya Wachina waliokuja ni ndogo sana. *(Makofi)*

Na. 206

**Uchapishaji wa Noti Mpya**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inabadilisha/kuchapisha noti mpya za fedha mara kwa mara kama ilivyofanya hivi karibuni:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza sababu za msingi za kubadilisha/ kuchapisha fedha hizo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuchapisha noti za kudumu kama ilivyo kwa dola ya Kimarekani ili kuepuka gharama?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, napenda kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Serikali nyingi duniani huchapisha noti za nchi zake kwa kuzingatia sera inayokubalika Kitaifa. Nchi nyingi huchapisha noti na sarafu zilizo na picha za kiongozi aliyepo madarakani na nyingine hutumia picha za viongozi au watu maarufu wa zamani wa nchi zao. Kwa mfano, fedha za dola za Marekani hutumia picha za viongozi wa zamani, wakati Uingereza kwenye fedha yake ya paundi hutumia picha ya watawala wa Kifalme waliopo madarakani kama ilivyokuwa kwa Mfalme George mpaka alipofariki na kurithiwa na Malkia Elizabeth II, ambaye kwa kuwa bado yupo madarakani fedha ya paundi inayo picha yake. Aidha, matukio makubwa yanayostahili kukumbukwa, mabadiliko ya teknolojia na tatizo la noti bandia, ni sababu nyingine zinazofanya Serikali kote duniani kubadili fedha zake mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania, kupitia Benki Kuu, imekuwa ikichapisha fedha zake kwa kutumia picha ya Rais aliyepo madarakani tangu mwaka 1965 hadi mwaka 1995. Baada ya hapo, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, hakutaka picha yake iwekwe kwenye fedha zetu. Hivyo, Benki Kuu ilitoa toleo la noti zenye picha ya Twiga. Noti hizi zilikuwepo kwenye mzunguko hadi mwezi Februari, 2003.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya teknolojia, hasa kwenye eneo la mashine za kurudufu nakala *(Photocopiers and Scanners)*, wahalifu walianza kuchapisha noti bandia na kufaulu kuziingiza kwenye mzunguko wa fedha. Ili kupambana na

tatizo hili, Benki Kuu ililazimika kutoa toleo jipya la noti ambazo zilianza kutumika mnamo mwezi Februari, 2003. Toleo hilo jipya lina picha za wanyamapori na majengo ya kihistoria, ili kuenzi na kutangaza utajiri wetu wa maliasili, utamaduni na uchumi. Vilevile, alama nyingine zaidi za usalama na ambazo ni ngumu kughushiwa ama kunakiliwa na mashine za kurudufu ziliongezwa kwenye noti hizo. Aidha, alama hizi za usalama ni rahisi zaidi kutambuliwa na wananchi na hivyo kuwafanya waweze kugundua noti bandia kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kutumika kwa *Automatic Teller Machine (ATM),* katika baadhi ya mabenki hapa nchini ni sababu nyingine iliyosababisha noti zetu kubadilika ili kukidhi mahitaji ya teknolojia hii mpya.

(b) Mheshimiwa Spika, wazo la kuchapisha noti na sarafu za kudumu ni zuri. Hata hivyo, kama nilivyokwishaeleza, mabadiliko ya teknolojia na mapambano dhidi ya uhalifu wa noti bandia wakati mwingine yanalazimisha ubadilishaji wa noti kama ilivyokuwa kwa Marekani na Uingereza miaka ya hivi karibuni. Aidha, baadhi ya noti huwa zinachafuka na kuharibika haraka kutokana na kasi kubwa ya mzunguko wake. Hali hii hulazimisha Benki Kuu, kuziondoa kwenye mzunguko na kuingiza noti mpya pale inapobidi kufanya hivyo. Hivyo, inabidi kuchapisha noti mpya ili kufidia pengo la noti zilizoondolewa.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu yake nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Serikali inapochapisha fedha mpya huwa inapata faida au hasara?

Pili, ikiwa inapata faida ni faida kiasi gani inakwenda Serikali ya Zanzibar au kama inapata hasara ni hasara ya kiasi gani inakwenda katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kuchapisha fedha ni gharama. Hupati faida ya moja kwa moja kwa kuchapisha fedha, inabidi Serikali igharamike ili kuchapisha fedha. Lakini faida inayopatikana ni kwa kukidhi mahitaji ambayo nimeyataja katika jibu langu la msingi kulingana na wakati na teknolojia ya kisasa na pengine kuzuia uhalifu. Kwa hiyo, faida inayopatikana ni kwamba tunakuwa na sarafu, fedha ama noti ambazo zitatumika kwenye uchumi kama *medium of exchange.*

Mheshimiwa Spika, pili, ni kiasi gani cha faida ama hasara kinakwenda Zanzibar na kingine kinakwenda Tanzania Bara. Ni kwamba hii ni nchi moja na kwa hiyo manufaa ama gharama zinazotumika, zinatumika pia kwa pande zote mbili za nchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yamejibiwa na muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, tunaendelea na mambo mengine. Kwa leo sijapata matangazo ya vikao vyote vyote vile, kwa hiyo, sina tangazo la kikao. Isipokuwa ninayo barua ya Mheshimiwa Waziri anayearifu kwamba, hatakuwepo Bungeni. "Natarajia kusafiri kwenda Dar es Salaam kwa shughuli za kikazi tarehe 7 Julai, na kurejea Dodoma tarehe 12 Julai, 2004. Wakati nitakapokuwa sipo, Mheshimiwa Waziri wa Afya ndiyo atakaimu Shughuli za Bunge". *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005
### Wizara ya Elimu na Utamaduni

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, lijadili na kupitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, kuwa Rais wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Dr. Amani W.A. Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Dr. Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani Zanzibar na Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Umoja wa Afrika. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum na pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, kwa kuteuliwa kuiwakilisha Tanzania katika Baraza la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC).* Nampongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira. Pia nawapongeza, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge na Mheshimiwa Danhi Makanga, Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki, kwa ushindi alioupata katika uchaguzi mdogo uliofanyika tarehe 30 Mei, 2004. *(Makofi)*

Napenda kutoa pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu, kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Yte Mwalyego. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Aid, nawapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji), pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Mbunge Viti Maalumu, kwa msiba wa kufiwa na baba yao mzazi. Mheshimiwa Dr. Laurence M. Gama, Mbunge wa Songea Mjini na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kwa kufiwa na watoto wao, pia natoa pole kwa Wabunge wengine waliopata mikasa ya ajali wakati wakija Bungeni - Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii ya mwanzo, kuwapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba yake ambayo imetoa tathmini, mwenendo na mwelekeo wa uchumi wa Taifa kwa jumla na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha, kwa hotuba yake iliyofafanua kwa ufasaha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2004/2005 ambayo imetoa kipaumbele kwa sekta muhimu katika kukuza uchumi ikiwemo Sekta ya Elimu ambayo inao wajibu mkubwa katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini (MKU) na kuboresha ufanisi wa nguvu kazi ya Taifa kwa njia ya elimu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Hotuba yake ya bajeti kwa kufafanua mambo muhimu ya elimu yaliyoamuliwa na Serikali na kwa uamuzi na maagizo yake kuhusu madai ya walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki, kwa kutoa ushauri na maelekezo ya kuboresha Bajeti na utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni baada ya uchambuzi wa kina.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Utamaduni imeendelea kuwa na majukumu yake kama nilivyoeleza katika hatouba ya bajeti ya mwaka 2003/2004. Majukumu hayo ni kusimamia na kuendesha:-

(a) Elimu ya Msingi na Elimu ya Awali.

(b) Elimu ya Sekondari ya Kawaida *(Ordinary Level)*: Kidato cha 1 hadi 4 na Elimu ya Sekondari ya Juu *(Advanced Level)*: Kidato cha 5 hadi 6.

(c) Elimu Maalumu *(Special Education)* itolewayo kwa wenye ulemavu kama vile wasioona, viziwi, wenye ulemavu wa akili na kadhalika.

(d) Elimu ya Watu Wazima *(Adult Education)* ikiwa ni pamoja na utoaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari kwa mfumo usio rasmi kwa watoto na watu wazima walioikosa.

(e) Utamaduni wa Taifa ikiwemo Lugha, Sanaa, Mila na Desturi na Ukaguzi wa Filamu.

(f) Mafunzo ya Ualimu Daraja A na Stashahada *(Diploma).*

(g) Ukaguzi wa Shule katika ngazi zote (Elimu ya Awali hadi Kidato cha Sita) na Vyuo vya Ualimu.

(h) Kupanga na kuratibu mipango yote ya elimu kuanzia Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

(i) Taasisi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara ambayo ni Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), Baraza la Mitihani Tanzania (BAMITA), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa

(BASATA), Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA) na Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu *(ADEM)*.

Katika kutekeleza majukumu hayo Wizara inaongozwa na Sheria ya Elimu Na. 25 ya 1978, Sera ya Elimu na Mafunzo, Sera ya Utamaduni, Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Mkakati wa Kupunguza Umaskini (MKU) na Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2000 ya Chama Tawala cha CCM. Ili kuhakiki ubora wa elimu itolewayo katika shule zote nchini, Wizara huendesha ukaguzi wa shule na hutoa mitihani ya kitaifa ya Darasa la IV, VII, Vidato vya pili, nne na sita na mitihani ya Elimu ya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mipango ya Wizara yangu kwa Mwaka 2003/2004 na malengo ya mwaka 2004/2005 kwa kila Idara, Taasisi na ngazi ya elimu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Msingi inayo Malengo Maalum yafuatayo:-

(a) Kurejesha Elimu ya Msingi kwa Wote *(Universal Primary Education -UPE),* yaani kwa kuwaingiza Darasa la Kwanza kila mwaka watoto wote wa miaka 7 na kuwaendeleza mpaka wahitimu Darasa la VII kwa kuzingatia Kifungu Na. 35 cha Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kama kilivyorekebishwa na Sheria Na.10 ya mwaka 1995.

(b) Kuongeza asilimia ya rika la Elimu ya Msingi (miaka 7-13) waliomo shuleni kutoka 57% mwaka 2001 hadi 95% mwaka 2005.

(c) Kupunguza kasi ya kuacha shule *(Drop Out Rate)* kutoka 6.6% kwa mwaka hadi 3.0 % kwa mwaka ifikapo 2005 katika kila shule.

(d) Kuboresha Elimu ya Msingi kutoka waliofaulu 22 % mwaka 2000 hadi zaidi ya 50% mwaka 2005.

(e) Kuongeza wahitimu wa Darasa la VII wanaoingia Sekondari kutoka 19.5% mwaka 2000 hadi 50% mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004 shughuli za Elimu ya Msingi zimeongezeka ifuatavyo:-

- Shule za Awali zimeongezaka 2,753 kutoka 6,948 hadi 9,701 ambalo ni ongezeko la 39.6%.

- Shule za Msingi zimeongezeka 884 kutoka 12,649 mwaka 2003 hadi 13,533 mwaka 2004 sawa na ongezeko la 7% na Wanafunzi wameongezeka kwa 8% kutoka 6,562,772 mwaka 2003 hadi 7,083,063 mwaka 2004 ambayo vilevile ni 61.6% ukilinganisha na wanafunzi 4,382,410 mwaka 2000 Bunge hili lilipochaguliwa.

- Walimu 14,261 wameajiriwa.

- Wanafunzi 196,273 sawa na 40.1% waliofaulu Mtihani wa Darasa la VII mwaka 2003 wameongezeka kwa 62,599 sawa na 46.8% kutoka 133,674 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Maafisa Elimu,Walimu Wakuu na Walimu wote wa Shule za Msingi kwa mafanikio hayo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2002-2006 ni kama ifuatavyo:-

- Mwaka 2004 watoto 1,368,315 waliandikishwa Darasa la Kwanza sawa na 83.4% ya kulinganisha na lengo la 1,640,969 wakiwemo wavulana 697,594 na wasichana 670,721. Kati yao shule za Serikali zina watoto 1,361,446 na shule binafsi watoto 6,869.

- Jumla ya wanafunzi katika shule za msingi mwaka 2004 ni 7,083,063. ikilinganishwa na 6,562,772 mwaka 2003 ambalo ni ongezeko la wanafunzi 520,291 sawa na 8.0%.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wa rika la elimu ya msingi (miaka 7-13) walioko shuleni *(Net Enrolment Ratio - NER)* imeongezeka kutoka 58.8% mwaka 2000 hadi 90.5% mwaka 2004. Kwa hiyo, malengo yaliyokuwa yamepangwa ya kufikia *NER* ya 77% na *GER* ya 85% yaliyomo katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini (MKU) kwa mwaka 2003 yamevukwa.

Wanafunzi wote shuleni kama asilimia ya idadi ya watoto wa rika lengwa *(Gross Enrolment Ratio - GER),* imeongezeka kutoka 77.6% mwaka 2000 hadi 106.3% mwaka 2004.

Mikoa ya Lindi, Morogoro, Kigoma, Dodoma na Tabora haijafikia kiwango cha *GER* ya asilimia 100 ambayo ni hatua ya lazima ingawa si ya kutosha kabla ya kufikia Elimu ya Msingi kwa Wote.

Walimu 14,261 wameajiriwa hadi 30 Juni, 2004 sawa na asilimia 91.8% ya lengo la walimu 15,533 waliotarajiwa kuwa wameripoti na kuanza kazi.

Walimu Tarajali wanaochukua mafunzo ya Ualimu Daraja A ni 10,788, ikilinganishwa na lengo la mwaka 2004 la wanachuo 10,000. Ruzuku ya Maendeleo ya shilingi 1,185,000,000 imetolewa na Serikali Kuu kwa Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na ununuzi wa madawati. Albaki ya Shilingi 65,742,120,600 ya Ruzuku ya Maendeleo itatolewa wakati wowote kutokana na mchango wa Wahisani ili kukamilisha malengo ya mwaka 2003/2004.

Ruzuku ya Uendeshaji ya shilingi 56,172,632,210 ilitolewa kwa Halmashauri kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya kiada na ziada, penseli, kalamu, chaki na madaftari, vivunge vya sayansi *(Science Kits)*, matengenezo na mitihani ya ndani ya shule na

shughuli za utawala ngazi ya shule. Kiwango hiki ni sawa na shilingi 7,930.55 kwa kila mwanafunzi. Albaki ya shilingi 14,762,862,790 sawa na shilingi 2,069.45 kwa mwanafunzi zitatumwa kwa Halmashauri wakati wowote baada ya kuzipokea kutoka kwa wahisani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, utekelezaji wa miradi mingine ya Elimu ya Msingi uliendelea kama ifuatavyo:-

Mradi wa Lishe Shuleni unaendeshwa kwa ushirikiano na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani *(World Food Programme - WFP)* na utaendelea hadi mwaka 2006 katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Singida na Manyara ambapo wilaya 11 zipo katika mpango huu. Lengo la mpango huu ni kutoa chakula kwa shule za msingi zinazowasomesha watoto wa jamii zinazohamahama kama vile wafugaji, wanaoishi kwa kuwinda, kula matunda na kurina asali.

Wilaya za Mradi wa Lishe Shuleni ni Monduli, Ngorongoro, Simanjiro, Kiteto, Dodoma, Kondoa, Mpwapwa, Singida Vijijini, Iramba, Manyoni na Karatu. Jumla ya shule 230 zinanufaika na mpango huu zikiwemo 10 za bweni na 220 za kutwa. Aidha, jumla ya wanafunzi 99,511 wananufaika na mpango huu. Kati ya hao wavulana ni 52,697 na wasichana ni 46,814.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Shule Zenye Mazingira Yanayomjali Mtoto *(Child Friendly School Project - CFS),* unatekelezwa kwa msaada wa *UNICEF* katika Wilaya 11 zifuatazo: Kisarawe, Masasi, Songea Vijijini, Musoma Vijijini, Ngara, Magu, Mufindi, Hai, Ilala, Kinondoni na Temeke.

Utafiti wa awali *(Baseline Survey)* na majadiliano na Jamii *(Community Dialogue),* ulifanyika na kukamilika katika Wilaya tano za Kisarawe, Masasi, Songea Vijijini, Musoma Vijijini na Ngara. Aidha, uchapishaji wa zana ya upimaji wa utekelezaji wa shule zinazomjali mtoto umekamilika, semina kwa walimu 60 toka Wilaya za Kisarawe na Masasi zimefanyika.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uboreshaji wa Elimu Ngazi ya Kata (UBEKA) au *Ward Based Education Management (WABEM),* unatekelezwa katika wilaya sita zifuatazo: Kisarawe, Masasi, Hai, Musoma Vijijini, Mufindi na Songea Vijijini. Semina za awali katika ngazi ya Kata zilikwishafanyika. Katika gharama za awali mradi ulikadiriwa kutumia Dola za Kimarekani 1,189,553 ambazo zimetolewa kwa uhisani wa *UNICEF.* Kwa makubaliano ya *UNICEF* na Wizara, shughuli hizi zitakwenda kwa pamoja na Mradi wa Shule zenye mazingira yanayomjali mtoto.

Mradi wa Utafiti wa Hali Halisi na Mipango ya Elimu ya Shule *(School Mapping and Micro-Planning),* vilevile, hadi kufikia Juni, 2004 Halmashauri 76 ambayo ni asilimia 64 ya Halmashauri zote nchini zimeshafanyiwa *School Mapping na Microplaning*. Aidha, Halmashauri 16 zimeshaanza kufanyiwa *School Mapping na Microplanning* kuanzia Juni, 2004. Halmashauri zinazofanyiwa *School Mapping* na *Microplaning*

kuanzia Juni, 2004 ni Monduli, Hanang, Kondoa Vijijini, Dodoma Vijijini, Mpwapwa, Ludewa, Same, Kiteto, Ngorogoro, Mbozi, Kwimba, Sengerema, Iramba, Singida Vijijini, Igunga na Urambo.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2003/2004, kutokana na uhisani wa Serikali ya Japan, yamejengwa Madarasa 107, Ofisi za Walimu 9 na Matangi ya Maji 24 na maliwato matundu 107 pamoja na samani yakiwemo madawati, mbao za kuandikia na za matangazo katika shule 15 za Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni. Aidha, ujenzi wa madarasa 250 kwa uhisani wa Japan ulikamilika katika mkoa wa Shinyanga. Shule zilizojengewa Vyumba vya Madarasa Mkoa wa Dar es Salaam ni Boma, Mchikichini, Gongo la Mboto B, Msongola, Mvuti, Kimara B, Uzuri, Mbezi, Mabibo, Mwananyamala B, Azimio, Sokoine, Madenge, Rangi Tatu na Temeke.

Mradi wa Kuzuia Ajira Mbaya ya Watoto kupitia MEMKWA, unaendeshwa kwa ushirikiano na Shirika la Kazi la Dunia, Halmashauri husika na Wizara yangu. Madhumuni ya Mradi huu ni kupunguza ajira mbaya ya watoto kwa kuwapatia Elimu kwa utaratibu wa MEMKWA. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya 11 za Ilala, Kinondoni, Temeke, Mufindi, Iringa Vijijini, Simanjiro, Arumeru, Arusha, Kondoa, Iramba na Urambo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 ni Mwaka wa Nne wa utekelezaji wa MMEM, ambao una malengo yafuatayo ya kutoa Elimu bora ya Msingi kwa wote, kujenga jumla ya madarasa 7,794 na nyumba za Walimu 6,000 yakiwemo madarasa ya MMEM 6,794 na nyumba za walimu 2,186, kuajiri walimu 7,286 na Walimu tarajali 10,000, kuandikisha Darasa la Kwanza watoto wote 1,041,880 wa miaka 7, kutoa Ruzuku za Maendeleo na Uendeshaji na kutekeleza MEMKWA kwa ukamilifu zaidi katika Wilaya zote.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2004/2005 ili kutekeleza malengo hayo zimetengwa Shilingi 271,222,783,504. Kati ya hizo shilingi 230,394,438,504 zimeombwa kupitia katika Mafungu yanayosimamiwa na mwenzangu mwenye dhamana ya TAMISEMI. Aidha, shilingi 40,829,345,000 zinaombwa kwa ajili ya kazi za MMEM zinazosimamiwa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, Malengo Maalumu ya Elimu ya Sekondari ni yafuatayo:-

(a) Kuongeza nafasi ya utoaji Elimu ya Sekondari kwa rika la Elimu ya Sekondari (miaka 14 - 17) kutoka 7% ya mwaka 2003 hadi kufikia 50% ifikapo 2010.

(b) Kupanua Elimu ya Sekondari katika kutekeleza Mpango wa Elimu ya Sekondari (MMES), kwa kuongeza nafasi ya kidato cha kwanza kutoka 21% mwaka 2003 hadi 45% ifikapo mwaka 2009.

(c) Kuboresha Elimu ya Sekondari kwa kuongeza asilimia ya wanaofaulu mitihani ya Kitaifa ya Kidato cha Nne katika madaraja I, II na III kutoka 39.1% mwaka 2003 hadi zaidi ya 50% ifikapo mwaka 2005.

(d) Kutoa Elimu ya Sekondari kwa usawa kwa jinsia zote, Wilaya zote kwa kuzingatia maelekezo ya kifungu 11(3) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinachosema: "Serikali itafanya jitihada kuhakikisha kwamba, watu wote wanapata fursa sawa za kutosha kuwawezesha kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za shule na vyuo vingine vya mafunzo".

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Idara ya Elimu ya Sekondari imekuwa na mafanikio yafuatayo:-

(a) Ongezeko la shule 208 za sekondari na la wanafunzi 47,746 wa Kidato cha Kwanza na 82,111 wa Kidato cha 1 hadi 4.

(b) Shule za Sekondari za Serikali zimeongezeka kutoka 649 mwaka 2003 hadi 828 mwaka 2004. Hili ni ongezeko la shule 179 (27.6%). Aidha, Shule za Sekondari zisizo za Serikali zimeongezeka kutoka 434 mwaka 2003 hadi 463 mwaka 2004. Hili ni ongezeko la shule 29 (6.7%).

(c) Jumla Shule za Sekondari zimeongezeka kutoka 1,083 mwaka 2003 hadi 1,291 mwaka 2004. Hili ni ongezeko la shule 208 sawa na 19.2%.

(d) Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza wameongezeka kutoka 99,744 mwaka 2003 hadi 147,490 mwaka 2004. Hili ni ongezeko la wanafunzi 47,746 au 47.9%.

(e) Wanafunzi wote wa Kidato cha 1 hadi cha 4 wameongezeka kutoka 319,487 mwaka 2003 hadi 401,598 mwaka 2004 ikiwa ni ongezeko la 25.7%. Ongezeko hili ni kubwa kuliko miaka yote iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kukarabati kwa uhisani wa Serikali ya Japan shule za Serikali 14 ambazo ni Utete, Korogwe, Nyang'wale, Itengule, Iringa Wasichana, Kibiti, Zunzuli, Tabora Wavulana, Bwabuki, Maneromango, Makambako, Kilwa, Manyara na Itandula.

(b) Kuzipa magari Shule tano katika mikoa mitano ambayo ilikuwa haijapewa magari mapya kwa ajili ya huduma za shule hizo na pia kuhudumia shule nyingine zilizomo katika mikoa hiyo. Shule zilizopewa magari ni Loleza, Kantalamba, Mwenge, Wotta na Musoma Kutwa.

(c) Kununua Kompyuta 80 kwa ajili ya Shule za Sekondari.

Idadi ya Shule za Sekondari za Serikali zinazotoa elimu ya Kidato cha 5 na Kidato cha 6 imeongezeka kutoka 81 mwaka 2003 hadi 84 mwaka 2004. Shule zilizoongezwa ni Kahororo, Mara na Longido. Shule zisizo za Serikali zinazotoa elimu

ya Kidato cha 5 na Kidato cha 6 ni 127. Kwa hiyo, jumla ya sekondari zenye Kidato cha 5 ni 211.

Mikondo mipya ya Kidato cha 5 imeongezwa katika Shule za Sekondari za Kilakala, Tabora Wavulana, Msalato, Tanga Ufundi, Musoma Ufundi, Minaki, Lindi, Songea Wasichana, Mawenzi, Ifunda, Bwiru Wasichana na Mwakaleli.

Wanafunzi waliochaguliwa kuingia Kidato cha 5 waliongezeka kutoka 10,158 mwaka 2003 hadi 12,253 mwaka 2004. Hili ni ongezeko la wanafunzi 2,075 sawa na 9.5%. Wanafunzi wengine 1,130 watachaguliwa kujaza nafasi katika shule za Serikali zitakazopanuliwa mwezi Julai/Agosti, 2004 na kufanya jumla kuwa wanafunzi 13,383 wa Kidato cha 5. Jumla ya Wanafunzi wa Kidato cha 5 na 6 imeongezeka kutoka 25,954 mwaka 2003 hadi 31,001 mwaka 2004. Jumla ya wanafunzi wa Sekondari Kidato cha 1 hadi 6 imeongezeka kutoka 261,896 mwaka 2000 hadi kufikia 432,599 mwaka 2004.

Katika kutoa Elimu ya Sekondari kwa usawa, Serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha kuwa idadi sawa ya wasichana na wavulana wanachaguliwa kuingia Kidato cha Kwanza kila mwaka.

(b) Kulipia gharama za elimu kwa wanafunzi kutoka familia zisizo na uwezo kiuchumi. Jumla ya wanafunzi 12,000 wanagharamiwa mpaka sasa.

(c) Kulipia Elimu ya Sekondari kwa Wasichana 2,361 wa Kidato cha 3 hadi 6 ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwalipia.

(d) Kuhamasisha ufunguzi wa shule za sekondari za kutwa hususan kwenye maeneo ambayo hayakuwa na shule za kutosha. Shule mpya 179 zimefunguliwa. Napenda kuipongeza Mikoa,Wilaya/Halmashauri zilizofungua shule nyingi mpya mwaka huu. Wilaya/ Halmashauri hizo ni Moshi Vijijini 9, Rungwe 8, Mbozi 7, Geita 7, Magu 5, Masasi 5 na Mbinga 5. Mikoa iliyofungua shule nyingi zaidi ni Mbeya 27, Kilimanjaro 18, Mtwara 16, Iringa 15, Mwanza 14, Kigoma 9, Ruvuma 8, Pwani 6 na Rukwa 5. Nawapongeza hao wote kwa juhudi zao.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha Elimu ya Sekondari yafuatayo yalifanyika:-

(a) Shule za Sekondari za Serikali 51 zilipewa jumla ya shilingi 330,432,530 kwa ajili ya ukarabati wa majengo. Utekelezaji ulivuka lengo kwa 70%.

(b) Shule za Sekondari za Serikali 644 zilipewa kiasi cha shilingi 490,152,400 kwa ajili ya ununuzi wa vitabu vya Sayansi na Hisabati.

(c) Walimu 461 walipatiwa mafunzo kazini, 327 mafunzo ya mbinu bora za ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati, 87 Programu maalumu ya Shahada ya Hisabati katika Chuo Kikuu cha Tumaini, 39 mafunzo ya Stashahada ya Uzamili katika

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 5 mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na 3 mafunzo ya kompyuta katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha.

(d) Walimu 102 wa Shahada na 1,000 wa Stashahada waliajiriwa. Aidha, walimu 615 wasiokuwa na ualimu kwa kusomea wameajiriwa kufundisha kwa liseni baada ya mafunzo mafupi ya pedagogia.

(e) Ujenzi wa maabara za masomo ya Sayansi uliendelea katika shule za Mbekenyera, Makiba, Mwaya, Mitole, Matekwe, Zingibari, Kongwa, Mangaka, Meatu, Mahiwa na Runzewe. Ukamilikaji wa ujenzi uko kati ya 60% na 88% katika shule mbalimbali.

(f) Ufaulu katika mitihani ya Kidato cha Nne Daraja la I hadi III umeongezeka kutoka 36.2% mwaka 2002 hadi 39.1% mwaka 2003.

Katika kuimarisha na kuboresha uongozi na usimamizi wa kutoa Elimu, Wizara ilipata mafanikio yafuatayo:-

(a) Kuwapatia mafunzo ya Uongozi ya mwezi mmoja Wakuu wa Shule 132 na Makamu Wakuu wa shule 126 wa Shule za Serikali.

(b) Jumla ya Wakuu wa shule 360 walishiriki katika Mkutano Mkuu wa Elimu uliofanyika Arusha tarehe 8 - 12 Desemba, 2003 na kuweka mikakati ya kuboresha huduma za Elimu katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, miradi mbalimbali ilitekelezwa na Wizara yangu kwa lengo la kuboresha Elimu ya Sekondari kwa mwaka 2003/2004 kama ifuatavyo:-

Mradi wa Uboreshaji wa Elimu ya Sayansi *(Science Education for Secondary Schools - SESS)*: Mradi huu una sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inalenga kuboresha ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati *(Science Education for Secondary Schools - SESS)* na sehemu ya pili ni Elimu dhidi ya UKIMWI *(Prevention and Awareness in Schools of HIV and AIDS - PASHA),* ambao ulianza rasmi Julai, 2003. Mradi wa *SESS* ulitoa mafunzo ya mbinu bora za kufundisha masomo ya Sayansi na Hisabati kwa walimu. Kazi mahsusi zilizofanywa na mradi huo katika kipindi hiki ni:-

(a) Kutoa mafunzo kwa wawezeshaji *(trainers)* 60 kutoka Mikoa ya Tabora, Kigoma na Shinyanga.

(b) Kuwalipatia mafunzo mahali pa kazi *(Cluster Workshop)* walimu 243 katika mikoa ya Iringa, Dodoma, Pwani, na Mwanza.

(c) Kuwalipatia mafunzo ya kufundisha mada za *HIV/AIDS* walimu 24 kutoka Mikoa ya Dodoma, Pwani na Iringa.

(d) Kuwalishirikisha katika kambi ya Sayansi wanafunzi wasichana 187 kutoka Mikoa ya Tanga, Pwani na Morogoro.

Mradi wa Pili wa Elimu *(Education II Project),* uliendelea na ujenzi wa maabara za masomo ya Sayansi katika Shule za Sekondari 36 za Serikali zilizojengwa na wananchi. Hadi kufikia Machi, 2004, maendeleo ya ujenzi wa maabara katika shule 36 za awamu zote tatu ulikuwa kama ifuatavyo:-

| Awamu | Asilimia Wastani wa Matarajio | Asilimia Kiwango Kilichojengwa |
|---|---|---|
| 1 | 100 | 88.05 |
| 2 | 100 | 63.37 |
| 3 | 87.39 | 42.96 |

(b) Kwa wastani ujenzi wa maabara zote umekamilika kwa 71.6%.

(c) Shule 18 zimepatiwa samani za maabara. Aidha, samani kwa ajili ya shule nane zimenunuliwa na zinasubiri ukamilishwaji wa maabara husika.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2003/2004, niliahidi kuwa Serikali ingekamilisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES). Ninafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, utayarishaji wa Mpango huo umekamilika na utagharimu jumla ya Shilingi bilioni 1,433.084 kwa miaka mitano ya 2004 - 2009. Katika bajeti ya mwaka 2004/2005 zimetengwa jumla ya Shilingi 91,481,468,500 zikiwemo Shilingi 59,413,581,900 za Maendeleo na Shilingi 32,067,586,900 za matumizi ya kawaida. Hii ni mara ya kwanza kuwa na bajeti kubwa kiasi hiki kwa Elimu ya Sekondari. Namshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa jitihada zake anazofanya kuhusu Elimu.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Mpango kwa mwaka 2004/2005 ni kuongeza vijana wa Tanzania wanaosoma na kuhitimu Elimu ya Sekondari wakiwa na matokeo mazuri ya kujifunza kutoka 345,000 mwaka 2003 hadi 2,000,000 mwaka 2010. Mpango huu unazo programu tano zifuatazo:-

- Kuongeza wanaojiunga na sekondari *(Improvement of Access)* kufikia 50 % ya rika lengwa (miaka 14 - 17) na 50% ua wahitimu wa Darasa la VII, pia 50% ya wahitimu wa Kidato cha Nne kujiunga Kidato cha Tano kila mwaka. Lengo hili litafikiwa kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Upanuaji wa shule zilizopo na ujenzi wa shule mpya hususan kule ambako haziko. Inatarajiwa kujenga shule mpya 1500 katika kipindi cha mpango.

(b) Kuongeza nafasi za Kidato cha 5 na 6 zaidi ya mara tano za mwaka 2003.

(c) Utumiaji mzuri wa walimu waliopo na upanuaji wa mafunzo na ajira ya walimu. Chuo cha Ualimu Dar es Salaam na Shule ya Sekondari Mkwawa, vitabadilishwa kuwa

Vyuo Vikuu Vishiriki vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili pamoja na Stashahada za Elimu, vitoe pia Shahada ya Ualimu katika miaka mitatu. Aidha, mafunzo ya Stashahada na Shahada yataoanishwa ili mafunzo ya Stashadada yatosheleze sehemu ya Shahada ya Ualimu ya mwaka wa kwanza. Kwa hiyo, mwenye Stashahada ya Ualimu ataweza kujiunga na Chuo Kikuu kukamilisha miaka miwili iliyobakia ili apate Shahada yake ya Ualimu.

(d) Kuisaidia Sekta Binafsi inayotoa Elimu ili iboreshe shule zake kwa sababu inasaidia Serikali kutoa elimu.

(e) Kupanua elimu ya sekondari kwa njia ya posta.

(f) Kupunguza viwango vya kuacha shule, kurudia na kufeli katika ngazi zote.

(g) Kupunguza mzigo wa elimu ya sekondari kwa familia kwa kupunguza ada na michango.

Kuongeza usawa *(Improvement of Equity)* kwa jinsia zote, wilaya zote, wenye ulemavu na makundi tofauti ya mapato kwa:-

(a) Kuelekeza uwekezaji kule kwenye uhaba wa shule pamoja na kukamilisha shule zilizopo.

(b) Kuwalipia ada watoto wa familia maskini.

(c) Kuongeza kujiunga, kubakia shuleni na kufaulu kwa wasichana.

(d) Kuboresha majengo na vifaa katika shule zenye wanafunzi wenye ulemavu.

(e) Kuboresha utoaji wa elimu kwa jamii zilizo nyuma kielimu na zisizofikika kwa urahisi.

(f) Kupunguza ada katika Sekondari za Serikali za kutwa.

- Kuongeza ubora *(Quality Improvement)* wa elimu ili wanaofaulu Kidato cha Nne katika Madaraja I - III waongezeke kutoka 36% mwaka 2003 hadi 70% mwaka 2009, kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuongeza na kuimarisha Mafunzo ya Ualimu Kazini.

(b) Kuboresha sifa za kujiunga na mafunzo ya ualimu wa Stashahada na Shahada.

(c) Kuboresha mitaala kwa kuzingatia masomo sahihi ya Elimu ya Sekondari na kuingiza ndani yake Elimu ya Kujitegemea na kuacha kufundisha masomo ya michepuo hususan ya Ufundi Kilimo na Biashara.

(d) Kuboresha maktaba za shule.

(e) Kutoa Ruzuku ya Uendeshaji wa Shule kwa kwa ajili ya mahitaji ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

(e) Kuboresha muundo na ubora wa mitihani.

(g) Kupanua mafunzo ya Elimu ya Ualimu ya Stashahada na Shahada.

(h) Kuingiza katika mitaala masuala mtambuka kama vile Elimu ya Jinsia na Mazingira na Elimu Dhidi ya UKIMWI *(HIV and AIDS).*

- Kufanya mageuzi ya kutoa madaraka *(Devolution of Powers)* kwa Mikoa, Wilaya na Shule ili kuboresha usimamiaji na uendeshaji wa shule za sekondari. Madaraka ya uamuzi, utendaji, usimamiaji wa fedha yatahamishwa kutoka Wizara kwenda ngazi za Mkoa, Wilaya na Bodi za Shule.

- Kuboresha Mfumo wa Usimamiaji wa Elimu kwa lengo la kuhakikisha kuwa, Wizara inatekeleza majukumu yake ya msingi *(Core Functions)* wa kubuni sera, kufuatilia na kutathmini, kutunga kanuni, kuainisha na kuhakiki utumiaji wa rasilimali. Lengo hili litafikiwa kwa kuimarisha Ukaguzi wa Shule na kuimarisha Uongozi wa Shule, kuboresha upatikanaji na utumiaji wa mfumo wa taarifa na mawasiliano ya Kielimu *(Education Management Information System - EMIS),* kujenga uwezo *(Capacity Building)* katika ngazi zote, kuimarisha mawasiliano na ufahamikaji wa mpango na kuimarisha ufuatiliaji na tathmini *(Monitoring and Evaluation).*

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kibajeti wa Utekelezaji wa MMES 2004 - 2009, utakua kwa kuongeza uwekezaji katika elimu kwa njia ya bajeti ya Serikali inayokwenda moja kwa moja kwa walengwa. Hatua na njia muhimu zitakazotumika kuanzia Bajeti ya mwaka 2004/2005 zitakuwa ni kutoa Ruzuku ya Maendeleo kwa ajili ya shule za Serikali zinazojengwa na wananchi kama ifuatavyo:-

(a) Shilingi 7.0 milioni kwa ajili ya ujenzi wa darasa ili kununulia vifaa vya ujenzi kutoka viwandani (mabati, saruji, nondo, misumari, rangi na vioo), pamoja na madawati, kabati, mbao za kuandikia, meza na viti.

(b) Shilingi 9.0 milioni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mwalimu ili kununulia vifaa vya ujenzi vinavyotengenezwa viwandani (mabati, saruji, nondo, misumari, rangi na vioo).

(c) Ujenzi wa maabara na maktaba kwa zabuni ya Serikali ngazi ya Wilaya

(d) Kusaidia ujenzi wa hosteli pale inapohitajika kwa kulipia vifaa vya ujenzi vinavyotengenezwa viwandani (mabati, saruji, nondo, misumari, rangi na vioo vya madirisha).

- Kutoa Ruzuku ya Uendeshaji wa Shule *(Capitation Grant)* kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia ya Shilingi 30,000 kwa kila mwanafunzi kwa Sekondari za Serikali na Shilingi 15,000 kwa mwanafunzi kwa Sekondari zisizo za Serikali ambazo haziendeshwi kibiashara na siyo seminari.

- Kutoa Ruzuku ya Maendeleo kwa mwenye shule asiye Serikali aliyeidhinishwa na Afisa Elimu Kiongozi kwa ajili ya ujenzi wa shule za wanafunzi wenye ulemavu kwa viwango sawa na ile inayotolewa kwa ajili ya Sekondari za Serikali zinazojengwa na wananchi.

- Kupunguza ada ya Sekondari za Kutwa za Serikali kutoka Shilingi 40,000 kuwa Shilingi 20,000 kuanzia Januari, 2005. Hatua hii imechukuliwa ili watoto wengi wa familia zenye mapato ya chini waweze kujiunga na sekondari kwa kulipia angalau shilingi 10,000 kwa muhula. Ada yote ya shilingi 20,000 itabakia shuleni na Serikali itatoa kwa kila shule kutokana na bajeti hii shilingi 20,000 nyingine kwa mwanafunzi kufidia punguzo la ada. Ikumbukwe kuwa Serikali itatoa pia ile Ruzuku ya Uendeshaji ya shilingi 30,000 kwa mwanafunzi. Kwa hiyo, kwa Sekondari za kutwa jumla zitakuwepo shilingi 70,000 kwa mwanafunzi kwa ajili ya uendeshaji wa shule ili kukidhi haja ya mahitaji ya shule.

- Kuongeza maradufu Ruzuku ya Elimu ya Sekondari kwa watoto wa familia maskini ili watakaonufaika waongezeke kutoka 6,000 kwa mwaka kuwa 12,000 kwa mwaka kuanzia mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu umeongeza uwezekano wa watoto wa familia maskini kujiunga na Sekondari za Bweni kwa Serikali kufanya yafuatayo: Kubakiza shuleni ada yote ya shilingi 70,000, kutoa pia shilingi 30,000 za Ruzuku ya Uendeshaji na kufanya jumla iwe shilingi 100,000 kwa mwanafunzi kwa mwaka na pia zimepangwa shilingi 862.47 za chakula kwa mwanafunzi kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua hizo za kibajeti, Sekondari zote za Serikali zitapewa fedha ya kutosha ya uendeshaji wa shule. Kwa hiyo, Bodi za shule haziruhusiwi kutoza michango yoyote kwa ajili ya uendeshaji wa sekondari zote za Serikali. Serikali inataka watoto wote wanaochaguliwa kwenda sekondari, wawe wanajiunga na kuendelea bila kuacha shule mpaka wahitimu ili tuweze kuyafikia malengo ya Mpango huu ya kuwa na wanafunzi wa Sekondari 2,000,000 ifikapo mwaka 2010 na wahitimu wa Sekondari wasiopungua 500,000 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mwaka wa kwanza wa Mpango huu utakuwa kama ifuatavyo:-

- Kutoa Ruzuku ya Maendeleo ya Shilingi 7.0 milioni kwa darasa kukamilisha ujenzi wa madarasa 1,456 katika shule zilizopo za mikondo miwili na mitatu ili ziwe za mikondo minne. Jumla ya Shilingi 10,192,000,000 zimetengwa kwa ajili hiyo.

- Kutoa Ruzuku ya Maendeleo ya Shilingi 7.0 milioni kwa ujenzi wa darasa, kukamilisha ujenzi wa madarasa 458 katika sekondari mpya katika maeneo yasiyo na sekondari za kutosha *(Underserved Areas)*. Jumla zimetengwa Shilingi 3,206,000,000.

- Kutoa Ruzuku ya Maendeleo ya Shilingi 9.0 milioni kwa ujenzi wa kila nyumba ili kukamilishia ujenzi wa Nyumba za Walimu 957. Jumla ya Shilingi 8,613,000,000 zimetengwa kwa ajili hiyo.

- Kukarabati shule 40 za Serikali zilizopo kwa Shilingi 2,734,000,000.

- Kukarabati shule nane za sekondari zenye wanafunzi wenye ulemavu na kuchangia ujenzi wa shule mpya mbili za wenye ulemavu Shilingi 1,231,400,000.

- Kukamilisha ujenzi wa maabara 90 katika shule 36 kwa Shilingi 1,109,273,900.

- Kujenga majengo yanayohitajika katika sekondari 14 za Serikali ili kuzibadilisha mwaka unaofuata zitoe elimu ya Kidato cha 5 na 6 tu na kupanua nyingine 64 za *A - level* kwa Shilingi 3,132,000,000.

- Kugharamia Elimu ya Sekondari kwa watoto 12,000 wa familia maskini kwa Shilingi 2,160,000,000 kwa Kidato cha Kwanza mwaka 2005.

- Kutoa Elimu ya Sekondari kwa mfumo usio rasmi *(Open and Distance Learning)* kwa Shilingi 1,878,000,000.

- Kutoa Ruzuku ya Shilingi 20,000 kwa kila mwanafunzi wa Sekondari ya Serikali ya Kutwa kufidia punguzo la karo. Jumla Shilingi 4,939,000,000 zimetengwa.

- Kutoa Ruzuku ya Uendeshaji ya Shilingi 20,000 kwa mwanafunzi kwa sekondari za Serikali na Sh. 10,000 kwa Sekondari zisizo za Serikali ambazo sio za kibiashara na sio Seminari. Jumla Shilingi 7,074,219,000 zimetengwa.

- Kupunguza masomo ya Sekondari kutoka 13 kuwa manane yakiwemo *Mathematics,* Lugha (Kiswahili na *English*), masomo ya Sayansi *(Biology, Physics* na *Chemistry)* na Sayansi ya Jamii *(History, Geography* na *Civics)* na kuacha kufundisha michepuo *(Technical Studies, Agriculture* na *Commerce)* ambayo ina vyuo vyake chini ya Wizara husika.

- Kuongeza nafasi za Mafunzo ya Ualimu wa sekondari, kwa kukibadilisha Chuo cha Ualimu Dar es Salaam na Shule ya Sekondari Mkwawa kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Elimu ya Ualimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Kutoa chakula sekondari za bweni: Shilingi. 9,417,173,200 sawa na Sh 862.47 kwa mwanafunzi kwa siku.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mazungumzo na Wabia na Wahisani ili kupata fedha za kutosha kutekeleza malengo yote ya Mpango. Naishukuru sana Bodi ya Benki ya Dunia ambayo tarehe 8 Juni, 2004 ilipitisha mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Kimarekani 124 milioni na Ruzuku ya Dola za Kimarekani 26 milioni. Fedha hii imewezesha MMES uanze katika Bajeti ya mwaka huu kwa Shilingi 53.8 bilioni

Mheshimiwa Spika, Malengo Maalum ya Elimu ya Ualimu ni yafuatayo:-

(a) Kuandaa walimu wa ngazi ya cheti Daraja A na Stashahada ili kukidhi mahitaji kwa shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

(b) Kuboresha mazingira ya kutolea mafunzo katika Vyuo vya Ualimu kwa kutoa vifaa bora na vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia.

(c) Kuimarisha Vituo vya Walimu *(Teachers' Resource Centres - TRCs)* katika ngazi ya Wilaya, Kanda na Taifa.

(d) Kuboresha taaluma na utaalamu wa ufundishaji wa masomo ya shule za msingi hususan kwa kuwapatia mafunzo maalumu kazini ya Daraja A *(In-Service Grade A)* walimu wote wa Daraja B/C na kuwatahini.

(e) Kupanua mafunzo ya Ualimu sambamba na upanuaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Idara ya Elimu ya Ualimu ilitoa mafunzo kwa:-

(a) Walimu tarajali wa Daraja A ambapo walimu 6,578 walihitimu kwa kufaulu baada ya mazoezi kwa vitendo.

(b) Mwaka 2003, wanachuo 15,283 waliandikishwa kufanya mitihani na kati yao 14,836 walifaulu na kuendelea mwaka wa pili wa mafunzo kwa vitendo shuleni.

(c) Walimu wa Stashahada 2,390 wamehitimu. Wizara ilivifanyia ukarabati Vyuo vya Elimu ya Ualimu 10 kwa gharama ya Shilingi 130,300,000. Vyuo vilivyofanyiwa ukarabati ni: Marangu, Dar es Salaam, Kleruu, Ilonga, Nachingwea, Tandala, Sumbawanga, Morogoro, Tarime na Mpuguso.

(d) Mwaka 2004, wanachuo 10,037 wamejiunga na Mafunzo ya Ualimu Daraja A tarajali katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na 751 katika vyuo visivyo vya Serikali.

- Wawezeshaji 763 walipatiwa mafunzo kwa ajili ya kuwaendeleza walimu wa C/B kufikia Daraja la A *(Inservice Grade A).* Walimu 25,000 wa Daraja C/B, wameandikishwa kwa ajili ya mafunzo hayo. Walimu 16 ambao hawajasomea taaluma ya Ualimu wanalipiwa gharama ya mafunzo ya Stashahada ya Uzamili katika Elimu *(Post*

*Graduate Diploma in Education).* Aidha, wakufunzi 250 wanasoma Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kugharamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, wanachuo tarajali 10,000 wa Daraja A na 3,624 wa Stashahada watajiunga na mafunzo ya Ualimu. Walimu 25,000 wa Daraja C/B watajiunga na mafunzo ya kujiendeleza. Walimu 49,000 watajiunga na mafunzo kazini ya ufundishaji kwa kutumia njia na mbinu shirikishi kupitia Vituo vya Ualimu. Aidha, walimu wa shule za msingi wa Daraja A watapewa mafunzo kazini ya aina mbalimbali kwa kutumia njia na mbinu shirikishi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/04, Idara ya Ukaguzi wa Shule ilikagua jumla ya asasi za elimu 15,733 sawa na 82% ya lengo la mwaka. Katika kuboresha kazi ya ukaguzi wa shule, Wizara imenunua magari mawili, kwa ajili ya ukaguzi wa shule na imeendesha mafunzo ya awali ya ukaguzi wa shule kwa wakaguzi wa shule wapya 127. Shughuli nyingine zilizofanyika ni pamoja na kutoa Jarida la FAHAMU ELIMU Na. 6 kuhusu somo la Kiswahili kwa lengo la kubaini maendeleo ya somo hilo na kufanya ukaguzi maalumu wa shule za Sekondari 179 kwa ajili ya upanuzi wa Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara imepanga kufanya ukaguzi wa asasi mbalimbali za Elimu 19,332. Aidha, Idara itanunua magari 13 na kutoa mafunzo ya awali ya Ukaguzi wa Shule kwa wakaguzi wa shule wapya 127. Shughuli nyingine zitakazofanyika ni pamoja na utafiti kuhusu maendeleo ya ufundishaji wa somo la Stadi za Kazi katika Shule za Msingi na Vyuo vya Ualimu Daraja la A na kuandika Jarida la FAHAMU ELIMU Na. 7 kuhusu somo la *Civics.*

Mheshimiwa Spika, Malengo Maalumu ya Maendeleo ya Utamaduni ni kama ifuatavyo:-

(a) Kupanua kiwango cha Ushiriki wa wananchi katika shughuli za Utamaduni.

(b) Kuboresha Usimamizi na Uendeshaji wa shughuli za Utamaduni.

(c) Kuimarisha Elimu na Mafunzo ya Fani za Utamaduni.

(d) Kuimarisha na kukuza Tasnia na Miundo Mbinu ya Utamaduni.

(e) Kulinda na kuimarisha Maadili na Utambulisho wa Taifa.

(f) Kuimarisha Ushirikiano wa Kimataifa katika Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Idara ya Maendeleo ya Utamaduni kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Iliandaa mashindano ya kupata Vazi la Taifa kwa wanaume na wanawake.

(b) Ilitoa misaada kwa miradi mbalimbali ya Utamaduni kupitia Mfuko wa Utamaduni.

(c) Iliendesha mradi wa Sanaa kwa wanafunzi wa shule za Msingi katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Pwani. Aidha, Wizara iliendesha Mradi wa TUSEME katika shule 16 za Sekondari za Wasichana na za mchanganyiko saba.

(d) Iliendesha tamasha la Sanaa la Ishirini na mbili la Bagamoyo lililoshirikisha wasanii wa Vikundi 64 vya ndani na nje ya nchi.

(e) Ilitoa Mafunzo ya Stashahada kwa wanafunzi 87 na mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 60 katika Chuo cha Sanaa, Bagamoyo.

(f) Ilitoa mafunzo kwa Maafisa Utamaduni wa Wilaya 96 juu ya jinsi ya kubadili mila na desturi zinazoongeza kasi ya maambukizi ya UKIMWI.

(g) Iliendesha Mkutano Mkuu wa Sekta ya Utamaduni.

Katika mwaka 2004/2005, Idara ya Utamaduni itatekeleza mambo kumi kuhusu utafiti wa mila na desturi, maonesho ya utamaduni na mafunzo ya utamaduni yafuatayo:-

(a) Itafuatilia matokeo ya mchakato wa mashindano ya Vazi la Taifa kwa wanaume na wanawake.

(b) Itaendesha mafunzo ya ukusanyaji, uhifadhi na usambazaji wa takwimu za Utamaduni kwa Maafisa Utamaduni 113 wa Halmashauri.

(c) Itaendesha mkutano wa Sekta ya Utamaduni utakaowashirikisha Wajumbe 300 kutoka Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika, Vyama vya Hiari na Asasi zisizo za Serikali.

(d) Itaendesha Programu za Sanaa kwa wanafunzi wa shule za msingi 70 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Jiji la Mwanza pamoja na programu ya TUSEME kwa shule za sekondari 23 za mikoa 19 ya Tanzania Bara.

(e) Itaendesha mafunzo ya Stashahada kwa wanafunzi 90 na mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 60.

(f) Itaendesha Tamasha la ishirini na tatu la Sanaa Bagamoyo.

(g) Itaendelea kusaidia miradi ya utamaduni kupitia Mfuko wa Utamaduni.

(h) Itaendesha tamasha la Utamaduni la Taifa litakaloshirikisha Mikoa yote.

(i) Itaendesha warsha ya mapambano dhidi ya UKIMWI.

(j) Itatengeneza filamu moja juu ya UKIMWI itakayooneshwa nchini kote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Idara ya Utawala na Utumishi ilishughulikia ajira ya walimu wapya 2,904 wa shule za Sekondari, Vyuo vya Elimu ya Ualimu na watumishi wasio walimu 28.

Aidha, jumla ya watumishi 275 walipata mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara inatarajia kuomba kibali cha ajira mpya ya watumishi 2,780 wa kada mbalimbali. Katika jitihada za kujenga uwezo wa watumishi, Wizara itapeleka Watumishi 100 kwenye mafunzo ya muda mrefu na 50 ya muda mfupi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Idara itahakikisha Programu ya kuboresha Utumishi wa Umma inatekelezwa kwa kushirikisha Sekta binafsi katika kutoa huduma za usafi, ulinzi na mapokezi katika jengo la Wizara Makao Makuu. Aidha, kuanzia Julai, 2004 Wizara itaanza utekelezaji wa mpango wa mwaka wa tathmini ya utendaji kazi wa watumishi kwa utaratibu mpya unaolenga kuweka malengo na matokeo katika utendaji kazi *(Performance Management System),* kwa watumishi wa Makao Makuu ya Wizara na kwenye Shule na Vyuo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu *(Agency for the Development of Education Management - ADEM),* walitoa mafunzo ya menejimenti na utawala kwa viongozi watendaji wa elimu wa ngazi mbalimbali 518. Katika mwaka 2004/2005, *ADEM* itatoa mafunzo mbalimbali kwa viongozi watendaji wa elimu 6,108 wakiwemo Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa wanachuo 90.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Idara ya Sera na Mipango ilishirikiana na Idara nyingine:-

(a) Kupanga, kuratibu na kutekeleza mipango ya elimu kulingana na Sera ya Elimu na Mafunzo na Utamaduni.

(b) Imesimamia ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya kazi.

(c) Imesimamia na kuratibu ukarabati wa shule za Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Ualimu.

(d) Imetekeleza wajibu wake wa kuwa kiungo kati ya Wizara yangu, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Wizara ya Fedha, Wahisani na Wadau mbalimbali.

(e) Shughuli nyingine zilizofanyika ni pamoja na kutayarisha programu na mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ya sab-sekta ya elimu ya awali, msingi,

sekondari, ualimu, elimu ya watu wazima na utamaduni, pamoja na kuandaa na kuratibu rasimu za maandiko mbalimbali zikiwemo hotuba za bajeti.

Katika mwaka 2004/2005, Idara ya Sera na Mipango itashughulikia masuala mbalimbali pamoja na:-

(a) Kufanya utafiti na tathmini kwa matumizi ya baadaye, kufuatilia mwenendo na utoaji wa huduma za elimu na utamaduni na kutoa ushauri wa kitaalamu.

(b) Itaendelea kuandaa na kuratibu rasimu na maandiko mbalimbali ya kitaalamu yanayohusu miradi na mipango, sera, takwimu, hotuba na makala mbalimbali.

(c) Itaendelea kuandaa mapitio ya matumizi ya fedha za umma *(Public Expenditure Review),* kuandaa *Medium Term Expenditure Framework (MTEF)* za Wizara na Sekta ya Elimu kwa ujumla kwa kushirikiana na sab-sekta nyingine za elimu.

(d) Itaendelea kusimamia na kuratibu ukarabati wa shule za Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Ualimu.

(e) Itatoa mafunzo kwa jumuiya za shule na vyuo kuhusu matengenezo madogo madogo na dhana ya utunzaji wa majengo na mazingira yake.

(f) Kuratibu misaada ya wahisani pamoja na kusimamia uimarishaji wa *EMIS.*

(g) Itasimamia udhibiti wa ubora wa vitabu na zana za kufundishia zinazotumika shuleni na vyuoni.

Mheshimiwa Spika, Afisa Elimu Kiongozi pamoja na kuratibu utekelezaji wa Sera za Elimu na Mafunzo na Utamaduni na kutoa miongozo ya kuboresha Elimu na Utamaduni, huongoza vitengo maalumu vilivyo katika ofisi yake. Aidha, Afisa Elimu Kiongozi husimamia shughuli za uhusiano wa Kimataifa ikiwa ni pamoja na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kilihamasisha Viongozi 759 wa Mikoa na Halmashauri kuhusu utekelezaji wa mkakati wa Kitaifa wa Elimu ya Watu Wazima na MEMKWA. Aidha, Kitengo kilitoa mafunzo ya wiki tatu kwa wawezeshaji wa MEMKWA 496 wa ngazi ya Halmashauri, watendaji wa ngazi ya Mikoa, Watendaji wa Kanda na washiriki kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha elimu itolewayo katika madarasa ya EWW na MEMKWA, kitengo kiliendesha mafunzo ya wawezeshaji 73 wa Elimu ya Watu Wazima na 96 wa MEMKWA katika Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi wanaosoma kupitia MEMKWA na wanakisomo kupitia MUKEJA ni 340,060.

Katika mwaka 2004/2005, Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima kitatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mafunzo kwa wawezeshaji wa MEMKWA 1,475 na MUKEJA 2,706.

(b) Kununua na kusambaza moduli za MEMKWA 81,132 na nakala 570 za Miongozo ya Elimu ya Watu Wazima katika Halmashauri.

(c) Kufuatilia maendeleo ya madarasa ya MEMKWA.

(d) Kuratibu masomo ya Elimu ya Sekondari kwa njia ya Posta utakaotekelezwa chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) 2004 - 2009.

(e) Kutoa miongozo ya uendeshaji wa MEMKWA na MUKEJA.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara ilitoa mafunzo ya muda mfupi kwa walimu 164 wasio wataalamu wa Elimu Maalumu kuhusu Elimu Ujumuisho. Pia, ilichapisha na kusambaza jumla ya nakala 1,500 za vitabu vya masomo mbalimbali ya shule za msingi kwa wanafunzi wasioona.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara itanunua mtambo mpya kwa ajili ya kuchapa vitabu na makala mbalimbali za *Braille* na itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa walimu wataalamu 36 wa wanafunzi Viziwi kuhusu Lugha ya Alama, matengenezo ya Shime Sikio *(Hearing Aids)* na utunzaji wake. Pia, itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa walimu 128 wasio wataalamu wa Elimu Maalumu kuhusu Elimu Ujumuisho. Vilevile, Wizara itatengeneza na kusambaza michoro mguso 100, ramani mguso 500 na Shime Sikio 500.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Kitengo cha Usajili wa Shule, kilisajili shule zisizo za Serikali 90. Aidha, shule103 zimethibitishwa Mwenye Shule na Meneja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/04 shule 179 zilizojengwa kwa nguvu za wananchi zilipewa kibali cha kuanzishwa. Aidha, katika mwaka 2003/04 waombaji 326 walipewa leseni za kufundisha baada ya kuwa na sifa zinazostahili.

Mwaka 2004/2005 Kitengo cha Usajili wa Shule kimepanga kufanya yafuatayo:-

(a) Kushughulikia maombi 130 ya kuanzisha na kuthibitishwa Meneja, Mwenye Shule zisizo za serikali.

(b) Kushughulikia maombi 229 ya vibali vya kuanzisha shule za sekondari.

(c) Kushughulikia maombi 400 ya leseni za kufundisha.

(d) Kuchapisha nakala 200,000 za vyeti vya usajili wa walimu.

(e) Kukusanya takwimu za walimu walio kazini na kuendelea kuwasajili.

(f) Kuratibu masuala ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Jumuiya ya Kusini mwa Afrika.

(g) Kuratibu Utafiti Na. 3 wa Ubora wa Elimu Katika Nchi 15 za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu kwa kushirikiana na Redio Tanzania Dar es Salaam, iliandaa na kutangaza vipindi 104 kama ifuatavyo: Ufundishaji Vipindi 52 na Boresha Elimu Vipindi 52. Aidha, vipindi 96 vya masomo ya Kiingereza na Maarifa ya Jamii darasa la VI na VII vilitangazwa. Hivyo, jumla ya vipindi vyote vilivyotangazwa vilikuwa 200.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, vipindi 248 vitatangazwa kama ifuatavyo:-

(a) Itaandaa na kutangaza vipindi 52 vya 'Boresha Elimu' ili kuendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu MMEM 2002 - 2006 na MMES 2004 - 2009.

(b) Itaandaa na kutangaza vipindi 52 vya Ufundishaji mitaala mipya kwa walimu.

(c) Itatangaza vipindi 96 vya Kiingereza na Maarifa ya Jamii darasa la VI na VII.

(d) Itaandaa na kutangaza vipindi 48 vya Kiingereza na Maarifa ya Jamii la *DV.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara iliendesha semina za wadau wanaohusika na utekelezaji wa Mpango wa Elimu Dhidi ya UKIMWI kwa waelimishaji wenza katika Asasi na Idara mbalimbali. Aidha, mafunzo ya elimu hiyo yalitolewa kwa walimu 48 wasioona, walimu wa shule za msingi 800, walimu wa shule za sekondari 1,620, pamoja na wafanyakazi wa Baraza la Mitihani la Tanzania, Taasisi ya Elimu Tanzania, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu *(ADEM)*. Vilevile, wizara imechapisha vitabu 13,314 vya Elimu Dhidi ya UKIMWI kwa wanafunzi wa darasa la V, VI, VII na kiongozi cha mwalimu nakala 19,600.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara itatekeleza mambo yafuatayo kuhusu Elimu Dhidi ya UKIMWI:-

(a) Kukamilisha mada za Elimu ya Kujikinga na UKIMWI kwa ajili ya kuingizwa kwenye mihtasari ya masomo chukuzi katika shule za Sekondari na vyuo vya Elimu ya Ualimu.

(b) Itaendelea kuchapisha na kusambaza maandiko ya mafunzo ya Elimu ya Kujikinga na UKIMWI shuleni na vyuo vya Elimu ya Ualimu.

(c) Itaendesha mafunzo kwa walimu wa shule za sekondari.

(d) Itafanya ufuatiliaji na tathmini ya programu ya UKIMWI shuleni.

(e) Itaendelea kutekeleza programu ya UKIMWI shuleni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ilitekeleza mambo sita yafuatayo:-

(a) Ilikamilisha Mfumo wa Taifa wa Ukuzaji Mitaala. *(National Curriculum Development Framework).*

(b) Ilitoa mafunzo ya MEMKWA kwa wawezeshaji 371 toka kanda zote saba za elimu.

(c) Ilitoa mafunzo mbalimbali kwa wakuza mitaala 33 na wafanyakazi waendeshaji 42.

(d) Iliandaa miongozo miwili ya kufundishia na kujifunzia Hisabati na Sayansi kwa shule za msingi.

(e) Ilifanya tathmini ya Mtaala wa Elimu ya Msingi.

(f) Ilirekebisha Mihtasari ya Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti kwa masomo yote na kuandikia moduli .za masomo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, TET itatekeleza mambo makuu yafuatayo:-

(a) Kuchapisha na kusambaza Mfumo wa Taifa wa Ukuzaji Mitaala *(National Curriculum Development Framework).*

(b) Kuendesha mafunzo kwa wawezeshaji wa MEMKWA mwaka wa pili na wa tatu na kufanya tathmini ya ufundishaji wa masomo sita ya MEMKWA.

(c) Kufaragua visanduku viwili vya Sayansi na Maarifa ya Jamii kwa shule za msingi.

(d) Kuboresha mtaala wa elimu ya msingi.

(e) Kugharimia mafunzo ya Wakuzaji Mitaala 3 na waendeshaji 3.

(f) Kuandika *Instructional Manual* ya masomo ya *Arts, Crafts,*Muziki na Michezo.

(g) Kuitisha mikutano 12 ya majopo ya masomo.

(h) Kuandika *Instructional Manual* mbili kwa ajili ya shule za msingi na shule za awali.

(i) Kurekebisha mihtasari ya sekondari na ualimu ngazi ya Stashahada.

(j) Kuandika *Methods Manuals* kwa ajili ya walimu.

(k) Kutayarisha Moduli tatu za chati za masomo ya Sayansi, Hisabati, Maarifa Jamii na Stadi za Kazi kwa shule za msingi.

(l) Kuandaa na kurekodi vipindi vinne vya masomo sita ya shule za msingi katika redio na televisheni.

(m) Kuandika miongozo miwili ya kufaragua zana zinazotumika kufundishia na kujifunzia.

(n) Kufanya semina tatu za taaluma kwa wakuza mitaala.

(o) Kununua gari moja kwa ajili ya usimamizi, utafiti na ufuatiliaji.

(p) Kuendesha semina sita za wakuu wa shule za msingi na sekondari.

(q) Kuandika na kuchapisha maandiko kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na madhara yake pamoja na kujumuisha mada za UKIMWI katika baadhi ya masomo ya shule za msingi na sekondari.

(r) Kununua vifaa mbalimbali kwa ajili ya Kituo cha Maarifa Kielimu, Vyumba vya majaribio ya Sayansi na kuboresha mandhari katika maeneo ya TET.

(s) Kuchapisha na kusambaza kijarida cha TET *(TIE Newsletter)* na jarida la *Tanzania Educational Journal (TEJ).*

(t) Kununua vitabu vya Dewey Decimal Classification kwa ajili ya maktaba ya TET.

(u) Kuendesha semina za kuwahisisha *(sensitize),* wafanyakazi kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na athari zake.

(v) Kujaribisha, kurekebisha na kusambaza maandiko kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na madhara yake katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo Elimu ya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) imetekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Imekarabati majengo ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika Mkoa wa Morogoro (WAMO).

(b) Imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 12 kuinua viwango vya elimu.

(c) Imetoa nakala 1,000 za majarida ya *Studies in Adult Education No. 60* na *Journal of Adult Education No. 12.*

(d) Imeboresha masomo ya Elimu kwa Njia ya Posta kwa kuhariri na kuchapa makala za Historia na Kiswahili.

(e) Imeendesha mafunzo ya cheti cha sheria kwa wanafunzi 166, stashahada ya Elimu ya watu Wazima 159 na mafunzo ya ushonaji 12.

(f) Imenunua kiwanja Mkoa wa Dar es Salaam cha kujenga kituo cha elimu ya kujiendeleza pamoja na jengo la ofisi ya kituo cha Sumbawanga.

(g) Imerekebisha mihtasari ya mafunzo ya Cheti na Stashahada ya juu ya EWW.

Katika mwaka 2004/2005, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza mpango wenye mambo yafuatayo kwa lengo la kuimarisha utoaji wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya Kujiendeleza nje ya mfumo rasmi kwa walioikosa walipokuwa katika umri sahihi wa kuwa shuleni:-

(a) Kuendesha mafunzo ya Stashahada ya EWW kwa watendaji 150.

(b) Kuimarisha, kurekebisha na kuchapa masomo kwa Njia ya Posta.

(c) Kutoa mafunzo kwa wakufunzi na walimu wa muda 200.

(d) Kuongeza wanafunzi wa Elimu ya Sekondari kwa Njia ya Posta kutoka 4,000 hadi 10,000.

(e) Kutoa majarida ya *Studies in Adult Education No. 61* na *Journal of Adult Education 13,* nakala 1000.

(f) Kuongeza wanafunzi wa mafunzo ya Cheti cha Sheria kutoka166 hadi 250.

(g) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kulingana na mahitaji kwa washiriki 200.

(h) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa TEWW 60.

(i) Kukarabati vituo vya Iringa na Tabora.

(j) Kujenga/kununua majengo kwa ajili ya vituo vya TEWW.

(k) Kuajiri wakufunzi 20 ili kuimarisha utendaji mikoani na Makao Makuu.

(l) Kuimarisha kitengo cha Utafiti na kununua magari matatu kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za Taasisi mikoani.

(m) Itaendelea kutoa elimu ya UKIMWI kwa jamii kwa kuendesha kampeni ya kitaifa ambayo inawalenga wananchi vijijini ambao hawapati taarifa sahihi juu ya mbinu za kupambana na janga la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Iliongeza vitabu 37,759 katika maktaba.

(b) Ilitembelea shule na taasisi mbalimbali 227 kwa ajili ya kuhamasisha.

(c) Iliendesha kambi za kujisomea katika vituo 5 vya Korogwe, Singida, Tukuyu, Kilosa na Songea.

(d) Iliendesha Tamasha la Wiki ya Vitabu katika vituo 10 vya Maktaba za mikoa.

(e) Ilitoa matangazo ya zabuni kwa ajili ya ukarabati maktaba za Kagera na Tabora pamoja na kuboresha Maktaba ya Mwalimu Julius Nyerere ya Butiama.

(f) Iliendelea na ujenzi wa Maktaba ya Mkoa wa Dodoma.

(g) Ilitoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 57.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, BOHUMATA itatekeleza mambo yafuatayo katika mpango wake wa kuendeleza maktaba nchini:-

(a) Kuimarisha na kuboresha huduma kwa kuongeza machapisho 40,000.

(b) Kuendeleza ujenzi wa maktaba ya Mkoa wa Dodoma.

(c) Kujenga majengo mahsusi ya Chuo cha Ukutubi na UhifadhiNyaraka, Bagamoyo.

(d) Kuendesha Tamasha la Wiki ya Vitabu katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Iringa, Mbeya, Songea, Tabora, Singida, Musoma, Mwanza na Morogoro.

(e) Kuendesha warsha na semina 4 za kuongeza uelewa na athari za UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Baraza la Mitihani liliendesha mitihani ya Kitaifa ya kumaliza Elimu ya Msingi ya Darasa la VII Tanzania Bara, Elimu ya Sekondari ya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita na Mitihani ya Ualimu Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mtihani wa Kitaifa wa kumaliza Elimu ya Msingi, yaani Darasa la VII mwaka 2003 kati ya watahiniwa 490,018 waliofanya mtihani waliofaulu walikuwa 196,273 sawa na 40.1% ikilinganishwa na 133,674 sawa na 27.1% waliofaulu mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne mwaka 2003, kati ya watahiniwa 54,904 wa shule, waliofaulu katika Daraja I, II na III walikuwa 23,751 sawa na 38.1% ikilinganishwa na 17,939 sawa na 36.2% waliofaulu mwaka 2002. Nawapongeza wakuu wa shule na walimu wote waliohusika na ongezeko la waliofaulu 5,812 pamoja na wanafunzi husika wote 23,751.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka 2003 unaonesha kuwa juhudi za kuboresha Elimu ya Sekondari zinazaa matunda mema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mtihani wa Kitaifa Kidato cha Nne mwaka 2002/2003 kati ya watahiniwa 12,003, waliofaulu katika Daraja I, II na III walikuwa 10,584 sawa na 88.2% ikilinganishwa na 9,992 sawa na 86.3% waliofaulu mwaka 2001/02.

Mheshimiwa Spika, katika mitihani ya Ualimu ya mwaka 2003 waliofaulu walikuwa 18,522 sawa na 94.7% ya watahiniwa wote 19,569. Katika mitihani ya Elimu ya Ufundi ya mwaka 2003 waliofaulu walikuwa 514 sawa na 54.6% ya watahiniwa 942 wa mitihani hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, BAMITA imetekeleza mambo muhimu yafuatayo yaliyopendekezwa na Tume Maalumu ya Serikali iliyochunguza mianya ya uvujaji wa mitihani miaka iliopita:-

(a) Ujenzi wa Jengo la Usajili wanapofikia wageni bila kuingia ofisi zingine za Baraza la Mitihani Tanzania.

(b) Ukarabati wa jengo la Kitengo cha Chapa na Uchapishaji.

(c) Ununuzi wa baadhi ya mashine za uchapaji mitihani.

(d) Ununuzi wa baadhi ya kompyuta na vifaa vyake kwa ajili ya kuandaa Kuweka mtandao wa Kompyuta *(Local Area Network - LAN),* kwa madhumuni ya kutoa huduma bora.

(e) Kufanya maandalizi ya awali ya ujenzi wa kituo cha Usahihishaji Mitihani Mbezi Wani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji huo ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kuanzia mwaka 2003, mitihani ya Kitaifa ya Darasa la VII, Kidato cha Nne na Kidato cha sita imeanza kuchapwa hapa nchini kwa usalama.

Katika mwaka 2004/2005, Baraza la Mitihani la Tanzania limejiandaa kwa ukamilifu zaidi kutekeleza wajibu wake wa kutunga na kuendesha mitihani yote ya Kitaifa kwa ufanisi unaohitajika, ikiwa ni pamoja na kuendesha na kusimamia mitihani itolewayo na Bodi tisa za mitihani ya nje. BAMITA itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Litafanya utafiti, tathmini, usanifu na ukuzaji mitihani mbalimbali ya kitaifa.

(b) Litaendesha mitihani ya: kumaliza Elimu ya Msingi; Maarifa *(Qualifying Test),* Kidato cha Nne na Sita, kuhitimu Elimu ya Ualimu Daraja la A na Stashahada *(Diploma)* ya Ualimu.

(c) Litaendesha mitihani ya Cheti cha Ufundi Sanifu *(Full Technician Certificate - FTC)* na Stashahada ya juu ya Uhandisi kwa niaba ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

(d) Litasimamia mitihani ya nje inayofanywa na watahiniwa hapa nchini.

(e) Litaendeleza ujenzi wa Kituo cha Kusahihishia Mitihani.

(f) Litatengeneza programu ya kompyuta itakayowezesha utoaji wa matokeo ya kufaulu mtihani wa Kidato cha Nne na uchaguzi wa wanafunzi wa kuingia Kidato cha Tano kwa pamoja ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), lilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Lilitoa elimu ya sanaa na uongozi kwa wasanii 104 katika taaluma zifuatazo:-

Uongozi wa vikundi, sarakasi, majukwaa, uingizaji, utengenezaji ala za muziki wa kiasili, ubunifu wa ngoma na miondoko, Utawala Bora na utunzi wa nyimbo za kuhamasisha maendeleo ya jamii

(b) Lilihamasisha Umma kutambua na kuthamini sanaa kwa kupitia mashindano ya kuchora, nyimbo za halaiki, matamasha ya sanaa kwa watoto na watu wazima.

(c) Liliendesha kwa kushirikiana na *Baraka Women Group,* mafunzo ya kuimarisha miradi kwa kazi za ufundi wa mikono kwa akina mama katika mikoa ya Dodoma, Morogoro na Tanga.

(d) Liliendesha warsha na semina juu ya elimu ya Hakimiliki na Hakishiriki kwa wasanii 304 Mikoa ya Dar es Salaam , Dodoma, Morogoro na Tanga.

(e) Lilikamilisha michoro ya ujenzi wa ukumbi wa wazi *(Open Air Theatre)* na kuiwasilisha kwa Mhandisi wa Halmashauri ya Jiji kwa uhakiki.

(f) Liliendelea na ujenzi wa ukuta kuzunguka eneo la BASATA ambapo asilimia 75 imekamilika.

(g) Lilitoa elimu ya UKIMWI kwa mikoa minne kwa kuendesha mashindano ya kuchora, maonyesho, matamasha na mashindano ya sanaa.

Katika mwaka 2004/2005, BASATA litatekeleza mpango wenye mambo yafuatayo ya kukuza sanaa:-

(a) Litakuza ujuzi, elimu ya kisanii kwa wasanii wa ufundi, maonyesho na muziki kwa kuendesha kozi fupi fupi 27.

(b) Litaendelea kutoa elimu ya Hakimiliki na Hakishiriki kwa wasanii 600, wakuzaji sanaa 90 na viongozi 13 wa vyama vya sanaa.

(c) Litahimiza jamii kuthamini na kuboresha muziki, kuanzisha/kuimarisha matamasha, halaiki na mashindano ya sanaa mbalimbali vijijini.

(d) Litaendesha Elimu ya Uongozi na Bajeti kwa watendaji 10.

(e) Litaanzisha ujenzi wa ukumbi wa wazi *(Open Air Theatre)*.

(f) Litakamilisha ujenzi wa uzio.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Baraza la Kiswahili la Taifa limetekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Lilisanifu Istilahi mpya za mchanganyiko kwa ajili ya kuziba pengo la msamiati katika mawasiliano ya kila siku Serikalini, mashirika na sekta binafsi na kuzisambaza kwa watumiaji kupitia vyombo vya habari.

(b) Lilikusanya na kusahihisha makosa kutoka vyombo mbalimbali vya habari na kuyawasilisha katika sehemu husika ili wayazingatie.

(c) Liliendesha semina kwa wafasiri, wakalimani, waandishi wa habari na watayarishaji wa vipindi vya Redio na Televisheni.

Katika mwaka wa 2004/2005, Baraza la Kiswahili la Taifa litatekeleza mambo yafuatayo katika kukuza Kiswahili:-

(a) Litafanya maadhimisho ya Nane ya Siku ya Kiswahili kwa kushirikiana na asasi mbalimbali za Kiswahili, kuwatunukia na kuwaenzi waliochangia maendeleo ya Kiswahili kwa kuzingatia kauli mbiu ya "Kiswahili na Janga la UKIMWI, 2004/2005".

(b) Litaendeleza vuguvugu la kuhamasisha matumizi ya Kiswahili kwenye sekta ya biashara na viwanda kwa kufanya utafiti kupitia Shirika la Viwango Tanzania.

(c) Litaratibu matumizi fasaha ya Kiswahili kwa vyombo vya habari kwa kuendesha Semina kwa Wahariri wa Vyombo vya Habari.

(d) Litaendesha Warsha ya Kusanifu Istilahi 250 mchanganyiko ili kuziba pengo la msamiati na kuleta uwiano wa matumizi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imebaini matatizo yafuatayo:-

- Baadhi ya Halmashauri zimeonesha udhaifu katika kutoa taarifa za utekelezaji na kutokufunga hesabu za mwaka za fedha za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) kwa wakati, jambo ambalo ni kinyume na sheria, kanuni na taratibu za usimamizi bora wa fedha za umma. Kasoro hii sharti irekebishwe mara moja kwa kuimarisha mfumo wa ukaguzi wa ndani. Udhaifu huu umesababisha kuchelewa kwa fedha za mwaka wa tatu kutoka kwa wahisani. Kila Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na Maafisaelimu (Wilaya) warekebishe kasoro hii.

- Bado baadhi ya Wakurugenzi wa Halmashauri hawataarifu Walimu Wakuu na Kamati za Shule kiwango kilichotolewa kwa kila mwanafunzi cha Ruzuku ya Uendeshaji iliyopokelewa kutoka Serikali Kuu. Narudia maagizo yangu ya mwaka jana kuwa lazima Walimu Wakuu na Kamati za Shule wapewe taarifa hiyo ili wafuatilie fedha zao kulingana na jumla ya wanafunzi walionao ili wazipangie matumizi.

Baadhi ya Halmashauri kuendelea kutokuzingatia vigezo sahihi katika ujenzi na uendeshaji wa Shule za Msingi, hivyo naagiza tena:-

(a) Ujenzi wa majengo ya madarasa na nyumba za walimu uzingatie vipimo sahihi vilivyoelekezwa na Wizara.

(b) Ukubwa wa Shule ya Msingi kwa wingi wa wanafunzi vijijini usizidi mikondo miwili yaani wanafunzi 40 wa mkondo mmoja x mikondo 2 x 7 (D I-VII)= wanafunzi 560 na Mijini usizidi mikondo mitatu yaani 40 x 3 x 7= wanafunzi 840.

(c) Wingi wa Wanafunzi Darasani wasiwe zaidi ya wanafunzi 40 wa umri sawa au karibu sawa ili wafundishike vizuri kwa kasi moja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara yangu itatekeleza maamuzi yafuatayo:-

(a) Kupunguza ada ya wanafunzi wa kutwa wa Elimu ya Sekondari kutoka Shilingi. 40,000/= na kuwa Shilingi 20,000/= kwa mwaka na Kutoa Ruzuku ya Uendeshaji ya Shilingi 20,000 kwa mwanafunzi kwa Sekondari za kutwa za Serikali kufidia punguzo la ada.

(b) Kujenga Maabara na Maktaba katika Shule za Sekondari za Serikali zinazojengwa na wananchi kwa tenda ya Serikali.

(c) Kuimarisha Mitaala ya Elimu ya Sekondari kwa kuingiza Elimu ya Kujitegemea; na Stadi za Kazi na Masuala Mtambuka *(Cross-cutting Issues)* katika kila somo na kupunguza idadi ya masomo yatolewayo kutoka 13 kuwa 8 ili kubakia na masomo ya msingi *(Core subjects) Civics,* Kiswahili,*English, Mathematics, Biology, History, Geography, Physics* na *Chemistry.* Masomo ya hiari *(options)* yaani *Home Economics, Computing and Information Science, Music, Fine Art, French, Arabic, Bible Knowledge, Islamic Studies, Pysical Education* na *Additional Maths* yatafundishwa katika shule zitakazoteuliwa kwa ajili hiyo.

(d) Kupeleka fedha na madaraka ya ununuzi wa vitabu vya kiada na ziada kwa Kamati za Shule, badala ya Halmashauri ili kuboresha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kufikia kitabu kimoja kwa mwanafunzi katika shule zote za msingi za Serikali

(e) Kutoa Ruzuku ya uendeshaji ya Shilingi 10,000 kwa mwanafunzi kwa Shule za Sekondari zisizo za Serikali ambazo sio za kibiashara na siyo seminari.

(f) Kutoa Ruzuku ya maendeleo kwa wananchi wanaojenga sekondari ya Shilingi milioni 7.0 kwa darasa na Shilingi milioni 9.0 kwa nyumba ya mwalimu na kusaidia ujenzi wa Hosteli. Aidha, aliyeidhinishwa kuendesha Sekondari kwa ajili ya walemavu atapewa Ruzuku viwango hivyo hivyo vya Ruzuku ya maendeleo.

(g) Kusambaza nakala za kutosha za miongozo yote muhimu ya MMEM na MMES kwa kila Halmashauri na shule zote za msingi na sekondari nchini.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya mwaka 2003/2004, yametokana na ushirikiano mkubwa uliotolewa na wananchi kwa mchango wao wa hali na mali katika kushiriki na kuchangia mipango ya elimu na utamaduni. Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu sehemu kubwa ya maendeleo katika Sekta ya elimu hutokana na moyo wa kujitolea katika kujenga majengo ya shule hususan madarasa na Nyumba za Walimu.

Nachukua fursa hii kuwapongeza wananchi pamoja na viongozi wote wa Mikoa, Wilaya, Vijiji pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani kwa mchango wao walioutoa katika kufanikisha ujenzi wa shule na utoaji na uendeshaji wa elimu na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, nazishukuru nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa kwa michango yao katika kuandaa na kufanikisha utekelezaji wa mipango ya elimu na utamaduni katika mwaka 2003/2004. Nchi hizo rafiki na wahisani ni Sweden, Japan, Norway, Uingereza, Ufaransa, Ireland, Uholanzi, Finland, Canada, Ujerumani, Ubelgiji, China na Korea ya Kusini.

Mashirika yaliyochangia elimu na utamaduni ni Benki ya Dunia, *ADB, SIDA, NORAD, GTZ, DFID, WFP, UNICEF, UNESCO, UNFPA , UNDP, CIDA, ILO, EU, JICA, USAID, JOVC, VSO,Celtel, CBP, Peace Corps, Book Aid International, Aga*

*Khan Education Foundation, Plan International, World Vision, Ireland Aid, Care International* na Mashirika mbalimbali yasiyokuwa ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na misaada utekelezaji wa mipango ya elimu na utamaduni kwa mwaka 2003/2004, haungefanikiwa na kukamilika katika kiwango nilichoelezea bila jitihada, ushirikiano na uongozi wa pamoja katika Wizara yangu. Natoa shukrani zangu za pekee kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Bujiku K. P. Sakila, Mbunge wa Jimbo la Kwimba, kwa ushirikiano, uaminifu na uadilifu wake aliouonesha kwangu na kwa viongozi wetu Wakuu na kwa ushirikiano wake na wenzetu wote Wizarani. Ninapenda pia kutoa shukrani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Bibi Mwatumu J. Malale, pamoja na wasaidizi wake akiwemo Afisa Elimu Kiongozi, Wakurugenzi wa Idara wote, Viongozi wa Elimu katika ngazi mbalimbali, Waalimu na Wafanyakazi wengine wote wa Wizara yangu, kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hususan jukumu mama la utoaji elimu na ukuzaji wa utamaduni kwa mwaka 2003/2004 na katika maandalizi ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu pia kwa Wenyeviti, Wakurugenzi Watendaji, Makatibu Watendaji na Wajumbe wa Mabaraza na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara yangu na wafanyakazi wengine wote katika ngazi mbalimbali kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuimarisha na kuendeleza elimu na utamaduni.

Pia, natoa shukrani na pongezi za pekee kwa uongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwa ushirikiano wao mzuri na ari yao ya kutatua matatizo ya walimu kwa kushirikiana na Wizara yangu na Serikali kwa ujumla.

Napenda kuwashukuru Viongozi wa Tawi la TUGHE la Makao Makuu ya Wizara kwa ushirikiano na ushauri wao katika kushughulikia masuala ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza yote hayo, ninaomba sasa Bunge lako Tukufu baada ya kuijadili hoja yangu pamoja na kuzingatia Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, lipitishe makadirio ya matumizi ya Shilingi 158,411,932,000 ili kuwezesha Wizara ya Elimu na Utamaduni kutekeleza mipango ya mwaka 2004/2005.

Kati ya fedha hizo Shilingi 52,811,648,100 zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na Shilingi 105,600,283,900 zinaombwa kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Mengi kaitika hoja haijapata kutokea. *(Makofi)*

Kuna Waheshimiwa Wabunge sita ambao hawajachangia kabisa tangu tumeanza. Nitaanza na hao katika hoja hii. Nao ni Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Ramadhani Khalfan, Mheshimiwa Maria Watondoha na Mheshimiwa Rhoda Kahatano, wajiandae kwamba ndio watakuwa wachangiaji wa mwanzo.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Utekelezaji Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha Uliopita na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilijadili Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa maeneo yafuatayo: -

(i). Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

(ii). Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mwaka wa Fedha 2003/2004; na

(iii) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu kwa mujibu wa Kanuni ya 88(1), Toleo la 2004, inapenda kutoa maoni na ushauri kwa nia ya kuboresha utendaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na dira ya Wizara inayolenga kuwa na Mtanzania aliyeelimika kwa kiwango cha juu, mwenye maarifa, mahiri na anayekomaa kiutamaduni ili aweze kukabiliana na changamoto za Kitaifa na Kimataifa katika nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi ifikapo mwaka 2025. Aidha, Kamati inaunga mkono dhima ya Wizara ya Elimu na Utamaduni inayolenga kuhakikisha kuwepo mazingira mazuri ya kisheria na kiutendaji yatakayowezesha wadau wote wenye nia na uwezo wa kutoa elimu iliyo bora, washiriki kupanua elimu hiyo katika ngazi zote na kutoa fursa sawa kwa wote.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka 2003/2004, hasa katika utekelezaji wa Mpango wa MMEM unaohusu Ujenzi wa Madarasa, Nyumba za Walimu, Matundu ya Vyoo na Ununuzi wa Samani na Vifaa vya Kufundishia na

Kujifunzia. Vilevile, kwa mafanikio yaliyofikiwa katika kuandikisha wanafunzi katika Shule za Msingi hasa darasa la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono hatua ya Serikali ya kuandaa na kuajiri walimu katika Shule za Msingi na Sekondari na kukidhi mahitaji ya ongezeko la wanafunzi katika kutekeleza mpango wa MMEM. Aidha, utekelezaji wa mpango huo ni pamoja na kuwahamisha baadhi ya Walimu hasa kutoka shule moja hadi nyingine na kuweka uwiano mzuri wa Walimu katika shule za mijini na vijijini na kuweza kuinua ubora wa elimu katika shule zote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, wakati Kamati yangu ikiendelea na uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, (Fungu 46), ilipokea kilio cha Walimu kutoka Chama cha Walimu Tanzania (CWT), ambayo takwimu zake ilionyesha kuwa walimu wana madai yaliyofikia Shilingi za Tanzania bilioni 18.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilishtushwa na kuguswa na suala hili na kubaini kuwa, madai na kero za walimu zinatokana na mambo yafuatayo: -

(i) Uhamisho usiozingatia kanuni na taratibu zilizoko;

(ii) Kutolipwa kwa fedha za likizo kama inavyotakiwa;

(iii) Kutolipwa kwa fedha za masomo wakati wanajiendeleza kielimu;

(iv) Malimbikizo ya mishahara;

(v) Mapunjo ya mishahara baada ya kupandishwa madaraja;

(vi) Fedha za matibabu ambazo walimu wanadai kwa magonjwa ambayo hayako katika orodha ya Mfuko wa Bima za Afya;

(vii) Bima zilizoiva kutolipwa na Shirika la Bima;

(viii) Ucheleweshaji wa mishahara na posho ya kujikimu kwa ajira mpya;

(ix) Kero zinazohusiana na malipo ya kustaafu;

(x) Kero ya malipo yasiyolipwa ya walimu wa madarasa ya MEMKWA;

(xi) Walimu wanafunzi daraja la III A waliopo katika mwaka wa mazoezi kutolipwa posho zao kwa wakati na inasemekana wengine hawajalipwa tangu Januari, 2004 hadi sasa inapata karibu miezi sita; na

(xii) Kutokuwepo mazingira mazuri ya kufundishia katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, hali hii inapelekea baadhi ya Walimu kulazimika kuishi maisha yasiyotazamiwa na kwa kweli walimu wa kike wako katika mazingira magumu zaidi na hivyo kuwa kwenye hatari ya kudhalilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaiambia Serikali kwa uwazi na ukweli kuwa, ni vigumu katika hali hii kujenga mazingira ya vijana kuipenda kazi ya ualimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hii, Kamati yangu iliunda Kamati Ndogo kwa mujibu wa kanuni ya 88(12), Toleo la 2004, kufuatilia madai haya ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, Kamati hiyo tayari imekutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, mwenye fungu 56 inayohusu maslahi ya Walimu wa Shule za Msingi na na imepanga kukutana na Waziri wa Fedha, Waziri wa Elimu na Utamaduni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za awali, Kamati imebaini matatizo yafuatayo: -

(i) Kuwepo kwa mawasiliano hafifu ndani ya Serikali yenyewe kutokana na ajira za Walimu kushughulikiwa na Wizara nne na hivyo kufanya maslahi yao na ajira yao kuwa kwenye mafungu tofauti hasa TAMISEMI, Wizara ya Elimu na Utamaduni na Menejimenti ya Utumishi wa Umma; *(Makofi)*

(ii) Mawasiliano hafifu kati ya Serikali na Chama cha Walimu (CWT) hasa katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya;

(iii) Upo uwezekano wa uzembe wa wazi na urasimu unaokwamisha Walimu kupata haki zao katika muda unaotakiwa; na

(iv) Katika mlolongo wa urasimu wa ajira za Walimu na maslahi yao, upo uwezekano wa ubadhirifu mkubwa unaofanywa na Watendaji wa Serikali kupitia migongo ya Walimu na si ajabu wapo waliobuni mradi huu kwa kuandaa *pay rolls* mbili. Moja yenye mishahara halali na nyingine yenye mishahara ya kuibiwa. Hali hii imethibitishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati wa hoja ya Bajeti ya Serikali pale alipotaja wizi wa kalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ya Huduma za Jamii ikiendelea na kazi hii, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa kauli hapa Bungeni wakati wa hoja yake, jinsi atakavyolishughulikia tatizo la Walimu ambalo limesemewa sana na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hatua yake hii ya awali na kwa kutoa maagizo yafuatayo ambayo tunayarudia kwa faida ya wote:-

(i) Kwamba Serikali imetenga Shilingi bilioni tisa kwa ajili ya kulipia madai ya Walimu na kuwa iwapo madai yatazidi kiwango hicho yatalipwa kutoka *Contigency Fund* ya Hazina; *(Makofi)*

(ii) Kwamba madai ya Walimu ambayo tayari yamehakikiwa yalipwe pamoja na mishahara yao ya mwezi Julai, 2004;

(iii) Kwamba Wakuu wa Mikoa wapeleke haraka timu za kuchunguza jinsi madai ya Walimu yalivyoshughulikiwa katika Halmashauri za Wilaya na taarifa imfikie ifikapo tarehe 31 Julai, 2004 ambayo ni baada ya wiki tatu tangu leo;

(iv) Kwamba waliokula fedha za Walimu wajisalimishe mapema; na *(Makofi)*

(v) Kwamba Waziri Mkuu naye ataunda Tume ya kuchunguza tatizo hili na atatoa taarifa katika Mkutano ujao wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kauli hii aliyoitoa Waziri Mkuu, Kamati ya Huduma za Jamii sasa inatoa nafasi kwa Serikali kufuatilia tatizo hili hadi itakapotoa taarifa yake Bungeni katika Mkutano ujao. Hata hivyo, Kamati inataka taarifa ya Serikali izingatie mambo yafuatayo: -

(i) Fedha kiasi gani zilitolewa kulipia madai ya Walimu, kiasi gani zililipwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa na kiasi gani zilitumika isivyotazamiwa na kiasi gani ziliibiwa; *(Makofi)*

(ii) Ni nani waliohusika;

(iii) Hatua gani zimechukuliwa au zitachukuliwa dhidi yao; *(Makofi)*

(iv) Kiasi gani na kwa utaratibu gani madeni yote ya Walimu yatalipwa;

(v) Serikali imefikiria nini sasa kuhusu mlolongo mrefu wa ajira za Walimu; na *(Makofi)*

(vi) Hatua gani zimechukuliwa kuziba kabisa mianya ya ubadhirifu wa fedha za Walimu katika ngazi zote hasa ya Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwa dhati kabisa kuwa, Serikali ikomeshe kabisa wenye mazoea ya baadhi ya watendaji kupuuza au kuchezea maagizo yake. Ni vyema wahusika sasa waelewe kuwa maagizo na maelekezo yaliyotolewa na Waziri Mkuu yamekubaliwa na Bunge na kwa lugha nyingine ni maamuzi ya Bunge, hivyo, hayapaswi kupuuzwa au kuchezewa na mtendaji wa ngazi yoyote ya Serikali. Tunaitakia Tume ya Waziri Mkuu kazi njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa shule ni muhimu katika kutathmini maendeleo ya shule na kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Aidha, ukaguzi wa shule ni njia ya kuleta uwajibikaji katika uendeshaji wa shule. Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(i) Kasi *(rate)* ya ukaguzi iongezwe kwa kutoa mafunzo zaidi kwa Wakaguzi ngazi za Wilaya na Kanda;

(ii) Serikali itenge fedha zaidi kwa ajili ya kufanikisha ukaguzi badala ya kuziachia shule na vyuo;

(iii) Taarifa ya Ukaguzi irejeshwe kwenye Halmashauri, Kamati za Shule na wadau wengine ili maeneo yenye udhaifu yaweze kuboreshwa na hatua zaidi kuchukuliwa; na

(iv) Idara ya ukaguzi sasa ipewe kipaumbele kwa kupewa usafiri hasa magari walau kila Wilaya iwe na gari moja kama kweli tumedhamiria kusimamia ubora wa elimu na siyo bora elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utelelezaji wa MMEM, shule zetu nyingi bado zinakabiliwa na tatizo la miundombinu hafifu, hali inayopelekea uduni wa elimu inayotolewa. Kamati yangu inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wahisani, Mashirika ya Umma na Watu binafsi, kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia hususan ujenzi na ukarabati wa madarasa na nyumba za Walimu, maabara, kusambaza vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Kamati pia inashauri kuwa, Serikali iendelee kuunga mkono Wananchi walioonyesha mafanikio katika ujenzi wa madarasa katika Shule za Msingi na kuvuka malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kuandaa mpango maalum wa kuimarisha Elimu ya Sekondari (MMES) ikiwa ni kuendeleza na kulinda mafanikio ya utekelezaji wa MMEM kuanzia mwaka huu wa fedha. Ni matarajio ya Kamati kuwa, Serikali itaanza maandalizi katika Vyuo vya Elimu ya Juu kupokea mafanikio hayo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa katika utekelezaji wa Mpango wa MMES, Serikali itoe upendeleo na kuona kuwa ujenzi wa Sekondari unafanyika katika maeneo yenye matatizo ya msingi yanayotokana na historia ya nchi yetu na mazingira ya kijiografia na kiuchumi. Vile vile, Kamati inashauri kuwa katika kutekeleza Mpango wa MMES, Serikali iwe makini na kuona kuwa matatizo au mapungufu yaliyojitokeza wakati wa kutekeleza mpango wa MMEM hayatokei katika mpango wa kuimarisha Sekondari na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa njia bora ya kuimarisha na kuendeleza elimu katika ngazi zote ni Serikali na Wananchi kujenga uchumi imara, unaokua, wenye uwezo wa kukabiliana na mahitaji ya jamii. Pia, Kamati inaamini kuwa bado idadi ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Juu ni ndogo kutokana na kiu ya Wananchi na hata tukijilinganisha na nchi zingine. Hivyo, pamoja na kazi nzuri

inayofanyika kuimarisha elimu chini ya MMEM na MMES, ni vema pia Serikali ikatafakari njia bora ya kuwa na mipango endelevu kwa fedha zetu za ndani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kupunguza ada kwa Shule za Sekondari, Kamati inashauri kuwa, ni vema ada ya Shule za Sekondari ikaondolewa kabisa kwa mtazamo wa kuhakikisha kuwa tunafikia asilimia 50 ya watoto watakaokwenda Sekondari na kumaliza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya sasa utaratibu wa kila mwanafunzi kulipa ada hata kwa kiwango hicho kidogo kilichoamuliwa, bado utaleta adha tu kwa watoto zaidi ya asilimia 50 kwa makisio na kwa hali ya umaskini uliopo wazazi wao hawatakuwa na uwezo na hivyo wengi wataacha shule na hasa ukizingatia kuwa mara zote Wakuu wa Shule za Sekondari watakuwa wakiwasumbua sana kwa kuwarudisha nyumbani kufuata ada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la ada litashusha kiwango cha taaluma kwani sasa tumefikia mahali kuwafanya Wakuu wa Shule za Sekondari wawe kama wakusanyaji ushuru *(Revenue Collectors),* badala ya kazi yao ya kusimamia taaluma (kama walivyokuwa Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji kuwa wakusanyaji kodi ya maendeleo na ushuru mbalimbali badala ya kusimamia maendeleo). Vinginevyo, Wakuu wa Shule wasiposaka ada watashindwa kuendesha shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaiasa Serikali kuacha mtindo huu. Ni vema Serikali ikatoa fedha *(Warrant of Funds)* za kuendesha shule kulingana na bajeti ya shule kama ilivyokuwa zamani ili wakuu hawa wasimamie elimu badala ya kufukuzana na wanafunzi pamoja na wazazi wasiokuwa na uwezo wa kulipa ada. Vinginevyo, Serikali itafute chanzo kingine cha fedha badala ya ada na tunaishauri Serikali ifanye utafiti zaidi wa adha hii ya ulipaji wa ada na Wakuu wa Shule kuwa wakusanyaji wa ada kama tunataka kuondoa kero hii kwa dhati badala ya maagizo kwa Wakuu wa Shule ambao hawana njia zaidi ya kukiuka maagizo haya mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inalipongeza Baraza la Mitihani la Taifa kwa kazi nyeti na nzuri inayofanya. Aidha, tunaipongeza Serikali kwa kuimarisha utendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa kufikia kiwango cha sasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, Kamati imebaini kuwa Baraza la Mitihani linakabiliwana matatizo ambayo yanahitaji hatua za Serikali kama ifuatavyo: -

(i) Bajeti ya Baraza la Mitihani inaathiriwa sana na utaratibu wa Mamlaka ya Kodi *(TRA)* kutoza kodi vifaa vya mitihani; na

(ii) Vyombo vya kusambazia mitihani vimechakaa mno, magari ya kusafirishia mitihani yamechoka sana na vitendea kazi ni vichache mno kulingana na ongezeko la wanafunzi. Pia, wataalam wengi ili kuongeza ufanisi wa kazi hii nyeti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Serikali imeimarisha Elimu ya Msingi na kuanzia mwaka huu wa fedha itaimarisha Elimu ya Sekondari na kuongeza idadi ya watahiniwa, vivyo hivyo ukubwa wa kazi za Baraza la Mitihani unaongezeka. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuimarisha na kuboresha uwezo wa Baraza hilo ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, pia, kumekuwepo na maelezo mbalimbali kutoka kwa wadau na wazazi kuwa Baraza la Mitihani limekuwa likichelewesha kutoa matokeo ya uchunguzi wa tuhuma mbalimbali za ukiukwaji wa taratibu za mitihani. Hivyo, Kamati inashauri Baraza la Mitihani kukamilisha kazi ya uchunguzi na kutoa haki mapema iwezekanavyo ili wale ambao wataonekana hawana hatia wasipoteze nafasi yao ya kuendelea na masomo kwa mwaka wa taaluma unaohusika. Kamati inaomba Wizara ifuatilie jambo hili zaidi na itapenda kupata taarifa ya matukio hayo wakati wa kupitia kazi za utendaji wa Baraza la Mitihani. *(Makofi)*

Taasisi ya Elimu ni chombo muhimu kinachohusika na kuandaa na kukuza Mitaala ya Elimu kuanzia ngazi ya Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu, kudhibiti ubora wa zana zinazotumika kutekeleza mitaala, kutunga na kuchapisha mihtasari na kuunda na kusambaza zana za kufundishia mashuleni. Hata hivyo, Taasisi hii muhimu imekuwa ikitengewa bajeti finyu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, Taasisi ya Elimu Tanzania itengewe bajeti inayolingana na majukumu yake na ipewe jukumu la kutunga na kuthibitisha vitabu vya kufundishia katika ngazi za elimu zinazohusika kuziandalia mitaala badala ya utaratibu wa sasa wa kuachia watu wote kuandaa vitabu na kuidhinishwa na Kamati maalum kwani imedhihirika kuwa baadhi ya vitabu havikidhi matakwa ya mitaala iliyokubaliwa Kitaifa na pia husababisha kuwachanganya Wanafunzi na Walimu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa Taasisi hii ni vyema ikawa chombo cha Muungano, kwa kuzingatia kuwa ingawa Serikali ya Mapinduzi ina chombo cha kuandaa mitaala inayotumika Zanzibar, ngazi ya Elimu ya Sekondari huwa wanatahini kwa mitihani inayotungwa na Baraza la Mitihani la Taifa inayozingatia mitaala inayoandaliwa na Taasisi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa ili kuwatendea haki watahiniwa ni vizuri kuwepo makubaliano kati ya Serikali zote mbili kuhusu mitaala inayotumika nchini kote katika ngazi zilizotajwa hapo juu. Watalam hasa wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Wizara ya Elimu Zanzibar, Taasisi ya Elimu, Baraza la Mitihani Tanzania na Wadau wote wa Elimu, kutoa tathmini ya kitaalam ambayo itakidhi maslahi ya Serikali zote mbili juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuishauri Serikali kufanya juhudi za makusudi kufufua Elimu ya Watu Wazima kwani ingawa Bunge limekuwa linaidhinisha

fungu kila mwaka, Elimu ya Watu Wazima imekuwa haifundishwi na idadi ya wasiojua kusoma na kuandika imekuwa ikiongezeka.

Kamati inashauri kuwa, Kamati za Elimu ya Watu Wazima zifufuliwe katika ngazi zote, pamoja na kuwashirikisha wadau wote yaani Halmashauri za Wilaya, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, watu binafsi, katika kukusanya na kutumia rasilimali zilizopo kwa ajili ya kufanikisha Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ione umuhimu wa kuanzisha mikakati ya kuleta mabadiliko yanayoendana na wakati katika kutekeleza majukumu yake, kama kuanzisha tovuti yake na kurahisisha mawasiliano kati yake na wanafunzi kwa kutuma masomo kwa njia ya mtandao wa kompyuta.

Aidha, Kamati inashauri Taasisi hiyo kuanzisha mahusiano ya karibu kati yake na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania badala ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pekee katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zote mbili hasa katika maandalizi ya mitaala, kutoa elimu kwa masafa, kutunga na kusahihisha mitihani.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inapenda kushauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha vitendea kazi vya Taasisi ya Elimu ya Watu wazima hasa kitengo cha uchapaji ambacho kinatumia mashine zilizonunuliwa miaka ya 1970, kwa kiasi kikubwa zimechakaa sana na kupitwa na wakati. *(Makofi)*

Aidha, Kamati inaona kuwa kuna ulazima wa Serikali kuboresha maktaba na Taasisi hiyo ambayo hutumiwa na wanafunzi na wafanyakazi kwani machapisho mengi yamepitwa na wakati na hivyo kutowasaidia sana wanafunzi katika kujiendeleza kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai na Naibu wake, Mheshimiwa Bujiku Sakila, kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Bajeti pamoja na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha wa 2004/2005. *(Makofi)*

Aidha, nawapongeza Wataalam wote wa Wizara ya Elimu na Utamaduni wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Mwamtumu Malale, kwa ushirikiano waliotoa Kamati ilipokuwa inajadili fungu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa umakini na ushirikiano wao wakati wa kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa Mwaka wa Fedha uliopita na kufikiria Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati yangu waliochambua Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni (Fungu 46), kwa kuwataja majina. Wajumbe hao ni wafuatao:-

Mheshimiwa Dr. Aisha O Kigoda, ambaye ndiyo Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Alhaji Ahamadi H. Mpeme, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Oscar T. Mloka, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, Mheshimiwa Hamisi J. Nguli, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mheshimiwa Halimenshi K. Mayonga, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Khamis Ali Salehe na mimi Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mwisho, nampongeza Katibu wa Bunge na Katibu wa Kamati hii kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KHAMIS ALI SALEH - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa mkono wa pole kwa wafiwa wote. Pia, natoa mkono wa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, kwa kifo cha ghafla. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa mwaka wa fedha 2004/2005, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 43(5)(b)(c).

Mheshimiwa Spika, Dira ya Wizara ya Elimu na Utamaduni ni kuwa na Mtanzania aliyeelimika kwa kiwango cha juu. Wajibu mkubwa wa Wizara katika dira hiyo ni kuhakikisha kuwa, kuna mazingira mazuri ya kutoa elimu bora kwa Watanzania. Mazingira ni pamoja na maslahi bora ya ualimu, madarasa, madawati, vitabu, nyumba za Walimu, bajeti pana ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na kadhalika. Tunaipongeza Kamati ya Huduma za Jamii kwa sababu kama tulivyoshuhudia, imekuwa ikitoa maoni na maagizo ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi na Wizara husika ili kuboresha mazingira ya kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003, Wizara ilitengewa Shilingi bilioni 45.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, lakini kufikia tarehe 30 Aprili, 2004 Wizara ilipatiwa asilimia 68 tu ya fedha zilizotengwa. Pia, Shilingi bilioni 57.8 ziliidhinishwa kwa matumizi ya shughuli za maendeleo. Lakini fedha zilizopatikana ni 74.6% ya fedha zilizotengwa kufikia tarehe 30 Aprili, 2004.

Mheshimiwa Spika, hili tatizo la kutoa pesa pungufu kwa Wizara mbalimbali limekuwa la kawaida. Mahitaji halisi ya Wizara hayawezi kutekelezwa kutokana na kutoa pesa nusu nusu. Sio hivyo tu, bali mara nyingi fedha zinazoidhinishwa hazitolewi kwa wakati au wakati mwingine nyingi hutolewa mwishoni mwa karibu kufunga mwaka na hivyo kutumika ovyo na bila usimamizi makini.

Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iwe inaidhinisha kiasi cha pesa ambacho ina uhakika kitatolewa kwa wakati. Serikali isiwafurahishe Wabunge na Wananchi kwa tarakimu ambazo hazitekelezeki. Hata yule kuku wa kienyeji huwa anadonoa kile ambacho ana uhakika wa kukimeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunza ni pamoja na ujenzi wa madarasa bora. Uwiano wa darasa bora ni 1:40. Wizara iliijulisha Kamati ya Huduma za Jamii kuwa sasa hivi uwiano wa darasa kwa wanafunzi Kitaifa ni 1:80. Kwa hiyo, bado kuna upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa pamoja na vyoo vya kudumu. Si hivyo tu, bali mojawapo ya matatizo yanayoikabili Wizara ni kwamba, baadhi ya Halmashauri zinashindwa kuzingatia viwango vya ujenzi. Hii ni pamoja na kushindwa kuzingatia vigezo vya kuendesha shule kama idadi ya wanafunzi katika darasa na idadi ya mikondo kwa kila shule.

Mheshimiwa Spika, huu ni mchezo wa kubebeshana lawama kwa sababu ni kweli kuwa vyumba vya madarasa havitoshi. Pia, Walimu Wakuu hawatakiwi kumkataa mtoto yeyote aliyefikisha umri wa kwenda shule. Sasa kama idadi ya watoto walioandikishwa ni kubwa kuliko uwezo wa shule, je, vigezo vya idadi ya wanafunzi na mikondo vitazingatiwaje? Katika suala hili tusiwalaumu Walimu Wakuu kwa sababu ni tatizo lililo nje kabisa ya uwezo wao. Wizara iendelee na juhudi zake za ujenzi wa madarasa na vyoo vya kudumu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo ya Waziri wa Elimu na Utamduni, kuna upungufu wa madawati zaidi ya milioni moja hadi kufikia Desemba, 2003. Maana yake ni kwamba, kama kila dawati linakaliwa na wanafunzi wanne, basi zaidi ya wanafunzi milioni nne wanakaa chini kwenye vumbi, juu ya mawe, magogo au matofali. Kwa kweli tukubaliane kuwa hapo hakuna shule wala elimu. Kwa hiyo, tendo la kufundisha na kujifunza halikamiliki vizuri.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa madawati bado ni mkubwa sana. Kuna uwezekano kuwa hizo takwimu za Wizara zimeishaongezeka sana sasa hivi. Tatizo hili limeanza siku nyingi zilizopita. Tunaishauri Wizara iongeze kasi ya kutengeneza madawati kwa kushirikiana na wadau wakuu wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu za Wizara zinaonyesha kuwa sasa hivi kuna upungufu wa nyumba za Walimu zipatazo 98,063. Kamati ya Huduma za Jamii iliiagiza Wizara kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga nyumba za Walimu. Waziri amekiri kuwa kuna tatizo kubwa la upungufu na nyumba za Walimu. Je, Walimu wasio na nyumba wanaishi wapi? Je, usalama wao ukoje? Je, Serikali haioni kuwa pia hii ni sababu mojawapo ya upungufu wa Walimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri amesema kuwa nyumba 997 zimejengwa maeneo ya vijijini yaliyo na mazingira magumu. Tunamwomba Waziri atujulishe upungufu wa vyumba vijijini ni asilimia ngapi? Kwa ujumla, mazingira ya Walimu vijijini ni magumu sana. Kutokana na ugumu huo Walimu wengi wakipangiwa vijijini hawaendi. Hata wale wachache wanaoenda, hawakai muda mrefu kwa sababu wanaishi mahali duni. Walimu wa kike wanabakwa na wengine kulazimika kuolewa bila kupenda. Serikali iweke kipaumbele maeneo ya vijijini kwa sababu nyumba za kupanga hazipatikani kama maeneo ya mijini.

Ukiangalia takwimu kama zilivyotolewa na *Basic Education Statistics,* zinaonyesha kuwa watoto kutoka familia zinazoishi vijijini, maendeleo yao kimasomo yanakuwa mabaya kutokana na kugawanya muda wa shuleni na ule wa kufanya shughuli za kiuchumi, kitu kinachosababisha maendeleo ya wanafunzi hao wa vijijini kuingia Shule za Sekondari kuwa ni chini ya asilimia 15 kwa wastani wa Taifa. *(Makofi)*

Mlinganyo wa Ubora wa Elimu Vijijini ni wa hali ya chini kwa kulinganisha na shule nyingi za mijini. Hii inachangiwa na Walimu wengi kwenye shule za vijijini kutokupewa nafasi ya kujiendeleza. Hii yote pia inaendelea kuchangiwa na Wakaguzi wa Elimu kutokufika kutembelea shule hizo kutokana na hali halisi na mazingira ya usafiri kwenda na kurudi shuleni, jambo linalosababisha uandikwaji wa ripoti za uongo kuhusu Ukaguzi wa Elimu na shule hivyo kuendelea kudumaza kiwango cha elimu vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitakiwa kutoa fedha za kuendeshea shule *(Capitation Grant)*. Serikali ilitekeleza ahadi yake ya kutoa fedha hizo japo kwa kiasi fulani. Tunaipongeza na kuishukuru Serikali. Hata hivyo, Serikali isiishie kutoa fedha za kuendeshea shule bila kufuatilia matumizi ya fedha hizo kwani tayari kumekuwepo vitendo vya kuzila pesa hizo. Kuwepo na nidhamu katika matumizi ili fedha hizo zitumike kwa kazi na malengo yaliyokusudiwa na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna upungufu wa vitabu vya kiada, ziada na rejea kwa ngazi zote. Takwimu za Wizara zinaonyesha kuwa kitabu kimoja kinatumiwa na wanafunzi watano.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya Wananchi juu ya vitabu ni kuwa Viongozi wa Wizara ya Elimu na Utamaduni wamegeuza vitabu kuwa biashara inayowaletea manufaa. Kuna tetesi za rushwa ya vitabu pale Makao Makuu ambayo inaendelea kimya kimya. Kwa mfano, kitabu cha mchapishaji hakiruhusiwi kuingia shuleni bila kutoa chochote yaani asilimia kumi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikiendelea kubadilisha vitabu vya kiada bila sababu za msingi. Wachunguzi wa masuala ya elimu wanajiuliza maswali yafuatayo: Je, vitabu vinavyokuwepo vinaonekana havifai? Je, hakuna vitabu vingine vya kiada? Je, kuna mabadiliko ya mihtasari? Je, Siasa ya nchi imebadilishwa?

Kwa ujumla, jibu la maswali hayo ni hapana. Huo ni ushahidi tosha kuwa kuna manufaa ya kibinafsi katika suala la vitabu vya Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa agizo lake la kuhakikisha madai yote ya Walimu yanalipwa. Mtu wa kawaida anaweza kujiuliza kuwa ni kwa nini agizo hilo litoke sasa hivi na siyo kabla ya hapa? Licha ya maslahi duni, kero kubwa ya Walimu ilikuwa ni madeni makubwa ambayo wanaidai Serikali. Madeni hayo yamefikia shilingi bilioni 18.3 hadi kufikia Desemba, 2003. *(Makofi)*

Je, katika kero hii Walimu wangewezaje kuwaelimisha Watanzania kwa kiwango cha juu? Mfanyakazi anaweza kuwa anaenda kazini kama kawaida, lakini amegoma bila kutangaza. Serikali iwe makini na hali hii ili isije ikajirudia tena. Serikali isiwe inasubiri hadi Walimu wanakata tamaa na wengine mpaka wanakufa bila kutimiziwa haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, yapo malalamiko kwa baadhi ya Walimu dhidi ya mabadiliko ya mishahara kuanzia Julai, 2003. Baadhi ya Walimu waliathirika na zaidi ni wale waliokuwa kwenye *bar* (ukomo). Mfano Walimu waliokuwa *TGS.* 8 kwa mshahara wa Sh.154,600/= walitegemewa kupata Sh.188,000/=. Hivi sasa wanapata Sh.161,000/= kabla ya makato. Hili suala linapaswa kushughulikiwa na kurekebishwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma za Jamii iliitaka Serikali kuajiri Walimu wenye sifa za kufundisha katika ngazi mbalimbali kuanzia Shule za Chekechea hadi Vyuo vya Ualimu. Pia, Serikali ilitakiwa kufanya tathmini juu ya utaratibu wa kuandaa Walimu kwa muda mfupi. Serikali imesema zoezi la kutathmini utaratibu huo lipo. Serikali isichukue muda mrefu kutathmini na kutoa matokeo ili tusije kurudia makosa ya *UPE* ya 1974.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya usafiri kwa ujumla katika nchi yetu yanafahamika. Pia, usafiri wa daladala katika miji mingi hasa kwa wanafunzi una matatizo makubwa sana. Kutokana na umbali na matatizo ya usafiri, wanafunzi wengi huchelewa kufika shuleni hata kama walijitahidi kuamka mapema. Siyo hivyo tu, bali kuamka mapema (usiku) kuna athari zake kama kubakwa kwa wasichana au kushambuliwa na majambazi au wanyama wakali.

Mheshimiwa Spika, Serikali, wadau na shule zenyewe kwa juhudi zao, wabuni mbinu za kuwaondolea wanafunzi kero ya usafiri. Hii ni pamoja na kuwa na usafiri wa Shule, vinginevyo wanafunzi wanaathirika sana kitaaluma, kisaikolojia na kurubuniwa na wajanja wachache hasa wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM 2002 - 2006), unategemea kwa kiasi kikubwa kupata fedha kutoka kwa wahisani. Fedha hizi hazipatikani kwa wakati. Kwa hiyo, malengo ya MMEM hayafikiwi. Haijulikani tutaendelea kuwategemea wahisani katika mazingira kama haya hadi lini? Siyo hivyo tu, bali kadri ya Taarifa ya Wizara, Halmashauri nyingi huchelewa kuwasilisha Makao Makuu taarifa za utekelezaji na shughuli zilizopangwa. Je, ni hatua zipi za kinidhamu

zilizochukuliwa dhidi ya Halmashauri hizo? Kama hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi ya Halmashauri hizo, je, ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, Mpango huu wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi umekuwa na matatizo mengine kama ifuatavyo: Tatizo la kwanza ni rushwa. Wadau wengi wa Elimu wanajumuishwa katika kutoa na kupokea rushwa. Kwa mfano, Walimu, Wafanyakazi Maofisini (Maafisa Elimu), pamoja na wazazi wenyewe. Wazazi hulazimika kutoa rushwa kutokana na matatizo wanayoyapata. Kwa mfano, uandikishaji wa watoto wa chekechea na darasa la kwanza. Pia, usahihishaji mitihani unamfanya mtoto aendelee na masomo ya msingi hata kama uwezo wake ni mdogo, hiyo siyo haki.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pili linahusu matumizi ya fedha za shule. Fedha zinazotolewa kwa mpango wa MMEM hutumiwa vibaya hasa na baadhi ya Walimu Wakuu na Wakurugenzi wa Halmashauri. Matokeo yake ni kutotimia kwa malengo yaliyokusudiwa. Kwa mfano, madawati yanayotengenezwa hayakidhi idadi na uimara ukilinganisha na kiasi cha pesa kilichotolewa.

Mheshimiwa Spika, katika taratibu za kiusimamizi na uendeshaji shughuli za elimu katika ngazi ya Kata, Serikali iliwaondolea ujumbe Waratibu Elimu Kata katika Kamati za Shule na kuwafanya wahudhurie vikao vya Kamati kwa mialiko. Michango yao ya mawazo na usimamizi inakuwa haina uzito, kama ambavyo ilionekana ni muhimu Waheshimiwa Madiwani na wanafunzi wawili wawe Wajumbe ndani ya Kamati, basi hivyo hivyo ifanyike kwa Waratibu Elimu Kata.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine la kuvunja vipindi mara kwa mara kutokana na sababu zisizo na msingi. Kwa mfano, kuwafanyisha wanafunzi kazi za nje bila sababu kama biashara. Pia, ufundishaji wenyewe unakuwa sio wa kiualimu. Kwa mfano, Walimu kuchelewa kuingia darasani na kufundisha, kutotumia mbinu tofauti ambazo ni shirikishi zinazomfanya mtoto aelewe. Kwa ujumla, Walimu Wakuu wengi hawatekelezi vizuri wajibu wao kiasi kwamba matatizo hayo yanajitokeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma ya Jamii iliiagiza Wizara kuongeza kasi ya kufundisha Wakaguzi wa Shule. Katika utekelezaji wa agizo hilo, Wizara imekiri kuwa bado kuna upungufu wa wakaguzi 244 ili kufikia mahitaji ya wakaguzi wa shule 1,269. Kutokana na upungufu huo, kuna ufuatiliaji mdogo wa jinsi walimu wanavyofundisha madarasani. Kwa hiyo, ufundishaji unalenga kutimiza wajibu na malipo tu.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi unakabiliwa pia na tatizo la usafiri. Wizara ilikiri kwa Kamati ya Huduma za Jamii, kuwa mwaka 2003, idara ya ukaguzi wa shule ina magari 62 tu. Ofisi za Kanda zina magari 48 kati ya Wilaya 114. Magari 15 tu kati ya hayo ni mazima na yaliyobaki ni mabovu. Hizi ni mojawapo na baadhi tu ya athari finyu kwa Wizara nyeti kama hii.

Kitu ambacho kinatia mashaka ni kwamba, katika mpango wa MMEM, shule nyingi mno za msingi na madarasa zinajengwa lakini ili kupata matunda ya kazi hiyo wakufunzi ndiyo kitu cha kwanza, shule ni popote ila tu wakufunzi wawepo, tunaweza kuwekeza nguvu na uchumi wetu kwenye majengo na baadaye yote yakachakaa na kudondoka. Lakini kama sehemu ya juhudi hizo zingewekwa ili kuwapata wakufunzi tu nadhani hata kiwango cha elimu kingepanda zaidi.

Tatizo lingine inaonyesha kuwa kuna hatari ya kukifanya kizazi hiki kutokuwa na upeo wa juu wa elimu ya sekondari kwani, haionyeshi kuwa uwekezaji unaofanywa kwenye shule za msingi unashabihiana na shule za sekondari. Inaonekana lengo la Serikali ni kuwawezesha vijana wetu kujua kusoma na kuandika tu. Tunashauri lengo lao liwe ni wajisaidie na kusaidia Taifa kwa ujumla pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Masomo ya Maarifa ya Jamii na Stadi za kazi yalianzishwa mwaka 1996. Somo la Maarifa ya Jamii linaunganisha masomo ya Historia, Jiografia na Uraia. Somo la Stadi za Kazi pia linaunganisha vitu vingi. Kwa mfano, muziki, ususi, uchapaji, ufinyanzi, usukaji, kuigiza na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Somo la Maarifa ya Jamii limekuwa na matatizo mengi. Makala za Mwalimu Yusufu Halimoja katika vyombo vya habari zimeainisha matatizo hayo kwa undani. Kuchanganya masomo matatu kumesababisha wanafunzi kushindwa masomo yao. Si hivyo tu, bali siyo rahisi kumpata mwalimu anayeweza kufundisha masomo hayo kwa ufanisi. Kwa hiyo, mafundisho huwa nusu kwa nusu. Wizara iyarudishe masomo yote matatu ambayo ni Historia, Jiografia na Uraia, ili yawe yanajitegemea kama zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Somo la Stadi za Kazi ni zuri kwa sababu linawasaidia wanafunzi pindi wanaporudi nyumbani. Lakini, somo hilo lina vipengele vingi kwa mwaka mmoja, kwa mfano, mtoto wa darasa la saba anatakiwa asome uchoraji picha, upambaji, ufinyanzi, uchongaji, usukaji, ushonaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pili la somo la Stadi za Kazi ni vitendea kazi yaani vifaa vya kufundishia. Shule nyingi hazina vifaa hivyo. Zaidi ya hapo walimu wa Stadi za Kazi hawakuandaliwa. Kwa hiyo, tunashauri ama somo hilo lifutwe kabisa mashuleni au ziteuliwe shughuli chache kama tatu au nne kwa mwaka ambazo zitamwandaa mwanafunzi kwa maisha ya kujitegemea akimaliza elimu ya msingi. Kama uamuzi huo utachukuliwa, basi vyuo maalum vianzishwe kwa ajili ya kuwaandaa walimu watakaofundisha somo hilo. Kinyume na hapo, tutakuwa tunaishusha elimu kwa kudhamiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masomo ya ziada *(tuition),* Serikali ilitoa tamko la kupiga marufuku *tuition* mashuleni. Sina uhakika na ufuatiliaji wa tamko hili. Sasa hivi biashara hii imeshamiri shuleni na nyumbani. Wazazi wengi wanapata kero kubwa ya kutoa pesa ya *tuition.* Kuna imani miongoni mwa baadhi ya wazazi kuwa walimu wengi hawafundishi vizuri hadi wapate pesa za *tuition.*

Mheshimiwa Spika, walimu wamebuni mbinu ikiwa ni pamoja na kubadili jina la masomo hayo. Mojawapo ya majina mapya ni masomo rekebisho. Kuna mamlaka chache zinazojitahidi kufuatilia utekelezaji wa tamko hilo. Hata hivyo, ufuatiliaji unafanyika shuleni kwa wanafunzi, ujanja unaotumika ni kuwazuia wanafunzi wasimwambie mtu yeyote kama kuna masomo ya *tuition.* Kwa hiyo, kuna siri kubwa katika uendeshaji wa masomo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanafunzi na wazazi wasio na uwezo wa kulipia masomo haya, hawafanyi vizuri kwenye mitihani ya mazoezi na muhula hata ile ya mwisho. Siyo vizuri kutaja majina ya baadhi ya shule zinazofanya hivyo, lakini mfano mzuri ni shule za hapa Dodoma Manispaa. Tunaishauri Serikali, *REO* na *DEO* wabuni mbinu mpya za kuondoa kero hiyo. Baadhi ya mbinu hizo ni kuwauliza wazazi na Serikali kuwalipa maslahi mazuri walimu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna baadhi ya shule zinazowataka wanafunzi kuchanga kiasi fulani cha fedha kila wiki kwa ajili ya kufanya mitihani. Kama mwanafunzi hakutoa fedha hizo haruhusiwi kufanya mitihani hiyo. Tunaomba ufafanuzi wa tamko toka Serikalini kuhusu suala hili. Je, limehalalishwa kimyakimya au linafanyika kinyemela? Kama sio halali, je, ni hatua zipi zinachukuliwa ili kukomesha tatizo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kero katika Makao Makuu ya Wizara, kero mojawapo kubwa ya walimu, wakufunzi na wafanyakazi wengine wanaokwenda Makao Makuu ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa shida mbalimbali za kikazi ni huduma mbovu. Baadhi ya Wafanyakazi wa Makao Makuu ya Wizara, hawatoi huduma nzuri, wateja kwao ni kero. Wana kiburi, wana lugha chafu, hawajali wateja, wanapoteza mafaili ya walimu na wakufunzi na wamekuwa miungu watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali iwapeleke wafanyakazi hao wakasome kozi inayoitwa *Customer Care* ndipo watajua nini maana ya kumhudumia mteja. Kitu kikubwa cha kushangaza ni kupotea kwa mafaili ya walimu na wakufunzi katika mazingira ya kutatanisha. Je, mafaili yanapoteaje? Je, mafaili yanapotea au ni mbinu za kutafuta rushwa? Kama inawezekana, watumishi waliopo Makao Makuu ambao wanatoa huduma isiyoridhisha waondolewe kisha waletwe wengine wenye utu ambao watakaa ofisini muda wote wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili ni ushahidi kuwa kushuka kwa elimu nchini kunasababishwa na sisi wenyewe. Tunaivuruga elimu kwa kutowajali wadau wake, hasa walimu. Serikali isizibe masikio kuhusu kero hizi kama haitaki kuendelea kushuka kwa elimu siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo ya *Tanzania Elimu Supplies (TES),* matamshi ya Waziri Mkuu ya 23/6/2004 na majibu ya maandishi yaliyotolewa na Waziri wa Fedha tarehe 22 Juni, 2004 juu ya *TES,* yanapingana na ukweli uliomo katika *TES,* hii ni kwa sababu ripoti aliyokabidhiwa Waziri Mkuu na Mkurugenzi wa *TES* yenye Kumbukumbu Na. *TES/WEU/O3/MGR/33* ya tarehe 5 Septemba, 2003 inaonyesha wazi tofauti ya kauli

hizo. Ndani ya ripoti hii, uongozi ulijenga hoja kwa nini wanadai mkono wa kwa heri pamoja na kiinua mgongo *(Severance Allowance).* Ripoti inachanganua madeni ya shirika, wadai na wadaiwa. Madeni ya shirika ni Sh. 531,877,837 na wao wanadai Sh. 222 milioni.

Mheshimiwa Spika, Maelezo ya *Prime Minister* na Waziri wa Fedha kwa Bunge lako Tukufu sio ya kweli. Katika uuzaji huu wa Mali ya *TES,* hujuma iliyojitokeza katika kuuza Kiwanda cha *TES Pugu Road* kimeuzwa kwa hasara. Mkataba wa siri kati ya *TES* na *Scandinavia* ulikuwa batili kwa sababu wakati Mkataba unasainiwa mali zote za *TES* zilikuwa chini ya *PSRC.* Hivyo, ni *PSRC* pekee iliyokuwa na Mamlaka ya kuuza Mali za *TES* pekee na si vinginevyo. Kambi ya Upinzani, inataka uchunguzi ufanywe kuangalia uhalali wa *Scandnavia* kukataa kulipa bei waliyo-*tender* ya Sh.11 bilioni na wao kukubali kulipa Sh.276,000,000 kwa madai ya kutumia Sh.600,000,000 kufanya ukarabati wa kiwanda.

Wafanyakazi wa *TES* wanaomba mkono wa kwa heri, kwa sababu wenzao wa *TANESCO, TRC, NASACO, DAWASA* na kadhalika, wamelipwa licha ya mashirika hayo kuendeshwa kwa ruzuku ya Serikali, *TRC* wamelipwa kiinua mgongo, ndani ya *TES,* Watumishi wanane wamelipwa kiinua mgongo. Kwa nini kuna *Double Standards* katika shirika hilo hilo?

Mheshimiwa Spika, licha ya malalamiko na matatizo hayo, Kambi ya Upinzani, inaona kuna hujuma zilizojitokeza katika zoezi la kufilisi Shirika la Vifaa vya Elimu Tanzania. Tunaiomba Serikali itueleze kama wafanyakazi walishirikishwa katika zoezi zima kama sheria inavyotamka. Je, mali za shirika zilithaminiwa kabla ya kuuzwa ili kupata thamani ya mali halisi?

Je, hapakuwepo na unyanyasaji wa wafanyakazi hao katika zoezi hilo? Je, agizo la Waziri Mkuu la tarehe 23 Desemba, 2003 kwamba wafanyakazi hawa walipwe michango ya *PPF* limetekelezwa?

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa matatizo haya ya Wafanyakazi wa *TES* na kwingineko na kujua ni watu gani walio nyuma ya hayo matatizo. Kambi ya Upinzani inataka kuundwa kwa Tume Huru ya Bunge, kufanya uchunguzi kwenye hili tatizo ambalo linaleta hasara kwa Serikali na kuzitesa familia za wahusika na vile vile itoe majibu ya kweli juu ya mustakabali wa Shirika la *TES.* Aidha, Kambi ya Upinzani inaunga mkono kauli ya Mheshimiwa Ibrahimu Marwa ya kuleta hoja binafsi ili Tume huru ya Wabunge, iundwe kuchunguza mgogoro wa *TES* na Serikali ili kubaini ukweli uko wapi na haki itendeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haielewi agenda ya siri iliyopo katika matatizo ya *TES.* Kwa nini wafanyakazi wananyimwa haki zao? Je, Serikali imefikia hatua ya kuanza kuwadhulumu wananchi wake? Kama Serikali imeamua hivyo, basi itamke wazi. Kambi ya Upinzani inaunga mkono mchango wa Mheshimiwa Dr. William Shija, ya kuitaka Serikali itoe majibu ya kweli juu ya mustakabali wa Shirika la *TES.* Pia

tunaunga mkono nia ya Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, ya kuleta hoja binafsi Bungeni ya kuunda Tume Huru ya Wabunge kuchunguza mgogoro wa *TES* na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ualimu kama *profession* una maadili yake. Ni mategemeo ya wadau wa elimu kuwa lazima maadili yazingatiwe ili kulinda taaluma hiyo. Kuna malalamiko miongoni mwa wananchi kuwa baadhi ya walimu hawazingatii maadili hayo. Kwa mfano, kuna baadhi ya walimu ambao wana upendeleo kwa wanafunzi. Kwa hiyo, hata kama mwanafunzi hana uwezo wa kimasomo darasani, mwalimu anafanya kila linalowezekana kuhakikisha mtoto huyo anafaulu mitihani.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine la kukiukwa kwa maadili ya ualimu ni chuki binafsi baina ya baadhi ya walimu na wanafunzi. Mwalimu anakuwa na chuki binafsi na mwanafunzi fulani kwa sababu anazozifahamu yeye. Matokeo yake ni kumfanyia mwanafunzi kila aina ya vitimbi hadi anakosa raha shuleni na hatimaye kufanya vibaya kwenye masomo yake. Wananchi hubakia kuhoji kama kweli mwalimu huyu amesomea taaluma hiyo au la?

Mheshimiwa Spika, suala la maadili ya ualimu ni pamoja na chuki binafsi kutokea mara nyingi zaidi kwa wanafunzi wa kike kuliko wa kiume. Kwa mfano, inatokea mwanafunzi wa kike anaugua ghafla darasani kutokana na maumbile, mtoto analazimika kuomba ruhusa lakini anakemewa kwa maneno ya kashfa yasiyo ya kiungwana. Pia kuna tabia nyingine imezuka miongoni mwa baadhi ya walimu ya kuwataka wanafunzi kutoa nguo za ndani wakati wanachapwa viboko. Mwalimu huhisi kwamba mwanafunzi kaweka vitu fulani ili kuzuia ukali wa viboko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mambo hayo hufanywa na walimu au shule chache lakini wanaleta sifa mbaya kwa Wizara hii kwa sababu samaki mmoja akioza, wote wameoza. Matatizo haya sio rahisi na wala hayataki majibu rahisi kama mtu anavyoweza kufikiria au kusema, siyo masuala ya mtu kuamka na kusema leta ushahidi. Siyo masuala ya kutaka maelezo kama watu hao wameripotiwa kwa Wakuu wa Shule, *PEO* au *DEO*. Haya ni masuala ya kisaikolojia ambayo yanataka kufanyiwa kazi kisaikolojia na Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, Wizara ya Elimu na Utamaduni ijiulize swali moja kama ifuatavyo: Je, watu wanasema mimi nikoje? Maelezo ya hotuba yetu yanaonyesha jinsi Wizara inavyoonekana machoni mwa wananchi. Wizara inashauriwa iwe mtumishi wa watu hasa wadau wake. Wizara imwone mdau wake ambaye pia ni mteja kama mfalme.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa tunaanza mjadala wa jumla, nilikosea kumtaja Mheshimiwa Maria Watondoha kwamba hajachangia, kwa kweli rekodi inaonyesha kwamba alishachangia

mara moja Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa hiyo, nitamhamishia kwenye kundi la waliokwisha changia mara moja.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya mwanzo ya kuchangia hoja ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, ambayo kwa kweli kama ulivyotangulia kudokeza, ina mengi sana mazuri ambayo haijapata kutokea, lakini kwa kweli yatatokea kwa sababu Serikali imedhamiria.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa sababu sijawahi kuzungumza humu ndani ya Bunge katika kipindi hiki, kama ilivyo ada napenda nitoe pole kwa Wabunge wote, waliopata matatizo mbalimbali yakiwemo matatizo ya ajali, matatizo ya misiba. Waliopata misiba ambao ni Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan na Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, kwa kufiwa na wapendwa wao. Ninaomba Mungu, azilaze mahali pema peponi roho za marehemu wapendwa wote. *Amen.*

Pia napenda kuwapa pole wale waliopata ajali ambao ni Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, ambaye bado yuko hospitali na Mungu amsaidie aweze kupona haraka.

Mheshimiwa Spika, nisisahau kutoa rambirambi kwa familia na Wananchi wa Mbeya Vijijini kwa kifo cha ghafla cha mwenzetu ambaye ametuacha kama utani Mheshimiwa Yete Mwalyego, naye namwombea Mungu amlaze mahali pema peponi na subira kwa wote ambao wamehusika kwa sababu kwa kweli ni tatizo la Mungu na akiamua basi amekwishaamua.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wamepata nafasi mbalimbali za kuchaguliwa Kimataifa na Kitaifa, Wabunge wa Bunge la Afrika, akiwemo Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, ambaye kwa kweli ameleta sifa na heshima katika nchi yetu kwa kuwa Rais wa Kwanza katika Bunge la Afrika. Tuombe tu kuwa naye pamoja ili angalau heshima hiyo iweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo ya kupongeza ni mengi lakini sasa niingie kwenye mada yenyewe. Napenda kuwapongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu Waziri, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Katibu Mkuu, Mama Malale, Wakurugenzi na Watendaji wa Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa kuandaa hotuba nzuri yenye maelezo ya kina na yenye takwimu nyingi tu za kueleweka kwa kweli ambazo zimetusaidia kuelewa mengi yaliyomo tangu shule na kila kitu kinajieleza katika hali ya takwimu. Nadhani wenzetu hawa kwa sababu wengi ni walimu, wamebobea katika kufupisha mambo kwa kutumia njia za sayansi na teknolojia ya kisasa kuliko kutumia maandishi mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, napenda kuchangia maeneo machache tu kwa sababu mengi niliyoyasoma na kuyaelewa kwa muda mfupi, kwa kiasi kikubwa kwa mwaka huu, Wizara imetoa matumaini ya mambo mengi sana kuwa yatakuwa

mazuri na tuombe kwa kweli yawe mazuri. Kwa hiyo, ni machache kwa sababu hatuwezi kukosa cha kuweza kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianzia na uandikishaji wa watoto shule, hasa shule za msingi, kweli kazi ni nzuri sana. Lakini napenda kueleza kwamba, uandikishaji kwa watoto wenye ulemavu nchini mpaka sasa hivi ni mdogo. Hii inatokana na sababu ambazo ziko nyingi tu, mojawapo ni kwamba, katika utafiti wangu mdogo, wakuu wa shule za msingi kadhaa, huwa wanakataa kuandikisha watoto hawa kujiunga na shule. Lakini mimi naona hili wala siyo kosa lao kwa sababu katika shule zetu nyingi bado mazingira ya kujifunzia na kufundishia watoto hawa wenye ulemavu siyo mazuri. Kwa hiyo, mwalimu atampokea mtoto halafu afanye nini, amuweke wapi, amfundishe nani?

Kwa hiyo, siyo kosa lao lakini ndiyo hali halisi hiyo. Tatizo lingine ambalo nimejifunza ni kwamba, bado katika nchi yetu kuna baadhi ya wazazi na walezi wa watoto hawa ambao wanaendelea na tabia ya kuficha watoto hawa wasiende shuleni kusoma kwa msingi huo hawawezi kupata elimu. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa ni kwamba, elimu kwa wote, hii MMEM ambayo imeanza miaka kadhaa katika nchi yetu ikisisitizwa hata na Umoja wa Mataifa na sisi wenyewe tukifanya kazi ya kutosha bado haijawafikia watoto wenye ulemavu, haijawa na manufaa kwa watoto wenye ulemavu, walio wengi katika nchi yetu kuanzia *level* ya *primary. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naipongeza Serikali kwa sababu baada ya kusoma hotuba hii, nimeona kwamba, itatoa ruzuku kwa ujenzi wa shule zitakazojengwa na taasisi au watu binafsi watakaohudumia watoto hawa wenye ulemavu. Hii nadhani ni njia mojawapo ya kuweza ku-*encourage* jamii hii ya watoto waweze nao kupata elimu ya kutosha. Pia nimejaribu kuona kwamba Serikali itatoa ruzuku kwa kununua vifaa vya kujifunzia na kufundishia na *braill machines* na kadhalika kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 40. Lakini hapo ningeshauri kwamba, pia Serikali isisahau kununua vifaa vya michezo midogo midogo ambayo hii inakuwa ni mbinu mojawapo ya kuwaelimisha watoto wale wenye ulemavu wa akili, wanaanza na hivyo vidogo vidogo halafu baadaye wanapanua zaidi.

Kwa hiyo, pamoja na aliyoeleza kwamba kutakuwa na *braill machines,* kutakuwa na vifaa vya kusikilizia, kwa kweli napenda kushukuru sana kwa sababu hili limekuwa ni tatizo, hili limekuwa ni kikwazo, hiki kimekuwa ni kilio cha muda mrefu. Pamoja na vifaa hivi ninapenda tena kushauri na kusisitiza kwamba, basi majengo yaliyoahidiwa kurekebishwa hapa katika shule zetu mbalimbali, yaweze kurekebishwa kwa sababu napo *accessibility* ya aina moja au nyingine ni kikwazo cha kupata elimu watoto wenye ulemavu hasa wale wenye ulemavu wa viungo na wasioona.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya elimu nzuri yoyote ile yanaendana na maandalizi mazuri ya walimu. Serikali inafanya jitihada sana kuwaandaa walimu. Lakini hapa napenda kutoa masikitiko kwamba, idadi ya walimu wanaoandaliwa kuweza kumudu watoto wenye ulemavu ni ndogo sana. Mwaka 2003/2004, waliandaliwa watu 164 tu na ninaamini watoto wenye ulemavu wako wengi pamoja na kwamba wengine hawajaandikishwa. Kwa hiyo, ninashauri kwamba, katika hili idadi ya walimu hawa

iongezwe ili kukidhi haja ya MMEM na MMES ambayo tumeamua kuitekeleza kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Kama inakuwa tatizo nilishashauri huko nyuma hivi kuna shida gani kama somo la elimu maalum, walimu wote wa ngazi zote wakifundishwa? Ili mtu anapomaliza kusomea huo ualimu anakuwa na dozi ya kumudu, watoto kama hawa kwa sababu nchi sasa hivi imeanza na suala la *inclusive education,* pamoja na kwamba kila shule sijui imetengewa pawe na kichumba fulani cha kufundishia hao, lakini je, ukikumbana naye darasani katika ujumla wake wewe ufanyaje?

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri ili kurahisisha hata gharama ya mafunzo na kadhalika, kuna tatizo gani kwa kila mwalimu akipata dozi ya *special education?* Hiyo, itasaidia halafu wengine basi wakaendelee huko ku-*specialize* iwe kama udaktari kwamba unapata ile *general dose* halafu unakwenda ku-*specialize* kwa kitu chako unachokifikiria, kwa nini tusifanye hilo kwa upande wa walimu hasa kwa elimu maalum? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendeleza mpango wa Elimu ya Watu Wazima hasa sasa hivi kwa kupitia MKEJA na MEMKWA ndiko tunakoelekea kwamba ni elimu kwa wale walioikosa, wazee au vijana. Kidogo hapo ningeshauri kwamba, katika hili kwa sababu nilikuwa kwenye ziara watu walizungumza hilo kwamba, Elimu ya Watu Wazima siku hizi haina hiki, haina hiki, nashauri ingefaa stadi zile za kazi, elimu, afya, mazingira na kadhalika, visisitizwe ili hawa wanapoondoka waondoke na taaluma hizo, waondoke na stadi hizo. Kwanza, wamechelewa kuzipata, sasa tusipowapa hata katika hii *stage* inakuwa bado tunakuwa na wananchi ambao kwa kweli hawajaelimika kwa sababu elimu siyo kusoma na kuandika tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa viongozi na watendaji wa taasisi na asasi mbalimbali zilizoko chini ya Wizara hii kwa kufanya kazi kwa bidii pamoja na matatizo ya kibajeti. Kwa mfano, Baraza la Mitihani la Taifa kwa kiasi kikubwa wameweza kudhibiti uvujaji wa mitihani. Lakini bado kuna tatizo la kucheleweshwa kupatikana kwa vyeti vya mwisho vya wahitimu. Mtu anakaa mwaka mzima hana cheti cha kuhitimu, anaweza akabahatisha kupata kibarua akakosa kwa sababu sehemu zingine hawataki zile *results slip* wanataka cheti chenyewe, sasa huna cheti, mtu utafanyaje? Unaweza ukakosa kibarua kwa ajili hiyo, kwa hiyo, ningeomba hilo liweze kushughulikiwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na hoja zilizotolewa na Kamati yangu ya Huduma za Jamii, kuhusu suala la madai na kero za walimu hasa kuhusu malimbikizo ya fedha za aina mbalimbali, kama ukurasa wa tatu na wa nne wa taarifa hiyo ulivyosema. Hata hivyo, nina wasiwasi pamoja na Agizo la Waziri Mkuu kwamba, zoezi hili la kulipa malimbikizo litatekelezeka kama alivyotoa tamko Mheshimiwa Waziri Mkuu na sisi kuliunga mkono kwa sababu wakati TAMISEMI imeshaunda timu ya kuhakiki malimbikizo hayo, kwamba ni dalili nzuri ya kulipwa walimu malimbikizo hayo wakati ambao Waziri Mkuu amesema nadhani Waziri wa Elimu ya Utamaduni, bado

hajaunda timu hiyo. Sasa je, walimu wale walioko chini yake nani anawahakikia hayo madeni?

Mheshimiwa Spika, ningeomba uhakiki huo hapo ushirikishe Chama cha Walimu kama TAMISEMI ilivyosema, kusudi kwa kweli zoezi hili liweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya utumishi ndani ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, mimi ni mwalimu wa miaka mingi tu, lakini ningetegemea sana kwa sasa hivi Wizara yetu, Watendaji wetu wa Wizara, waweze kuharakisha kidogo katika kutatua matatizo ya Watendaji wao wakiwemo walimu. Kumekuwa na mtindo wa muda mrefu kwamba, ukienda pale unaweza huyu umwone na mara uambiwe faili lilipotea, likaenda, mpaka mtu mwenye tatizo unapata matatizo kidogo kwamba sasa nifanyeje mbona inakuwa hivi. Lakini ninashauri ule mkataba wa huduma ya wateja, basi uanze kufanya kazi vizuri ndani ya Wizara yetu kusudi tuweze kuondoa manung'uniko mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, naomba kusisitiza utiliwe mkazo sana katika awamu hii ya pili ya MMES na MMEM kuhusu ujenzi wa nyumba za walimu. Awamu ya kwanza ilikuwa ni madarasa tu ndiyo walikuwa wanahangaika, nyumba moja, mbili, walimu wana matatizo ya nyumba za kuishi. Mwalimu usipoishi karibu na nyumba kwa kweli ufundishaji na maandalizi unakuwa mgumu, unaishia kulipua, unalaumiwa umefelisha kumbe mazingira ya utendaji kazi ni magumu. Kwa hiyo, naomba kabisa msisitizo wa nyumba za walimu kwa awamu hii sasa uwe kama wananchi watakavyosisitiza kujenga shule au maabara, kinyume cha hapo kwa kweli mipango itakuwa mizuri, hela tutazitoa lakini *out come results* ya mwisho inaweza ikawa siyo tunayoitegemea katika sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa kweli napenda kufurahi kwamba bajeti hii ina matumaini mengi sana. La msingi ni kwamba tuliyoyasema yaendane na vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Kabla sijagusia mambo yote yanayohusu hotuba hii, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa jamii, familia, rafiki, ndugu na wananchi wa Mbeya Vijijini, kwa kumpoteza Mbunge wao, Mheshimiwa Yete Mwalyego.

Mheshimiwa Spika, pia nachukua nafasi hii, kumpongeza rafiki yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurudi tena Bungeni. Amerudi na nguvu ya CCM, kwa hiyo, tunamshukuru kuwa na sisi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ni nzuri na imeangaza mambo mengi na tumeona picha ni nzuri, lakini kama hotuba hii ingekuwa ndiyo picha halisi Vijijini na Wilayani,

basi Taifa letu lingepeta kwa suala la elimu. Mimi nadiriki kusema kuwa, elimu katika maeneo fulani bado iko katika hali mbaya sana. Kuna matatizo ya msingi katika elimu. Lakini matatizo hayo hayashughulikiwi. Hapa katika kitabu hiki ambacho tumekipata sasa hivi cha *Education Projects and Programs* katika ukurasa wa 38 kinasema: *"Primary Education Development Plan (PEDP),* mwaka 2002 mpaka 2006, *to ensure that all chidren have equitable access to good quality primary education to enrol all children aged 7 to 10 to improve education quality".* Kuhusu sekondari, ukurasa wa 69 kitabu hiki kinasema: *"Secondary Education Development Plan (SEDP), to enrol more children in secondary schools retained and ensure that they learn properly". (Makofi)*

Mwaka 2000 ilitakiwa kuwa walioingia katika Sekondari ni asilimia 21 na itakapofika mwaka 2010 itakuwa asilimia 50. Sasa hapa najiuliza, ubora wa elimu unaweza kupatikanaje kwenye mashule ya Vijijini kwa mfano katika Shule za Wilaya yangu kuna Shule ya Ndago Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne, Walimu ni watatu tu kwa miaka yote. Nimejaribu kufuatilia hili suala, nimefika mpaka Wizarani. Walimu ambao walipangwa kwenda kule hawakwenda na wanaendelea na leo wanapofanya mtihani hakuna anayefaulu. Huo ndio ubora wa elimu kama sio kuwadhulumu watu wa Iramba mnafanya nini hapo? *(Kicheko/Makofi)*

Kuna Shule ya Sekondari ya Tumaini ya Kinampanda. Shule hii ya mchanganyiko wa wavulana na wasichana, kwa miaka kumi haina Mwalimu wa *Domestic Science.* Wasichana wanapofanya mitihani kutoka kwenye Shule ile hawawezi kupasi kwa sababu hawajafundishwa kwa miaka kumi. Shule ile ile pia haina hata Mwalimu wa kufundisha mahesabu. Sasa huu ubora tutaupata wapi katika mashule? Ubora maana yake labda Mheshimiwa Waziri anaongelea ubora kwa Shule zile ambazo zinapendelewa. Hali hii nina uhakika ipo katika Wilaya nyingi.

Mimi ningeshauri, wakati wa Bajeti ndio kutafuta ufumbuzi wa matatizo makubwa kama haya. Sasa kama suala la ualimu halijatatuliwa; kwa nini mashule mengi hayana walimu na wakipangwa hawaendi? Kwa nini Wizara isifanye utafiti wa kutosha na hii Shule inaendelea kuwa ya Serikali na imesajiliwa, wanafunzi wanapofanya mitihani hawawezi kupasi kwa sababu hawajafundishwa? Sasa hakuna la ubora.

Ninavyoona hapa tunachokifanya ni kuwa *education broke without development.* Mashule mengi Vijijini hasa katika Wilaya yangu iwe mashule ya msingi au ya sekondari, ni mahali pa kukusanyika kucheza kwa sababu kama kuna Walimu wawili tu au watatu, watafundisha masomo yote hayo?! Kwa hiyo, suala hili sio kulitazama kwamba kwa kuwa sio katika maeneo ambayo yanapendelewa mengine yanaachwa hivyo hivyo, matatizo yako pale pale. Sasa ninaloomba sitaki maelezo. Naomba Mheshimiwa Waziri aweke kwenye Bajeti yafuatayo kuhusu mashule yale ambayo yako kwenye wilaya yangu ambayo yana matatizo. Mwaka huu sijui hata kufaulu kwenyewe, wanafunzi watatu tu ndio wameingia Sekondari. Katika wale wanafunzi ambao wamekwenda Kidato cha Tano sidhani kama wako zaidi ya watatu. Sasa hiyo inakuwa kama kubagua, kwa nini maeneo mengine yabaguliwe na mengine yapete? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningeomba fedha zitengwe katika Bajeti hii. Labda ningefika mwezi uliopita Mheshimiwa Waziri angeniambia Bajeti imekwisha, hatuna fedha. Sasa tunapitisha Bajeti, naomba mashule ya Ndago, Kinampanda, Kizaga, Lulumba yapangiwe fedha za kutosha kusudi wapate walimu wanaotakiwa kuwepo pale, tena Walimu wenye sifa, sio wa kuokoteza ambao hawana kazi waende kufundisha kwa sababu wanajua kusoma na kuandika tu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pili, ningeomba tutazame ubora wa elimu katika mazingira ya utandawazi. Miaka ya nyuma tulikuwa tunajitahidi na *standards* zetu au vigezo vyetu vya ubora vilikuwa vya Kitaifa. Leo ambapo ulimwengu huu umekuwa kama Kijiji kimoja, tunawatayarisha vijana wetu ambao wataweza kuhimili ushindani Kimataifa na Kitaifa. Vijana wetu watakapomaliza elimu ya msingi au Sekondari, ndio wao watakuwa wakulima wetu, wafanyabiashara wetu, ni wale ambao watashindana na wenzao kutoka mahali pengine duniani katika soko la ajira, soko la biashara, soko la utamaduni na soko la michezo.

Sasa tunapokuwa na wananchi ambao hawawezi kujieleza na kueleweka, watakwendaje wakaingia kwa mfano Nigeria wakafanye biashara au wakatafute ajira? Leo ukifika Kariakoo kuna Wachina wanauza madawa pale, wamekuja. Lakini kwa nini sisi wananchi wetu ambao kwa miaka ijayo wasiende Beijing nao wawe na vibanda vyao vya biashara? Lakini kwa sababu hawana lugha ya kujieleza, sasa ninachotaka kusema ni kwamba lazima Taifa hili lijue kuwa suala la kuwa na lugha ya Kimataifa ya kujieleza litiliwe maanani. Mimi sioni ubaya wowote kama sisi tukianza kufundisha lugha ambazo tunajua kuwa tunaweza kuwatayarisha wananchi wetu waweze kushindana. *(Makofi)*

Kwa mfano Kiingereza, Kifaransa, Kichina, soko kubwa duniani hapa, hata Mwamerika na Mataifa mengine yameona yamefanya kosa kutokufundisha vijana wao au watu wao lugha ya Kichina. Ningeomba Serikali itazame uwezekano wa kuamua kuwa lugha ya kichina iwe mojawapo ambapo wanafunzi wanaweza kufundishwa Sekondari kusudi wanapomaliza, watakapokuwa wafanyabiashara itakuwa vizuri kwenda kufanya biashara yake na China bila kutafuta mkalimani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kumalizia kwa kusema kuwa, suala la ubora wa elimu uendane na matayarisho kwa wananchi wetu kusudi watakapopambana wakati inapofika kuwa wako katika hali ya kujenga Taifa au kujenga uhusiano, wakati sisi tulipokuwa tunamalizia shule na kuingia kwenye ajira za Kimataifa ilikuwa inatosha kuwa na lugha nzuri moja wanayozungumza ya Kimataifa na sifa zako ambazo umesomea. Lakini leo lazima uwe *Computer Literate.* Pasipokuwa na *Computer Literate* hutakwenda popote. Mambo ya kuandika hotuba ndefu kama hizi tunazosoma zimepitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba pia Walimu ambao sasa ni chombo muhimu katika elimu, paanzishwe motisha maalum katika kujaribu kuwavutia waende kwenye vituo vya kazi ambavyo vina mazingira magumu. Hili nimezungumza mara kwa mara lakini hatutaweza kuwa na walimu wa kutosha kama hatutakuwa na *Special Incentives Scheme.* Hapa tunacheza na binadamu. Elimu ni haki ya mwananchi, ni haki ya msingi,

ni haki ya Kikatiba. Kwa hiyo, lifanywe kila liwezekanalo suala hili la upungufu wa Walimu ikiwezekana limalizwe na inawezekana. *Is a question of arranging priorities.* Ningeomba suala hili lifikiriwe na ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu anipatie ufumbuzi kuhusu matatizo ya Shule ya Sekondari nilizozitaja katika Wilaya yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hotuba hii lakini sitataka maelezo ya maneno, nataka maelezo ya matendo. Kwa hiyo, naomba nipate ufumbuzi na sisi huko Iramba hatuwezi kuendelea kubaguliwa watoto wasifaulu kwa sababu hawafundishwi kwa kuwa hawana Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache ningeomba kuishia hapa, lakini nimeongea kwa uchungu sana kwa sababu kuna ubaguzi unaendelea polepole sio kwa maandishi lakini kwa vitendo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri ya Bajeti ya kipindi hiki. Awali ya yote nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mungai, Naibu Waziri Sakila, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri na kwa jinsi walivyopanga taarifa yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge hili mimi ni mara yangu ya kwanza. Nilipoanza nilikuwa kwenye Kamati ya Huduma za Jamii, nilikuwa napata mashaka kuhusu Mheshimiwa Mungai na nilikuwa simwelewi. Lakini kwa jinsi nilivyokaa naye mpaka sasa hivi, nimegundua kuwa yuko mahiri sana, anafanya kazi kwa makini na anatekeleza Sera za CCM kwa uhodari bila ya matatizo. Kwa hiyo, naendelea kumpongeza na kumtakia kila la kheri na Watendaji wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kutoa pole kwa wale wenzetu ambao wamepata matatizo ya kufiwa kama Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Asha Kigoda. Pia natoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, mwenzetu ambaye alikuwa anatoa mchango mzuri sana kwenye Kamati ya Miundombinu. Vile vile natoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Gama, kwa kufiwa na mwanawe. Mwenyezi Mungu aweke roho zao mahali pema Peponi. *Amina.* Wakati huo huo niwape pole wote waliopata ajali na kwamba Mungu awasaidie waendelee na afya nzuri.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Mtwara katika Elimu ya Msingi tumekuwa wa pili kwa kipindi hiki. Kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Shirima, kwa kazi yake nzuri na Afisa Elimu Mkoa, Ndugu Isaya, pamoja na Watendaji wote, Maafisa Elimu Wilaya wa Mkoa ule na Kamati za Elimu ambazo zilikuwa zinasimamia utendaji wa kazi kwenye Shule za Msingi kwa jitihada zao na ninazidi kuwatia moyo kwamba waendelee kwa sababu nchi hii hasa katika Mkoa wa Mtwara hatutaweza kupata maendeleo kama sisi wenyewe hatukusimama katika kushikamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliomba kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu, bahati mbaya sikupata nafasi. Kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mtwara, wamenituma kwamba nimwambie katika ziara yake aliyoifanya alivyotembelea Mkoa ule alipata tatizo la maji. Kwa hiyo, wamenituma nimwambie kwamba bado hali sio nzuri, wanahitaji kupata huduma za maji. Alipotembelea kila Wilaya aliona mwenyewe misururu ya wananchi wanaotafuta maji na walivyoongea na Vikao vya Wazee na akaahidi atamtuma Waziri wa Maji. Ni kweli na ninamshukuru Waziri wa Maji alikwenda. Lakini bado tatizo lipo. Sasa hicho ni kilio cha wanawake wa Mkoa wa Mtwara, mimi nawasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa nataka niipongeze Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi inavyotekeleza sera ya nchi hii na kwa jinsi walivyoamua kujidhatiti kwenye suala la elimu. Elimu ni jambo nyeti na kama hatutasimamia suala la elimu ni wazi Idara zote zinaweza zikawa haziendi kwa sababu watu wake watakuwa wa mashaka mashaka kuhusu elimu. Sasa kwa jinsi wanavyojidhatiti, mimi nazidi kuwasogeza na kwamba leo taarifa aliyoisoma Waziri imenifurahisha sana kuona vipengele ambavyo vilikuwa ni kero Vijijini na vingi Serikali imeanza kuvitoa. Kwa mfano katika Taarifa yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba walimu watapewa mafao haraka iwezekanavyo. Mimi nasisitiza kwamba ni kweli kabisa umefika wakati hizo kero ziondolewe kwa haraka iwezekanavyo kwa sababu walimu hawa wanasikia hata kama hawana redio wanasikia kupitia pengine kwa majirani kwamba Serikali sasa hivi inataka kuwalipa masurufu yao. Kwa hiyo, walipwe kwa wakati na pia suala la kupunguza ada kwa Shule za Sekondari Sh. 20,000/= badala ya Sh. 40,000/=, kweli ni katika pongezi ambazo naendelea nazo. Ninayo mifano ya wazazi ambao kweli walikuwa wanashindwa kulipa hizo Sh.40,000/=, kwa hiyo leo nina hakika kama wamekuwa wanasikiliza hotuba ya Waziri, wamefurahia na wanazidi kuipenda Serikali yao na hivi ndivyo inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Walimu wanajituma sana. Wakati wa likizo za Shule za Msingi wanakosa muda wa kupumzika hasa kwa Darasa la Nne na la Saba. Inabidi wawasaidie vizuri kusudi watakapofanya mitihani waende na wakati. Lakini bado sisi kama walezi wa Walimu hatujasimamia kwa dhati kuona hawa Walimu wanaishi katika mazingira gani. Mazingira wanayoishi hawa Walimu ni magumu, kama alivyoanza mwenzangu kuzumgumza huko nyuma, wengine hawana nyumba. Nataka nimthibitishie Waziri kwamba Walimu wa P*rimary School* wa Mkoa wa Mtwara wanasafiri maili 25, sio Kilometa, maili 25 mpaka 30 kutoka kwenye Vijiji kuja Makao Makuu ya Wilaya. Wanasafiri kwa mazingira magumu, wanasafiri kwa baiskeli, wengine wanathubutu kutembea kwa miguu maana Vijiji vyao viko kwenye milima. Serikali inawasaidiaje hawa na hawa ndio wanaoiweka elimu iwepo? Leo tusingeweza kuipongeza MMEM hapa kama sio Walimu wa Shule ya Msingi kusimamia pamoja na Kamati zao. Lakini tuone tunawasaidiaje, tuwaboreshee maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara, historia imejiandika huko nyuma. Baada ya uhuru Walimu na watumishi kwa ujumla walikuwa hawapendi kwenda Mkoa wa Mtwara, lakini leo wapo Walimu Wachaga, Wagogo, Wanyiramba na Wasukuma pia wapo. Kwa hiyo sio suala la kusema kwamba eti mipango haiendi kwa sababu wapo kule Wamakonde au Wamachinga peke yao, ila ile ni nchi yao! Kwa hiyo, tuone ni

jinsi gani tunawasaidia na ikiwezekana basi tuone tunawakopesha angalau baiskeli kuwapa motisha wale Walimu walioko katika mazingira yale magumu. Wakati nazungumzia Shule za *Primary,* labda sasa niende kwenye Shule za Sekondari. Katika Taarifa za Wizara Mkoa wa Mtwara unaonesha una Shule 25 za Sekondari; kwa nini? Sababu ni zile ambazo nimezisema kule mwanzo kwamba ukosefu wa miundombinu, ukosefu wa motisha, walimu au watumishi wanakuwa hawataki kuja katika Mkoa ule. Kwa hiyo, utakuta na Serikali imekuwa imejisahau kabisa, imeachia. Hizi Shule ambazo zimetajwa, wamejenga wananchi wenyewe kwa njia ya kujitolea. *(Makofi)*

Kwa mfano ukienda Tandahimba, Newala japokuwa kwenye jedwali lile la Shule 25 za Wizara wamesema kwamba Shule za Serikali, ni baada ya kukabidhi. Sasa je, unaweza ukawa ni mkweli kama Mcha Mungu, kama ni Muislam au Mkristo lazima tuiangalie hiyo, tusiangalie sheria tu na kanuni na dini pia tuiangalie. Katika Mikoa mingine wamejenga wananchi wenyewe kwa njia ya kujitolea? Hawakupewa Serikali Shule? Sasa na Mikoa mingine kama Mtwara au Kanda ya Kusini, Serikali ijenge basi shule ili na wenyewe wajisikie kwamba wako sehemu ya Tanzania.

Lakini wanahangaika wenyewe, hakuna motisha na ndio maana uwiano wa Shule, idadi zimetofautiana. Mikoa mingine ina Shule 65, 75, 80, lakini katika Mkoa wa Mtwara Shule 25. Hilo ninasema kwa uchungu sana kwamba hatujachelewa kwa sababu ndio Bajeti hii tunaizungumza, Mheshimiwa Waziri aone jinsi gani Mkoa wa Mtwara unainuliwa kielimu. Elimu ni bora, elimu ni muhimu na wote tunaitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, katika Mkoa wa Mtwara wasichana ambao wamekosa Shule kwa kupata mimba ni 888 na kati ya hao ambaye amehukumiwa ni mmoja tu. Je, hawa wengine wako wapi? Ni wazi kwamba sheria ziko za utata, bado wananchi wale hawajazijua. Serikali inazungumza humu kila siku inasema kwamba sheria tunazitunga na tutasimamia, lakini tunazisimamiaje wakati watoto wa kike wanaumia? Eh! Wanaoweka mimba sio wanafunzi tu, wengine ni watu wazima, Maofisa na bado hao watoto wa kike tunawaacha wanakosa elimu, haki haitendeki! Tunataka na watoto wa kike nao wasome, waende Chuo Kikuu na wenyewe.

Raslimali tunaikosa kupitia akina mama. Kwa sababu wapo akinamama ambao wana vipaji vizuri sana, wameshika Wizara, wameshika Idara, wako wengine ma-*Captain,* lakini je, hawa ambao tunawaacha leo, kesho wangekuwa na wenyewe watu wazuri wa kutoa mchango katika Taifa hili? Kwa hiyo, sheria nataka zikae wazi. Ikiwezekana baada ya Bunge hili tuone sheria zinatumikaje za kuwanasa wale ambao wanaharibu watoto wa kike ili na wenyewe wapate elimu sawa. Hili sio tatizo la Mkoa wa Mtwara, ni tatizo la nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa uchungu kabisa, katika Shule za Sekondari zilizoko katika Mkoa wa Mtwara nyingine hazina Walimu wa kutosha. Pia katika masomo ambayo wanapewa hawa wanafunzi wanakosa somo la sayansi. Somo la sayansi watawezaje kusoma kama walimu hawapo na hili ni somo nyeti? Nasikia, sina hakika kwamba mtoto kama hakufaulu somo la sayansi ambalo lina *marks* kubwa, halimpasishi vizuri. Tangu tumepata uhuru watoto wetu wamekuwa wanakosa somo hili. Lakini

Mikoa mingine masomo ya sayansi watoto wamekuwa wakifaulu. Hilo nalo hamwoni kwamba ni jambo ambalo sio zuri? Mimi nataka mabadiliko yafanyike kwa kuona hizi Shule na zenyewe zinapata walimu wa kufundisha masomo ya sayansi kusudi nao washinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tumepata mafunzo hapa kupitia Wizara ya Ujenzi, wanasema wanataka ma-*engineer*. Hivi *engineer* unampataje? Tunataka ma-*doctor, doctor* unampataje kama somo la *science* halipati? Kwa hiyo, hicho ni kilio cha Mkoa wa Mtwara ambacho nakiwasilisha hapa kwamba Wizara ya Elimu iwe makini iangalie na uwiano uwepo na kuangalia matatizo, jinsi gani tuwasaidie hawa wanaojituma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikirudia kule nyuma, ingawa haipendezi, historia inajiandika. Sisi katika Mkoa wa Mtwara tulikuwa wa kwanza kwa kutekeleza mpango wa MMEM na sherehe ilifanyika pale Kitaifa. Kipindi hiki tumekuwa wa pili kwa Shule za *Primary.* Halafu ni hao hao ambao hatupati huduma nyeti za Serikali. Eti ukisema humu ndani wanasema Mkoa wa Mtwara wanapenda kulalamika. Sio kulalamika jamani, tekeleza basi hizo huduma uone kama tutasema sisi!

**MBUNGE FULANI:** Pasua.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Kilugha wanasema: *Yahaliwangu nghava nkakuleke! (Kicheko)*

Maana yake ni kwamba, "Sasa atakuwa anafuata mfupa tu kila siku na mkono sasa hivi ananirushia na ndio Mheshimiwa Boma naishi kwa matumaini".

Mheshimiwa Spika, Bajeti tunapitisha kila mwaka kipindi kinakwisha sijui nitasema nini mimi ndani ya Mkoa wangu kama Mbunge kwamba mambo gani nilisema katika Bunge, maswali gani niliuliza ambayo Serikali ilinitekelezea?

Tunataka sisi kuishi kwa matumaini kuishe kabisa na sisi tuishi kwa kuiona Serikali yetu. Serikali ni sikivu, inajali watu wake, lakini katika vipengele hivi inajali kivipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasikia uchungu sana. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Kweli! *(Kicheko)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Kwa hiyo naona kheri ninyamaze lakini kwa maana ya kuishi kwa matumaini na kwa kutegemea Wizara itekeleze. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RAMADHAN H. KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia leo katika hotuba hii ya Wizara ya Elimu. Kwa sababu ndio kwanza nasimama kuongea, ningeomba nitumie nafasi hii kutoa pole na rambirambi kwa wale wote waliopata matatizo hapo nyuma kidogo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Vile vile niwapongeze Wabunge wenzake, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Kissassi, Mbunge wa Dimani, Mheshimiwa Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini na Mheshimiwa Dr. Shija, Mbunge wa Sengerema wote kwa kuchaguliwa katika Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Vile vile ningependa nimpongeze Dr. Pius Ng'wandu kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu wa Afrika na vile vile nimpongeze Ndugu Arcado Denis Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira. *(Makofi)*

Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum na pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitapenda pia niwapongeze Wabunge wengine wawili, Mheshimiwa Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge hili na vile vile nimpe pole kwa ajali aliyoipata wakati akija Bungeni.

Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki katika uchaguzi mdogo uliofanyika tarehe 30 Mei, mwaka huu, 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe pole kwako na kwa Bunge zima pamoja kwa familia ya Marehemu Mwalyego, kwa kifo cha Mbunge mwenzetu huyu kilichotokea ghafla tukiwa hapa Bungeni. Aidha, ningependa pia niwape pole Waheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda na Dr. Aisha Kigoda, kwa kupotelewa na Marehemu mpendwa Baba yao.

Vile vile niwape pole Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama na Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na watoto wao na nimalizie labda kwa kuwapa pole wenzetu waliopata ajali njiani wakija huku na mikasa mbalimbali kama Mheshimiwa Anne Kilango pamoja na mkasa uliotokea hivi karibuni katika Wilaya ya Mbarali wa ajali iliyoukumba msafara wa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nimpongeze sana Waziri wa Elimu kwa hotuba yake aliyoitoa leo na ninataka kwanza kukiri kwamba wenzetu hawa kwa hakika wamezingatia dira yao kama inavyoonekana na vile vile dhima kama walivyoainisha.

Kwenye dira naomba nisome, wanasema hivi: “Kuwa na Mtanzania aliyeelimika kwa kiwango cha juu, mwenye maarifa, mahiri na aliyekomaa kiutamaduni ili aweze kukabiliana na changamoto za Kitaifa na Kimataifa katika nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi ifikapo mwaka 2025".

Hiyo ni dira na ukisoma kwa makini hii hotuba ambayo iko mbele yetu hapa inaonekana kabisa inaelekea huko, yaani dira kama inavyojieleza hapa. Mimi katika dhima, wanasema kuhakikisha kuwa kuna mazingira mazuri ya kisheria na kiutendaji yatakayowawezesha wadau wote wenye nia na uwezo wa kutoa Elimu iliyo bora washiriki kupanua Elimu hiyo katika ngazi zote na kutoa fursa sawa ya Elimu bora kwa wote pamoja na kuimarisha uendeshaji, Usimamizi na miundombinu ya Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, mimi nawapongeza sana wenzetu hawa katika Wizara hii kwa haya ambayo tumeyaona hapa, wametusomea hapa na kama ilivyo katika dira na dhima kama nilivyoisoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mimi nitapenda nifungamane zaidi na hotuba hii hii bila ya kutoka nje kwa kusema kwamba tuangalie ukurasa wa tatu, wanazungumzia utekelezaji wa mipango ya 2003/2004 katika upande wa Elimu ya Msingi. Mimi ni shahidi kwamba kweli utekelezaji wa mpango katika mwaka 2003/2004 kwa kweli mipango hii ilitekelezwa kwa kiwango cha juu sana cha ufanisi na mfano wa haya naweza nikazungumzia ni baadhi ya wafadhili waliokuja nchini kutoka Jumuiya ya Ulaya walitaka kuona nini kimefanyika katika awamu ya kwanza ya mpango huu wa MMEM walikuja Bagamoyo. Msafara ule uliongozwa na Profesa Seilla akifuatana na Dr. Black kusema kweli walipofika Bagamoyo walipoona baadhi ya shule ambazo zimejengwa kwa kufuatana na mpango huu waliridhika sana na kutuhakikishia kwamba wangependa kuisaidia nchi yetu katika kuendeleza Elimu. Kwa hiyo, huo ni ushahidi toka kwamba kweli walichokisema hapa katika utekelezaji wa mpango huu wa Elimu ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, vile vile tukiangali ukurasa wa tano, mafanikio ya kufaulu vijana wetu shuleni. Ni kweli kwamba kuongezeka kwa wanafunzi kufaulu kufikia asimilia 40.1 kutoka asilimia 27.1 vile vile ni ushahidi kwamba tunapiga hatua katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo pia ningependa kulizungumzia ni kwamba sasa hivi elimu ya Msingi kusema kweli tunapiga hatua kubwa na ni vizuri kwamba vijana wetu sasa wanaonekana kushiriki kikamilifu katika kujiendeleza na katika kuondokana na tatizo la ujinga. Kabla sijamalizia eneo hilo la elimu msingi ningependa nizungumzie tatizo ambalo lilikuwa linakabili eneo la Bagamoyo. Bagamayo lilikuwa ni eneo pekee nadhani nchini lililokuwa na shule duni sana. Mfano mzuri ni shule iliyokuwa inazungumzia sana ya Mwetemo na kupigwa picha nyingi sana vile vile shule ya Visezi. Lakini leo shule hizo ukiziona kwa kweli hutaamini kwamba ni zile zilizokuwa katika hali mbaya kiasi kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa nipongeze Wizara kwa jinsi ilivyosimamia mradi mzima huu wa MMEM na maandalizi yaliyofanywa katika kuziandaa Kamati zetu za Shule katika kusimamia matumizi ya fedha za MMEM katika shule mbalimbali. Mimi binafsi ningependa kuzipongeza Kamati zote za Shule katika Wilaya ya Bagamoyo kwa jinsi zilivyosimamia mradi huu wa MMEM na kuonyesha mafanikio makubwa katika eneo lile. Kusema kweli nazishukuru sana Kamati za Shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye Idara ya Elimu ya Sekondari, ukurasa wa 11 kusema kweli vile vile naona maadalizi yanaanza kuwa mazuri kwa upande huu ukitilia maanani mafanikio makubwa yaliyopatikana katika mpango wa elimu ya Msingi, tusingejiandaa upande wa Sekondari ungekuwa mashakani kuhimili wimbi kubwa la watoto wanaomaliza elimu ya msingi kuingia Sekondari, ukurasa wa 11 Serikali inasema kwamba Serikali itafanya jitihada kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa kuweza kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za shule na vyuo vingine vya mafunzo. Hili ni jambo zuri na linaonyesha jinsi gani Wizara imejiandaa kikamilifu kukabiliana na hali hiyo. Vile vile kiwango cha kufaulu katika shule za sekondari ukurasa wa 14 vile vile wanatueleza kwamba tumepiga hatua katika eneo hili na kwamba napenda niipongeze shule ya Sekondari ya St. Mariam pale Bagamoyo kuwa ya kwanza kitaifa katika kufanikisha wanafunzi wake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda kuwa mchache na nina mambo mengi naomba niende haraka haraka ukurasa wa 19 pale kuna mpango wa Sekondari. Mimi nilikuwa ni miongoni mwa watu ambao walikuwa na mashaka sana na mipango ya Sekondari kutokana na eneo letu kuwa katika moja ya maeneo ambayo yana shule chache sana za sekondari. Lakini jawabu ninalipata katika ukurasa wa 25 katika kipengele cha 18.2 kwamba wanazungumzia mipango ya kuhudumia maeneo ambayo yana shule chache na kweli Bagamoyo ni moja katika maeneo yanayoangukia katika tatizo hili. Kwa hiyo, naishukuru Wizara kwa kuliona hili na kwamba naomba nikumbushe kwamba kama wakati utafika basi haya yaliyopo hapa kwa maneno yangewekwa katika vitendo ili tuweze kukabiliana na tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla kengele ya pili haijanililia ningeliomba kwamba niipongeze vile vile Wizara pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kulikabili tatizo la madeni ya Walimu na hatua ambazo zinachukuliwa.

Kusema kweli tatizo hili lilikuwa la nchi nzima wala halikuwa la eneo moja na kila mahali na kila mmoja alikuwa anaona kwamba kwake lilikuwa baya zaidi lakini kimsingi ni kwamba lilikuwa la nchi nzima na tayari tumepata jawabu. Ningeomba tu Wizara iendelee kulisimamia vizuri litekelezwe kwa ufanisi mkubwa tuondokane na tatizo hili moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 36 unazungumzia kuwafundisha mafunzo ya management Walimu. Mimi nafikiri hili vile vile linanipa moyo na chuo hiki bahati mzuri kipo pale kwetu Bagamoyo naona jinsi walivyopanga kuwaelimisha Walimu na hii inanipa ubora kwamba wale wanaolalamika kwamba ubora wa elimu ni duni labda wangeanza kutokwa na mashaka kwamba tunaendelea kuboresha viwango vya Walimu

kusudi na wao waweze kutusaidia kuboresha kiwango cha elimu kwa wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba tu nisije nikasahau kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenyewe pamoja na Katibu Mkuu, Wataalam wake wote kwa kuandaa hotuba hii vizuri na mimi naomba niishie kwa kusema kwamba naiunga mkono hoja hii kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Elimu na Utamaduni. Kabla ya yote napenda kutoa pole kwa familia ya Marehemu Yete Sintemule Mwalyego. Naomba Mungu awape subira na Mungu amweke mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepotelewa na wapenzi wao tukiwa katika Bunge hili. Naomba Mungu awape subira na aziweke roho za Ndugu zetu waliotangulia mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga kwanza kwa kufanya uamzi wa burasa wa kurejea nyumbani katika Chama Cha Mapinduzi. Karibu sana Bwana Makanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili napenda kumpongeza Bwana Makanga kwa ushindi wa kishindo aliowaonyesha wana Bariadi kwamba CCM ndiyo chama ambacho kinafaa kukaa na watu ambao wanataka kuijenga nchi yao kwa uaminifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Elimu na Utamaduni na kumpongeza Waziri hasa na viongozi wenzake akiwemo Katibu Mkuu, akiwemo Kamishna wa Elimu pamoja na Wakurugenzi weote kwa jinsi walivyoandaa hotuba hii ambayo ni mzuri kwa kweli inaonyesha wazi utaalam ulivyo katika Wizara ile. Ingepaswa hata tusichangie kwa sababu inajieleza wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa vile tumeona mambo mengine kweli kuandika ni kuzuri sana lakini pengine utekelezaji kwa ajili ya watu ambao wanapswa kutekeleza yale ambayo yameandaliwa katika kitabu hiki kizuri yanashindakana, basi pale na hapa ni vizuri tuweze kuwakumbusha wenzetu kwamba labda wawe makini kwa sababu ya utekelezaji.

Mhesahimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Walimu na maslahi yao kwa kero. Kwa sababu mipango mizuri iliyoko katika kitabu ambacho Mheshimiwa Waziri alikuwa anasoma na wewe ni shahidi ulisikia makofi ya watu wakipiga kwa nguvu zao zote Wabunge wakichangamka ambavyo unaona huwa inatokea mara chache ni kwamba

ni mipango mizuri lakini ni kwa nini Walimu hawa ambao hata mwaka jana tulikuwa na Bajeti nzuri ya Wizara ya Elimu na Utamaduni Walimu hawa wanasumbuliwa hawapati haki yao kwa sababu kila Mtanzania katika nchi hii anapewa haki kwa kulingana na kazi yake anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi kuona Walimu jinsi wanavyofanya kazi zao vizuri. Katika kazi zote ngumu ambazo Serikali inataka zifanyike kwa haraka wanaokimbiliwa ni Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Sensa, katika Uchaguzi na katika kazi nyingine mbalimbali ambazo zinahitaji kuangaliwa kwa uangalifu zinafanywa na Walimu. Ni vipi Walimu hawa wasiweze kupewa mshahara wao kwa wakati unaotakiwa, wasipewe nyongeza sawasawa na mishara yao. Ni lazima zirundikane ili waje wapewe baadaye hizo fedha zitatoka wapi katika Bajeti ipi. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu ameagiza na bila shaka itasababisha kuunda Kamati na Kamati hizo ambazo zitalipwa fedha, sasa mimi najiunliza Wizara zinaunda kazi kwa watu fulani au zinatakiwa nini, hawatekelezi kazi vizuri ili watu wapate kuingia kwenye Kamati wakapate posho au ni kitu gani?

Mheshimiwa Spika, ninaiomba sana Wizara, suala la Walimu kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyosema iwe mwisho jamani kuzungumza kila siku Walimu, Walimu. Kwa sababu hata hawa walioandaa kitabu kama wasingepita kwenye mikono ya Walimu wasingekuwepo hapo walipo. Hata huyo *Chief Education Officer* kama ndiyo amefanya kazi hiyo na timu yake asingekuwepo bila Walimu. Kuanzia *Primary* mpaka Chuo Kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wako ma-*DEO* mnao, kama Mkurugenzi anazembea hawa wanaletaje taarifa kwako. Na wakileta taarifa unafanya nini na hiyo taarifa kwa sababu Maafisa Elimu wapo. Haiwezekani mkasema tu Wakurugenzi wanazembea. Hata Maafisa Elimu wenu ni wazembe. Tena ni wazembe wa kutupa, kwa nini mpaka zifike zaidi ya bilioni 4 za nyongeza tu za Walimu na wao wako kule Vijijini. Na wao ndio wanasaini zile fomu za likizo. Anastahili kwenda likizo. Sasa kama mtu anastahili kwenda likizo si lazima apewe hela? Kuna Tume ya Walimu katika kila Mkoa kila Wilaya zinafanya nini? Kwa nini malimbikizo haya yakaweze kufikia kiasi kilichofika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kuna mahali ambapo ni lazima Mheshimiwa Waziri akaangalie kwamba watu wawajibishwe hatuwezi kuja tu hapa kila mwaka aje atusomee taarifa nzuri zilizoandikwa vizuri lakini utekelezaji wake uwe wa kutisha kama hivi. Tumejenga majengo mazuri, tunampongeza sana Walimu na wenzake, Waziri wa Elimu na Utamaduni na wenzake kwa jinsi walivyojenga majengo mazuri kwa MMEM. Lakini kama majengo haya yatakaa na watoto wasiofundishwa, kuna faida gani. Hakuna maendeleo yoyote, maana Walimu watakuwa na mgomo wa kimya kimya na sisi tunafikiri ni vyema Walimu wasiwe provoked wakaanza kugoma kimya kimya, kuna mwenzangu mmoja aliyetangulia amesema kwamba kuna tuition ambazo hata zimebadilishwa na majina. Sasa tusiwafikishe hapo Walimu katika nchi yao ambao na

wenyewe ni raia ambao wanastahili kupewa haki wakapoteza haki zao kwa kutokufuatilia vizuri. Naomba muwawajibishe na ma-*DEO* na Maafisa Elimu.

Mkurugenzi anaweza kuwa hana shida na mwalimu. Sasa mtoto wa kambo kama mama hamtumzi vizuri, mama wa kambo anaishi na mtoto wa kambo asipomtunza vizuri ni lawama ya baba. Baba anakuwa wapi? Kwa nini haulizwi? Baba atalaumiwa. Kwa sababu wewe una hakika kabisa kwamba huyu mama hakumzaa huyu mtoto. Inawezekana asiwe na mapenzi ambayo anatazamia kwake. Kwa hiyo, ni lazima baba uwe karibu sana. Sasa ma-*DEO* ndiyo wenye uchungu, akina mama kule. Ndio mama wa Walimu, wako wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aniambie Walimu wake huko Mikoani na Wilayani wanafanya nini? Naomba aangalie kwa makini kabisa masuala yanayohusu Walimu. Vifaa katika kitabu alichowakilisha leo Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba vifaa vya kufundishia Walimu wanapata na ambavyo ilikuwa kero sana siku zilizopitwa. Sasa sijui kama wanavitumia hivyo vifaa. Kwa sababu kama mtu ameumia ni vigumu sana kufanya kazi kwa umakini. Mimi wakati mwingine nilipokuwa nasoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa mapema nikasema labda kuna njama fulani, labda wana chuki fulani, wale wanaotekeleza kazi za kuwalipa mishahara, na kuwalipa haki zao wana nini kwa nini hawezi kuwalipa wenzao haki kama inavyopaswa.

Je, yeye mwenyewe huyu mliyemweka aangalie kama hakulipwa kama hakwenda likizo, kuna Walimu wameniambia miaka minne hawajaenda likizo. Haki iko wapi kwa mwalimu. Naomba tuwatendee haki kama raia huru katika nchi yetu ambayo wanastahili kupata haki zao zote.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuzungumza kidogo juu ukaguzi. Naona wamefanya kazi yao viziri. Lakini nikashitushwa kwenye Idara kwamba magari mawili tu yalinunuliwa. Magari mawili yanafanya nini. Mheshimiwa Waziri naomba magari yaongezeke, unapoweka Bajeti punguza kidogo kwenye shughuli zingine ambazo nyingine sio nyeti sana. Moyo wa Wizara ni wakaguzi. Ukaguzi ni moyo wa Wizara. *(Makofi)*

Ili wafundishe vizuri Walimu kule wakijua kwamba Mkaguzi anaweza kwenda wakati wowote watafanya kazi yao vizuri. Kwa hiyo, ninaomba Wizara iimarishe ukaguzi, iimarishe Ukaguzi, iendelee kuimarisha isiridhike na kwamba wamekagua hizo shule 1,115, haitoshi. Kwa hiyo, tunaomba huduma kwenye ukaguzi ionekane.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia pia juu ya Taasisi ya Elimu. Taasisi ya Elimu ndiyo inayotunga mitaala. Katika taarifa hii Taasisi ya Elimu inaonekana imefanya kazi nzuri na wametunga mitaala. Lakini sina hakika kama hii mitaala inaendana na vitabu vya kiada.

Mheshimiwa Spika, naomba Taasisi ya Elimu, inapotunga mitaala yake iende pamoja na vitabu vya kianda ili taaluma iweze kuhamishwa vema kwenda vichwa vya

wanafunzi. Kwa sababu mwalimu anapokuwa na mtaalam tu ameshika mkononi peke yake bila vitabu vya kiada vya wanafunzi, kazi inakuwa ngumu zaidi kwa mwalimu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie Bodi ya Huduma za Maktaba kama ndiyo inasimamia Maktaba zilizo Mikoani. Kuna Maktaba nyingine kwa kweli zinatisha. Maktaba yetu kule Kagera, Mkoa wa Kagera haina vitabu, inavuja. Na walijaribu kujenga nyumba nyingine pale pembeni tangu mwaka 1988 msingi uko vile vile mpaka leo. Sasa kama Bodi ya Huduma za Maktaba ndiyo inasimamia Maktaba za Mikoa ninaomba iongeze nguvu waweze kuangalia kwamba maktaba hizi hazivuji, kwa sababu kama tutatoa wanafunzi wengi kama Mheshimiwa Waziri alivyotuambia na tukafurahi kwamba mamilioni ya wanafunzi watakaotoka shule za Sekondari wakikaa hivyo hivyo hawataweza kuendelea lakini wakiwa na Maktaba mahali ambapo watakwenda kuongeza kunoa elimu yao itawasaidia. Maktaba ni kitu kizuri sana kwa maendeleo ya binadamu.

Kwa hiyo, naomba Bodi ya Huduma za Maktaba isiwe tu pale kwenye *Tanganyika Library* na mahali pengine waziboreshe Maktaba za Mikoa kama tunavyohitaji.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Kiswahili. Nimeona wameainisha kazi nzuri nyingi na ambazo nyingine ni kweli tunaziona. Lakini tumepata heshima ya Kiswahili kuzungumzwa katika Afrika. *(Makofi)*

Ni heshima ambayo ni njema kwetu. Na ni baraka kwetu. Kwa sababu Kiswahili kimetuunganisha Watanzania. Kwa hiyo, mimi nafikiri labda huo utakuwa ni mwanzo pia wa kuunganisha Afrika. Kwa hiyo, mimi naomba Baraza la Kishwahili liwe na mitaala ambayo itawafundisha vizuri wakalimani. Wakalimani wajifunze waelewe ili wanapokwenda katika Bunge, Bunge la Afrika na katika mikutano ya Afrika ya viongozi, Marais waweze kutafsiri na watu watamani kujifunza Kiswahili. Mimi naomba sana hilo ni ombi na ninajua jinsi mlivyo mtalitekeleza. Kwa sababu mambo ya ubora huu mnajua.

Sijui ni mahesabu tu yanatupiga chenga ndio huwa hamwezi kufuatilia kulipwa Walimu. Mimi sielewi kwa sababu mambo mengi Wizara ya Elimu na Utamaduni inafanya vizuri. Ila tu maslahi ya Walimu, labda hamna watu wa mahesabu huko kwenye Wizara yenu. *(Makofi)*

Basi nitamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha pia awape, mfanye kazi njema kama mlivyozifanya. Nimefurahi kusoma mambo mengi katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ninaomba Wizara ya Elimu na Utamaduni, iangalie elimu ya watu wazima. Ni msingi wa kuwasaidia Watanzania wakaweze kufanya kazi zao vizuri. Kumfundisha mtu mzima aelewe. Lakini sijui kama imetajwa hapa. Kwa sababu mambo ni mengi nilikuwa nakimbia kimbia. Inawezekana ipo mipango ya elimu ya watu wazima labda nimepitiwa, licha ya Taasisi. Mimi nafikiri elimu ya watu wazima ni ya msingi pamoja na watoto wakubwa wamepita umri wa kuanza shule wataingia katika madarasa. Lakini wako walio tayari kwenye kilimo.

Tunawafanya nini hawa ambao wanalima sasa hiyo, watoto wanaoendelea katika MMEM na MEMKWA na shughuli nyingine waweze kufuata.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri katika hilo alivalie njuga. Elimu ya watu wazima. Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wasemaji wetu wawili wa mwisho ni Mheshimiwa Maria Watondoha na Mheshimiwa Jenista Mhagama. Mheshimiwa Makwetta atakuwa wa kwanza kipindi cha mchana.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja hii ya leo ya Wizara ya Elimu ya Utamaduni. Awali ya yote naomba niungane na Watanzania wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba Rais wetu mpendwa amerejea nyumbani na tuendelee kumwombea ili afya yake iweze kuendelea kuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili niungane na wananchi wa Mbeya Vijijini katika msiba wa Ndugu yetu Mpendwa Marehemu Yete Mwalyego, ambaye ametutoka hapa duniani, lakini kazi ya Mungu kwa kawaida haina makosa. Kwa hiyo, naomba wananchi wa Mbeya Vijijini tumshukuru Mungu tuendelee kumwombea, roho yake ailaze mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, niungane pia na Waheshimiwa Wabunge katika kumpa pole Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, kwa kufiwa na mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, niungane pia na wenzangu kuipongeza Wizara ya Elimu na Utamaduni kwa hotuba yao nzuri ambayo wameiwasilisha hapa. Napenda kumpongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu wake, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Katibu Mkuu, Mama Malale, Walimu wenzangu wote pale Makao Makuu ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na Wataalmu wengine na Walimu wote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba awali ya yote niwape pole kwa kazi ngumu ambayo wanaifanya. Kwa kweli kazi ya ualimu ni kazi ya wito na ni kazi nzito na nyeti. Baadhi wanaifanya katika mazingira magumu sana. Ninafahamu wapo waalimu ambao hawafanyi kazi yao vizuri. Lakini hatuwezi tukasimama Bungeni tuka-*generalize* tukisema Walimu ni wa ovyo. Walimu wanafanya kazi nzuri na wanastahili kupongezwa. *(Makofi)*

Hata wataalam wetu walio Wizara ya Elimu na Utamaduni nina hakika wanafanya kazi nzuri na isingewezekana kuwa majalada yote yapotee, ama sivyo wengine tuliostaafu tusingeweza kuyaona. Wanafanya kazi nzuri lakini liwizara lile lazima tujue ni kubwa, Elimu na Utamaduni. Kwa hiyo, kazi yake pale ni kubwa. Mimi naomba waendelee na kazi nzuri wanaoifanya sasa. Kwa mfano mmoja tu ukitaka uhamisho wa mwanafunzi wa shule ya sekondari ambao unafanyika Wizara ya Elimu na

Utamaduni, haichukui zaidi ya siku mbili ambayo ni *improvement* kubwa sana kuliko miaka ya nyuma na wote tunafahamu. Naomba waendelee na juhudi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze hotuba nzuri aliotoa Mheshimiwa Waziri ambayo kwa kweli inatoa matumaini makubwa kwa wananchi Watanzania. Inatuonyesha azma ya Serikali ya CCM kuhakikisha kwamba tunaenda na wakati. Maana nchi yoyote ikiwa na watu ambao hawana elimu hawawezi kuendelea. Kama wahenga walivyosema elimu ni ufunguo wa maisha. Pamoja na hotuba nzuri hii ninaomba nichangie katika maeneo yafuatayo na kutoa ushauri.

Kwanza, nipongeze mpango wa MMEM, umetekelezwa vizuri. Tuna madarasa ambayo yanavutia. Ukienda Vijijini sasa unajua kweli kuna elimu inatolewa. Lakini elimu si madarasa peke yake, ni pamoja na vitabu vya ziada na kiada ambavyo Serikali inatolea mchango wa fedha, inatakiwa kuwepo kwa Walimu. Walimu wa kutosha, ninasisitiza Walimu wa kutosha. Maana ukimpa mzigo mwalimu kwa kweli atafanya kazi ya kulipua maana na yeye ni binadamu na anachoka. Akiwa na kazi ya kusahihisha madaftari 100 hawezi kukamilisha, ndiyo maana unakuta wengine wanabadilisha *exercise* za wanafunzi darasani, mwalimu anatoa majibu huku anasahihisha.

Kwa hiyo, unakuta anatiki mengine ambayoni makosa. Kama mzazi makini unafuatilia unakuta makosa yametikiwa vema wakati kwa kweli ingekuwa kosa. Kwa hiyo, nasisitiza suala la Walimu wa kutosha na Walimu wenye taaluma.

Mheshimiwa Spika, mpango wa MMEM ulivyoanza tulijenga madarasa ya kutosha. Tuka-*enroll* wanafunzi wengi lakini hatukuwa na Walimu wa kutosha. Kwa hiyo, tatizo likawa pale pale kwamba tume-*enroll* wanafunzi, hatuna Walimu. Kwa hiyo, mimi ninachoshauri Serikali ninaomba suala la elimu tusifanye *crash programme.* Ni kweli vyuo vingi vilipewa nafasi ya kufundisha Walimu katika kipindi cha mwaka mmoja tofauti na miaka miwili ili tupate Walimu. Lakini wakati huo wanafunzi tayari walikuwa mashuleni na hawana Walimu. Ninashauri tuwe na mpango kwamba tunajenga madarasa huku tuna-*train* walimu. Madarasa yamekamilika walimu wamekamilika tu-*enroll* wanafunzi wa kutosha ili wanafunzi wakifika wasikae *idle.*

Mheshimiwa Spika, tumesikia kwenye redio, sehemu mbalimbali, kuna shule mwalimu mmoja, walimu wawili ambao kwa kweli hawawezi kukidhi mahitaji. Huo ushauri wangu wa kwanza. *(Makofi)*

Ushauri wangu wa pili, Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulielezwa juu ya mpango wa MEMKWA na leo nafikiri umegusiwa. Lakini mpango huu wa MEMKWA hauna fedha, sijaona mahali ambapo umetengewa fedha.

Mheshimiwa Waziri alituambia kwamba wanaokuwa *enrolled* darasa la kwanza ni wale waliofikia miaka saba, miaka minane kwenda juu wanakwenda kwenye madarasa ya MEMKWA. Sasa Halmashauri kweli zimetenga fedha za kutosha maana kweli sehemu zote unakuta madarasa ya MEMKWA hayana fedha za kutosha. Kwa hiyo, hata wale wanaojitolea wasipopata *honorary* mwezi wa kwanza, mwezi wa pili

wanavunjika nguvu, wale wanafunzi wanang'aa macho. Serikali ilisema kwamba madarasa ya MEMKWA yapo, kwa hiyo naomba tusiwaache hivi hivi.

Serikali iangalie uwezekano na ihakikishe, siyo uwezekano tu, bali ihakikishe kwamba hawa wanatengewa fedha za kutosha maana ni wanafunzi wa Kitanzania wenye haki ya kupata elimu. Inawezekana wamechelewa kuwa *enrolled* darasa la kwanza walipofika miaka saba kwa sababu ambazo zilikuwa nje ya uwezo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, naomba niipongeze Wizara katika mpango wao wa kuongeza au kupanua elimu ya sekondari. Kwa kweli elimu ya msingi, tu ikipanuliwa na ukawa na wengi nchini wana elimu ya msingi haiwezi kukidhi haja. Lakini tukiwa na vijana wengi waliomaliza elimu ya sekondari basi tutakuwa na wananchi wengi zaidi ambao wana upeo. Lakini katika hili pia naomba nishauri kama nilivyoshauri kwenye MMEM kwamba tupanue shule za sekondari lakini vile vile tuongeze walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazo shule ambazo zina matatizo ya walimu, nichukue mfano wa shule ya sekondari ya Liwale ina *stream* mbili mbili toka *form one to four* lakini ikama ya walimu ni tisa. Hawajavuka hapo kama wamefika sana labda kumi na mbili, hawakidhi mahitaji. Nenda shule ya sekondari ya Mitole hawajawahi kuwa na mwalimu wa hesabu, wanafunzi wanasoma pale, wazazi wanahangaika maana shule ya sekondari ya Mitole iko Kilwa huko Vijijini ndani, wazazi wanatakiwa wachangie chakula na wanafunzi hawana walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, shule ya sekondari ya Matanda nayo ipo Kilwa, mwalimu anakaa miezi miwili au mitatu anahama. Kweli wanahamishwa kwa utaratibu lakini kwa nini wakae kipindi hiki kifupi ndio wahame. Wanafunzi pale wanabaki bila walimu. Naomba kutoa wito kwa Serikali tusiandae *semi-literacy* watu ambao wamepata elimu nusu, tunataka waandaliwe watu wenye taaluma ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tuangalie *analysis* waliofanya katika hii *basic statistics* ya *division one* mpaka *four* na *failures*. Ukiangalia *division one* bado ni wachache sana na hiyo inadhihirisha kwamba tuna upungufu wa walimu. Kama tungekuwa na walimu wa kutosha wa taaluma zote, *division one* wangeongezeka. Lakini angalia *division four,* mwaka 1995 ilikuwa 55%; 2002 ni 50.1% na 2003 ni 50%. Kwa hiyo unaona wazi kabisa kwamba kiwango cha kufaulu bado ni kidogo na hii ni kwa sababu hatuna walimu. Kwa sababu, mwanafunzi kwa mfano wa shule ya sekondari ya Mchinga, Mtama, Nachingwea hana walimu wengine lakini atafanya mtihani sawa na mwanafunzi wa Dar es Salaam ambaye ana walimu wa masomo yote.

Sasa huyu mwanafunzi wa Mchinga, Nachingwea au Liwale unatarajia atafikia kiwango kweli kinachostahili au tutapata wanafunzi wanaoingia *form five* na *six!* Naomba sasa Wizara pamoja na kufanya *analysis* hii ya waliofaulu *division one, two, three* mpaka *four* na waliofeli, naomba watuonyeshe waliofaulu *division* hizi wengi wanatoka wapi Mijini au Vijijini. Utakuta wengi wanatoka Vijijini, nina hakika sio wa Mijini maana wa Mijini wana umeme, wana *computer,* wana a*ccess to libraries,* wana

walimu wanaweza kuwapa *tuition* lakini wa Vijijini ndiyo hawa wengi wanaopata *division three, four and failures;* lakini ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ushauri wangu ili tuhakikishe tunatoa elimu bora na ya uhakika na iliyo *equal* kwa Watanzania wote basi tuandae kwanza walimu wa kutosha, tuwasambaze katika shule zote. Mwalimu kama hataki kufika kule asikubaliwe kuajiriwa sehemu nyingine, maana mtu akilalamika anahamishwa anakwenda kwingine. Sasa utakuta mtoto wa Liwale hana mwalimu, mtoto wa shule ya sekondari Mmelo kule hana mwalimu, lakini ni mtu anayestahili kusoma vile vile. Tunataka kupanua vile vile *form five* na *form six* kwa lengo zuri, lakini mimi nina *experience* nilipokuwa Wizarani pale tulifungua nakumbuka *CBN* Maswa, sijui kama inaendelea maana tulikosa walimu wa kwenda pale kwenda kufundisha *Nutrition, Chemistry* na *Biology.*

Kwa hiyo, naomba tusipanue shule tu bila kuandaa walimu. Kilio changu mimi tutoe *quality education* tusiandae *semi-literacy* ambao baadaye watatupa matatizo, hawataweza ku-*compete* na sasa hivi ni utandawazi. Nenda kaangalie maeneo mengine tumeajiri watu wa nchi za nje kabisa kwa sababu vijana wetu wana elimu, wanapenda kusoma, lakini hawakupata kiwango kinachostahili *to the International Standards.*

Mheshimiwa Spika, la nne, naomba nichangie haraka haraka juu ya elimu ya walemavu, niungane na mzungumzaji wa kwanza. Nitoe mfano wa Chuo cha Patandi. Chuo cha Patandi kipo Arusha, kinafundisha walimu wa ulemavu. Lakini walemavu wapo viziwi, wasioona na walemavu wa viungo. Mimi nina mfano wa mwanafunzi amekwenda pale ana ulemavu wa kutokusikia vizuri.

Kwa hiyo, vipindi vingi vimempita na hakufaulu vizuri kwa sababu ya aina ya walimu tulio nao. Viziwi ni walemavu wanaozungumza kwa ishara ya vidole tofauti na vipofu ambao wana *Braille*. Kwa hiyo, maandalizi ya aina ya walimu wanaofundisha walemavu ni muhimu sana maana hata walemavu wana akili nzuri na wanaweza kufaulu vizuri sana.

Sasa chuo kama cha Patandi wahakikishe wana walimu wanaoweza kuwafundisha walemavu wasiosikia na vipofu maana walemavu wa viungo wanaweza kusikia na kuona, kwa hiyo wanaweza kumsikiliza mwalimu. Kwa hiyo, maandalizi ya aina ya walimu ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nizungumzie maslahi ya walimu. Mwalimu akiajiriwa anakaa zaidi ya mwaka halipwi. Kuna urasimu mkubwa sana kati ya Wizara ya Elimu, Idara Kuu ya Utumishi na Wizara ya Fedha au Hazina. Hali hii inakatisha tamaa walimu, vijana wetu wanakwenda Vijijini, hawapati mshahara mwaka, hivi lengo letu ni nini?

Tunataka vijana hawa waishie kwenye UKIMWI, maana mtu akishindwa kuishi atafuta njia nyingine. Nia ni nini na tulishaona mfano katika magazeti na maeneo mengine mwalimu wa kike amebakwa kwa sababu amekosa mahali pa kuishi akalazimika kwenda kuishi kwenye nyumba za watu.

Kwa nini mpaka leo kunakuwa na urasimu mkubwa na tunachelewesha maslahi ya walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naomba kwanza na mimi niungane na wananchi wa Wilaya ya Mbeya Vijijini na hasa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa msiba mkubwa walioupata wa kumpoteza Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Mwalyego. Kwa kweli tunawapa pole sana na tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi pia naungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu Ndugu yetu Mungai. Kwa kweli naweza kusema kwamba Mheshimiwa Mungai ni miongoni mwa wale Askari wa Miavuli ambao wameshatua chini. Baada ya kutua chini wameonyesha ni kwa kiasi gani kwamba ile miavuli yao imebaki huko juu, wao sasa wanafanya shughuli ambazo waliagizwa kuja kuzifanya katika kuleta maendeleo ya elimu katika nchi yetu ya Tanzania. Nampongeza sana na Naibu wake. Lakini nawapongeza sana Wakurugenzi wa Wizara hiyo ya Elimu.

Bunge hili toka lilipoanza kila Mbunge aliyesimama akitolea mifano ya maendeleo onekanivu ilikuwa ni katika sekta ya elimu ikiongoza sekta nyingine pia ambazo zimeweza kuelezewa, lakini kwa kweli sekta ya elimu imejionyesha wazi hasa hata katika maeneo ya Vijijini na hata Vijiji ambavyo viko mbali kabisa na Makao Makuu ya Wilaya na Mikoa. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na nawapongeza sana watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ambaye ni mwanamke mwenzetu na naamini kwamba anaonyesha mfano bora wa watendaji wanawake katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa pongezi hizo katika Wizara hiyo ya Elimu, mimi naomba nianze kuzungumzia kwa usemi ufuatao, kila lililo jema ukifuatilia linatokana na ubora wa elimu au uelimishaji bora ndio unaoleta mafanikio na maendeleo endelevu. Tunapozungumzia suala la elimu, sasa hivi tumebeba bendera ya maendeleo makubwa ya elimu, lakini tukiangalia bendera hiyo tuliyoibeba ya maendeleo makubwa ya elimu inajionyesha katika suala zima la majengo bora, imara, nadhifu ya yenye kuvutia.

Lakini mimi naomba niongeze kwamba haitoshi kujivuna katika nchi ya Tanzania kupiga hatua kielimu ama kwa kuingiza watoto wengi shuleni, ama kwa kuwa na majengo yanayovutia, yaliyo bora na ya kudumu bila kuangalia idadi ya walimu tulio nao kwanza, huduma wanazopata walimu hao ili kuweza kutekeleza azma ya ufundishaji. Lakini vile vile uboreshaji wa mitaala itakayoendana na wakati muafaka wa maendeleo ya Taifa katika karne hii ambayo ni ya utandawazi na inayobeba kwa kiasi kikubwa suala zima la sayansi na teknolojia ya hali yajuu.

Mheshimiwa Spika, sioni kama kuna umuhimu wa kuchukua suala zima la soko huria kuliingiza katika suala la elimu na hasa upande wa vitabu vya mitaala. Vitabu vinavyotumika katika kufundishia kwenye shule zetu. Mimi sioni kama tunaweza kuboresha elimu yetu kwa kuruhusu kila mtu anayefikiria kutengeneza kitabu kinachotumika kama cha ziada ama kiada kikafundishia ama kikatumika kama nyenzo ya kufundishia katika shule zetu bila kuwa na kitengo maalum cha ku-*control* vitabu hivyo vyote katika nchi yetu kama tulivyokuwa na kitengo hicho toka mwanzo. Tunaweza kuwa na soko huria katika mambo mengine lakini sio katika vifaa vya kuboresha elimu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nilizungumze hilo kwa nguvu kubwa kwa sababu sasa hivi imekuwa kama ni tabia, Wizara imesahau kule nyuma tulikokuwa. Tanzania Elimu Supply imefanya kazi kubwa sana kushirikiana na kitengo cha mitaala kuona ni namna gani mitaala inaboreshwa na vitabu vya ziada na kiadi vinatengenezwa kwa uhitaji wa Taifa letu na tuliona kabisa kwamba ni jinsi gani elimu yetu ilikuwa bora katika kipindi kile cha nyuma. Naomba nitoe ushauri huo kwa Wizara kuangalia upya suala hilo na kulizingatia na kulipa kipaumbele cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ushauri huo ningeomba sasa niingie katika ushauri wangu namba mbili kama nilivyosema kwamba elimu bora sio majengo tu bila kuwa na walimu wa kutosha, bila kuwaangalia walimu hao wanapata huduma kiasi gani na bila kudhibiti suala zima la ukaguzi wa ndani katika suala zima la kuboresha elimu. Nilipokuwa napitia taarifa ya mwaka 2003/2004 ya Wizara ya Elimu katika ukurasa wa 24 kulikuwa na tatizo la kupanua mafunzo ya walimu ili yaendane na upanuzi wa elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, imenisikitisha kidogo kugundua kwamba wanachuo wa mafunzo ya ualimu daraja la kwanza wamepungua kutoka 16,189 kwa mwaka 2003 hadi 10,037 katika Vyuo vya Serikali na katika Vyuo visivyo vya Serikali 751 kwa mwaka 2004. Lakini katika eneo ambalo linaelezea matatizo ya tatizo hilo la kupungua kwa walimu hakuna kitu kilichoonyeshwa, ina maana kwamba hakuna matatizo, kupungukiwa kwa walimu ni kwamba hakuna tatizo. Ukiangalia katika *column* ile ya utatuzi hakuna kilichoandikwa. Sasa hili sijui katika huu ukurasa wa 24, tuhesabu ni tatizo ama sio tatizo au ni fanikio ama sio fanikio. Ningeomba wakati Waziri anajibu hoja hizi anisaidie kuelewa, ninaamini kabisa tuna matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, juzi juzi nilikuwa ziara katika Kijiji cha Matimila. Kijiji cha Matimila shule za msingi hazina walimu na labda leo Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hii hoja atusaidie kujua ni vigezo gani vinavyotumika kuwagawa walimu hawa ambao wanapata mafunzo maalum katika kuondoa tatizo la uhaba wa walimu katika maeneo ambayo ni ya pembezoni. Ni kwa nini maeneo mengine hayana hilo tatizo lakini maeneo mengine mengi na hasa ya Vijijini bado tatizo hilo ni kubwa. Tunaomba tusaidiwe.

Mheshimiwa Spika, lakini nilipokuwa naendelea kupitia kitabu hiki katika ukurasa wa 32 huko nyuma tunaona kulikuwa na tatizo pia la kuwa na magari ya

wakaguzi, Mheshimiwa Rhoda Kahatano amezungumza. Wilaya 78 hazina magari na Wilaya 42 magari yake ni machakavu lakini Wizara inanunua magari mawili. Hayo magari mawili yatapelekwa wapi, mimi nilikuwa naomba basi yaletwe Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo, nimesema Mkoa wa Ruvuma Wabunge wote wameguna, ina maana kila mmoja ana tatizo ndani ya Wilaya yake. Kwa maana hiyo tatizo hili ni kubwa na hatujui kwa nini Wizara haikutoa kipaumbele kuangalia tatizo hili na kutoa kipaumbele katika kutatua tatizo la ukaguzi. Lakini hapo hapo tumeona kwamba kulikuwa na mpango wa kuendesha mafunzo ya awali ya ukaguzi kwa wakaguzi wapya 127, lakini bado upo upungufu wa wakaguzi 244, kuwepo kwa mpango endelevu wa mwaka kwa wakaguzi wa shule, sasa kama bado tuna *gap* kubwa ya wakaguzi hao wote, je, tunakwenda mbele au tunarudi nyuma?

**WABUNGE FULANI:** Tunarudi nyuma.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ndiyo maana nasema uwiano wetu upo katika kuboresha majengo zaidi na sio kuboresha elimu yenyewe.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naendelea kuangalia kitabu hiki cha maendeleo na mipango yote kinasema, tunazungumzia suala la walimu kila siku, walimu hawapati huduma bora wanazostahili kupata. Sasa tunasema kwamba katika ukurasa 102 tunaona kabisa kwamba kulikuwa na mpango wa kuwaelimisha walimu majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma ambayo ndiyo ingeweza kusimamia madai yao na mafao yao ya kila siku.

Lakini tunaambiwa kwamba kuna matatizo ya uhaba wa Bajeti na *RTD* haisikiki katika maeneo ya pembezoni ingawa elimu hiyo imekuwa ikitolewa kupitia *RTD.* Sasa tunaitangazaje Tume hiyo na hawa walimu ambao wapo pembezoni wanaotaka kuijua Tume hiyo na kujua haki zao watafanya nini?

Haya ndio mambo ya kuyazingatia, walimu wamekuwa na kilio cha mishahara, malimbikizo yao ya posho mbalimbali na wamekuwa wakiishi katika maisha ambayo ni magumu. Nawashukuru Wabunge wengi wamezungumza, walimu wa kike wananyanyasika katika maeneo wanayoishi.

Lakini hata walimu wa kiume pia wanashindwa kuhudumia familia zao. Sasa kama haya mambo yote hayaeleweki eleweki vizuri, tunafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuona umuhimu wa kuhakikisha malipo ya malimbikizo ya malipo ya walimu yanafanyika katika mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 104 bado kuna matatizo ya kuhakikisha kwamba mafao ya uzeeni na mirathi ya walimu yanashughulikiwa kwa wakati. Sasa pale katika

matatizo panasema, mirathi huchelewa kufunguliwa na kumbukumbu za mirathi kutokamilika ama kutokuwa sahihi. Nani alaumiwe katika hili?

Nilikuwa naomba Wizara ya Elimu sasa hivi iache kutuorodheshea matatizo bali ituletee ni namna gani wamechukua hatua kwa hao wote wanaosababisha matatizo haya ya walimu kila siku na ni namna gani mikakati inachukuliwa ili kupambana na hao wanaotaka kudhalilisha kazi ya ualimu ambayo ni kazi nyeti ambayo kazi hiyo hata Baba wa Taifa alikuwa nayo na ndiyo iliyoletea sifa kubwa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka niongeze lingine moja kabla kengele haijanigongea, nalo ni suala la umuhimu wa lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili imepata umuhimu mkubwa. Tunaona katika *African Union* sasa hivi lugha ya Kiswahili imepewa kipaumbele lakini sisi tutaanza lini kuipa kipaumbele lugha hii ya Taifa? Kila lugha ina kwao. Ndugu yangu Shango alikuwa anazungumzia Kichina, Kichina kina kwao kwa Wachina. Kama ni Kiingereza kina kwao.

Sasa sisi tumepata bahati ya kuwa na lugha ya Kiswahili ambayo sasa inapata umaarufu mkubwa sana katika bara la Afrika, lakini na katika dunia nzima. Sasa hivi tunachelewa nini, hivi ni kwa nini Wizara ya Elimu isianze kuona umuhimu wa kutumia lugha hii kama lugha rasmi katika kufundishia halafu lugha ya Kiingereza ikafundishwa kama zinavyofundishwa lugha nyingine za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwamba kila mmoja anapenda kusifia chake. Sasa sisi tusiposifia hiki cha kwetu, Uganda wenzetu watatupora lugha hii ya Kiswahili, Kenya watatupora lugha hii. Sasa hivi hata Rais wa Msumbiji amejidai kuhutubia kwa lugha ya Kiswahili, ataipora na kuipeleka huko.

Sasa sisi sijui tutabaki na nini. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu afikie mahali sasa akubali umuhimu wa lugha ya Taifa kama ya kwetu na kuitengenezea mpango maalum wa kuiboresha katika shule zetu za sekondari.

Mheshimiwa Spika, kwenye kitabu hiki cha mpango wa maendeleo lugha hii ina wastani wa kufaulu wa C mpaka sasa hivi. Ni aibu, ni lugha yetu ya Taifa lakini wastani wa kufaulu ni C. Sasa sijui tunaiboresha namna gani. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kutoa hiyo changamoto ya kuhakikisha kwamba lugha hii inaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, mpango wa kuboresha majengo ya Sekondari ni mzuri, lakini naomba kabisa Wizara itoe maelezo yakinifu, wananchi watahamasika kujenga shule nyingi za sekondari halafu tuje kuambiwa kwamba fedha haitoshi kuhudumia shule hizo zote. Hapo sasa ndiyo itakuwa shughuli nzito.

Kwa hiyo, ni bora mapema kuwe na uwiano na mgawanyo wa utekelezaji wa mpango huu, kila Wilaya ijenge shule ngapi, shule ngapi ambazo zitahudumiwa katika mpango huu na shule ngapi ambazo labda ziendelee kuwa ni za nguvu za wananchi wenyewe. Kwa kweli ni mpango mzuri na mimi naupongeza sana lakini unatakiwa

utolewe taarifa ya kiutekelezaji ambayo haitaleta mkanganyiko wa mambo katika maeneo ya wananchi na hasa jamii itakapoamua kuanza kujitolea kujenga majengo haya ya shule katika kuboresha elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuamua kupunguza ada za watoto wa shule. Watoto wengi wa kike kwa kuwa ada ilikuwa ni kubwa, wazazi walikuwa wanatoa kipaumbele kusomesha watoto wa kiume kuliko wa kike. Lakini kwa sababu ya kupungua kwa ada hii ninaamini watoto wengi na watoto wote katika familia watakwenda shule na kupata elimu hiyo ya sekondari. Lakini naomba kuishauri Wizara iishauri Serikali kuona uwezekano wa kufuta kabisa ada hii huko mbele kwa sababu bado kabisa tunakubaliana kwamba umaskini wa kipato katika maeneo ya Vijijini bado ni mkubwa na hivi sasa tumekuwa na sera ya uwezeshaji wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hiyo kwa asilimia mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mpaka hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi cha kikao cha leo. Alipokuwa akichangia sasa hivi Mheshimiwa Mhagama alisema wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hoja hizi jioni ya leo. Napenda kukumbusha kwamba Wizara hii imepangiwa siku mbili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atajibu hoja hizi kesho jioni sio leo. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kuna usemi kuwa: "Katika ufalme wa matumaini hakuna kipupwe." Nimesimama hapa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Elimu na Utamaduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ningependa niungane na wenzangu walionitangulia kuwaunga mkono kwa salamu zao za rambirambi pole na pongezi kwa wenzetu Waheshimiwa Wabunge waliopatwa na mikasa, misiba na vilevile pongezi wale waliopewa nyadhifa mbalimbali katika Mashirika mbalimbali ya ndani na ya nje ya nchi yetu. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kabla sijaendelea ningependa kuthibitisha kama ni kweli katika ile karatasi ya kwanza ya hotuba nadhani neno ni kuongeza na siyo kupongeza. Nazungumzia ile *quotation* ya usemi wa Rais naomba Wizara ithibitishe. Haya ni masahihisho. Siyo kupongeza ni kuongeza yaani kuboresha elimu na mazingira ya kusomeshea watoto wetu, ni vyema kuimarisha na kuongeza uwezo siyo kupongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya masahihisho hayo, ningependa niseme kwamba nimesoma vitabu vya Wizara hii, hotuba na vile vitabu vya ziada lakini ningependa kusema kwamba kama ni taarifa kwa kweli inatosha na inamsaidia sana mchangia hoja kusema lolote lile kuhusu elimu. Tunawapongeza kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watumishi wa Wizara na walimu wote kote nchini kwa kazi nzuri wanayofanya ya kulea na kuelimisha watoto wa Taifa hili. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Njombe Kaskazini, kama ningekuwa na uamuzi wangu binafsi na uwezo wa kifedha basi nguvu zote zingeelekezwa kwenye elimu, kwa sababu elimu ni ufunguo wa maisha, elimu ni nguzo ya demokrasia, elimu ni uhuru wenyewe. Bila elimu hatuwezi kufika popote pale. Kwa hiyo, tafuteni kwanza mafanikio katika elimu bora na mengine yote yatafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa niipongeze Wizara kwa kujenga mazingira mazuri ya kutolea elimu, yaani, majengo, vitabu na kadhalika wanajitahidi sana na dalili zinaonyesha kwamba wanafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa kupongeza walimu kote nchini kwa uvumilivu wao katika kufanya kazi hii nyeti na ngumu na bila kusikilizwa wakati mwingine. Naomba Mheshimiwa Waziri au mhusika asikilize kilio cha walimu. Juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo kwamba ifikapo tarehe fulani malimbikizo ya mishahara ya walimu na madai mengine yawe yamelipwa. TAMISEMI walianza kazi tarehe 21 Juni, mwaka huu, nadhani kesho watakuwa wamekamilisha kazi hiyo wao waliunda timu kwa kutafuta usahihi wa madeni ya shilingi bilioni 13. Wizara hii inatakiwa kulipa bilioni 4 kwa walimu lakini bado haijaunda timu na tarehe karibu zinakwisha. Ningependa kujua kama kweli wataweza ku-*meet the deadline.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo kama nilivyosema elimu ni ufunguo wa maisha na ukitaka kujua ubora wa Taifa lolote lile angalia elimu inayotolewa kwa watu wake. Ubora wa Taifa lolote lile hutegemea ubora wa elimu inayotolewa kwa watu wake. Je, elimu ya Tanzania inatoa aina gani ya watu au ubora watanzania ni matokeo ya ubora wa elimu inayotolewa katika nchi hii? Sina jibu kamili lakini ningependa kushauri kwamba kama lazima tuwe na Taifa bora basi lazima tujue kasi ya mabadiliko.

Mabadiliko yanakwenda kwa kasi kubwa kiasi kwamba katika maeneo kama ya elimu tusipoangalia sisi wafuasi tunaweza tukawaacha mbali kiasi kwamba tukajikuta tuko pekee yetu. Nasema hakuna *choice* lakini ni vizuri tukaangalia *speed.* Je, watu tuko nao? Silabasi inabadilika kila siku, mitaala inabadilika kila siku, *scheme of work* inabadilika kila siku baadaye watu wanakaa katikati wakisubiri mabadiliko kwa sababu kabla hawajakamilisha lile limekuja jipya. Kwa hiyo, wanakuwa watu wa kukaa katikati kusudi wasionekane wako upande wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mabadiliko haya ambayo nayapongeza sana karibu kila ukurasa nimesema pongezi, pongezi, pongezi. Ningependa kusema yale yaliyosemwa na wenzangu Maria Watondoha na Jenista Mhagama kwamba katika mazingira ya elimu, majengo na vifaa tumepiga hatua kubwa sana lakini elimu ni zaidi ya majengo na vifaa tu. Kwa hiyo, nadhani thrust ya pili iwe katika elimu yenyewe yaani mitaala, *contexts of education, scheme of work,* walimu wenyewe, vitabu vyenyewe, muda wa kusomea ualimu na sifa za wakufunzi wa ualimu. Tusipoangalia eneo hilo tunaweza tukabaki na majengo na watu wanaitwa walimu wamesimama madarasani lakini hawana kitu kichwani. Ni vizuri tukajua kwamba elimu haitapatikana kwa watoto kukaa ndani ya majengo yaliyoandikwa shule ya sekondari au shule ya msingi eti ukiingia humo utapata elimu kwa njia ya *osmosis* eti utapata elimu kwa kukaa ndani ya majengo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni lazima tuangalie yale yanayohitajika katika elimu. Kwa mfano, uwiano wa walimu, vitabu na elimu aliyonayo mwalimu. Najua kutokana na mwamko wa kujenga shule sasa imebidi tuanze kupunguza walimu katika shule zilizopo na kuwa na *crash programme* ya kuwafundisha walimu wa sekondari kwa miezi miwili na kuwagawa. Kwa kweli hawa ni kama walimu wa *UPE.* Hofu yangu ni kwamba tunaweza *extended primary schools* ambazo zitaitwa *secondary schools* kwa maana kwamba watu wanakaa pale miaka minne lakini wanatoka kama walivyoingia. Sawa, watakuwa wamepata elimu kidogo.

Mheshimiwa Waziri wakati fulani najua alitaka kuleta mapinduzi fulani akasema kwamba wale wanaopata *division four* katika mtihani wa kidato cha nne wasipewe vyeti kabisa na kwa idadi hiyo maana yake tungekuwa na *failures* zaidi ya asilimia 60. Nashukuru alisikiliza ushauri wetu na leo bado wanaendelea kupewa vyeti. Lakini nasema kwamba katika hili lazima tuangalie kwamba tunaweza kuwa na watu wengi wanamaliza *secondary schools* au *primary school* lakini hawana elimu ya miaka minne ya *secondary school* au miaka saba ya *primary school* yaani wamepita tu. Kwa hiyo, ni vizuri tukahakikisha kwamba masharti ya lazima kwa walimu na elimu inapatikana kwa kila mwaka unaotakiwa kuwa katika shule za msingi au sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo mipango hii inaweza ikatoa matunda ambayo hayakutegemewa licha ya nia nzuri. Nadhani hili ndilo lile alilolisema Mheshimiwa Leonard Shango kwamba unaweza ukawa na *education growth without education development* kwa maana ya kukosa *quality.* Lakini katika ukurasa wa 20 mpaka 24 Mheshimiwa Waziri ameelezea mikakati yake ya kuimarisha *quality* katika shule zetu. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kushauri hapa kwa sababu muda hauruhusu ni kwamba elimu haiwezi kusimamiwa kutoka Dar es Salaam. Kwa hiyo Ofisi ya Afisa Elimu wa Mkoa iimarishwe kwa maana ya kuongeza watumishi na vilevile hata *quality* au elimu ya ma-*REO* iimarishwe kusudi walingane karibu na wale wa Makao Makuu ya Wizara ili wasimamie elimu yote katika ngazi ya Mkoa na kwamba jina la *REO* libaki. Kuita Sekretariat ya Mkoa kwa maana na Afisa Elimu wa Mkoa anakuwa Sekretariet mnafanya elimu isiwe na msimamizi. Hivi sasa Afisa Elimu wa

Mkoa anasimamia Elimu ya Sekondari au elimu yote kwa kubabaisha babaisha tu lakini hana *mandate* iliyoandikwa. Napendekeza jina la *REO* libaki na cheo hiki kitabaki na asimamie elimu yote. Watumishi zaidi ya asilimia 60 katika Mkoa ni walimu leo wanabakia wanasimamiwa na Sekretariet. Hatujui nani hasa wa kumbana. Kwa kweli hili ni kosa. *(Makofi)*

Halafu pale apewe wasaidizi wa maeneo yafuatayo:- Assistant *REO Primary, Assistant REO Secondary, Assistant REO Teachers, Assistant REO* chochote kile peleka kule. Hapo utakuwa na elimu, sasa hivi wameondoa watumishi wote amebaki peke yake tu halafu ndiye anayesimamia elimu haiwezekani. Asilimia 60 au 50 ya watumishi ngazi ya Mkoani ni walimu lakini hawana *Major General* au hawana Kamanda nadhani ni vizuri hili lifafanuliwe kusudi tuweze kuimarisha elimu katika nchi yetu.

La pili, napendekeza kwamba kuweko na programu ya elimu ya ufundi kama hii vilevile nazungumza kwa Serikali. Tunafundisha elimu ya *Awareness* lakini elimu ya ufundi haina mtu. Kuna *VETA,* kuna Vyuo vikuu pale juu, hii elimu ya ufundi hapa nayo iwe na mkakati kama huu wa MMES kusudi kuwe na watu wanaoweza kuumba vitu katika nchi yetu vinginevyo mambo yatakuwa siyo kamili.

La tatu, napendekeza kwamba ule mtindo wa kuwa na Tume ya kutazama mfumo wa elimu katika nchi yetu kila baada ya miaka kumi ufufuliwe. Sasa hivi ni miaka 20 imepita hatuna Tume ya kuangalia elimu inavyokwenda katika nchi yetu. Kutokana na utandawazi na mabadiliko yanayotokea katika dunia ni vizuri Mheshimiwa Waziri kukawa na utaratibu wa kutazama kila baada ya miaka kumi kunakuwa na *review* Kamati ya kutazama dunia nzima wenzetu wanakwendaje vinginevyo itakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Somo la hesabu kwa kuwa ni msingi wa sayansi liwe ni somo la lazima kwa watoto wote kutoka *form one* mpaka *form four* na walimu wote wanaosomea ualimu lazima wafundishe hesabu, vinginevyo hatutaweza kuwa na *base* ya sayansi. Sasa hivi somo hili limefutika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba tutafute walimu kote duniani, hasa Wahindi na kuwajaza katika Vyuo, vyetu vya Ualimu kusudi wafufue somo la hesabu. Bila hesabu hatuwezi tukafika popote pale. Hili somo limekufa hivi sasa. Kiswahili kama lugha ya kufundishia kuna maneno mengi. Lakini mimi nashauri kwamba tutembee katika miguu miwili. Watoto wetu hawajui Kiingereza wala Kiswahili wala Kihehe. Sasa katika hili tusipoangalia tunaweza tukatengwa kabisa. Hivi unataka ufundishe Kiswahili tu ili utatue tatizo gani? Kwa sababu sasa hivi Kiswahili ni *automatic with or without thrust* ya Serikali. Kiswahili kitakwenda tu.

Lugha zetu za kikabila sasa zinatumika kwa matambiko tu. Kwa hiyo napendekeza Wizara iwe *clear* inataka lugha ipi itumike wapi. Hili linatakiwa uamuzi. Tuwe wazi katika hili. Vinginevyo tutatengwa na dunia. Hivi sasa Watanzania wanawakimbia watalii kwa sababu hawawezi kuongea nao katika lugha yoyote ile. Ukikaa na wenzako wa Uganda na Wakenya unakimbia. Sasa *interaction* hii katika

dunia ya utandawazi itakuwaje? Lugha ipi itakusaidia kuvua samaki. Mimi nadhani katika hilo Mheshimiwa Waziri awe *clear* na aweke msimamo. *(Makofi)*

Vilevile napendekeza tuwe na shule za mfano. Wazo kuwa tutajenga *Secondary School* zote 10,000 zenye sifa sawasawa tutaua nchi kielimu. Huwezi kuzinunulia shule zote vifaa vyote. Mtindo wa sasa wa kuwa na shule chache *Special Schools* uendelee ila tuongeze kila Mkoa, kila kanda halafu tuziimarishe ili ziwe *Blue Schools* halafu hizi zingine za kawaida tuendelee nazo kwa sababu ya sababu fulani. Lakini haiwezekani kwenda kwenye utandawazi na shule zote hizi katika hali ya umaskini tulionao. Tutakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la kimsingi ni lile ambalo wengi wamelisema nalo linahusu *linkage* kati ya Wizara na shule za msingi. Kwa kweli Waziri anasimamia taaluma, majengo ni TAMISEMI mtindo ambao mahali pengi tunapata matatizo ya nani tumwulize maswali. . Mimi huwa nashangaa maswali yakiulizwa anajibu Mheshimiwa Joseph Mungai kwa ufundi lakini ingetakiwa ajibu Pinda kwa sababu yeye ndiye anayehusika ingawa ni Serikali moja kama anavyojibu kila siku. Lakini kunyofoka kwa Muungano huu kati ya Wizara zenye utaalamu na TAMISEMI ni tatizo kubwa. Kwa kweli Ndugu Charles Keenja tunamwonea. Mabwana shamba wanakusanya kodi kule chini na hana *control* nao. Yeye yuko kama *Major General without infantry.* Natumaini mtaliangalia suala hili kama Serikali kwa lengo la kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote, ningependa kurudia tena kwamba bila elimu ya kisasa hatuwezi kufika popote pale. Kwa hiyo, *seek the education kingdom and the rest will be added into you. Thank you. (Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi nichangie hii hoja ya Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mtu yeyote atakayesema kwamba eti Wizara ya Elimu na Utamaduni haijafanya kitu. Wizara ya Elimu inastahili kupongezwa sana na imeonyesha mfano na ndiyo mfano wanaouangalia wananchi Tanzania kujua kwamba Serikali ipo inafanya kazi ni kupitia Wizara ya Elimu na Utamaduni. Kwa hiyo, mimi nampongeza sana Ndugu yangu Mheshimiwa Joseph Mungai pamoja na viongozi wote wa Wizara jinsi wanavyoiendesha. Ukiangalia mambo ya MMEM kila mahali shule zinajengwa. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wangu wa Moshi Vijijini naipongeza sana Wizara! Kwangu shule zimejaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hakuna zuri lisilokuwa na matatizo madogo madogo. Matatizo madogo madogo tunayosema ni ya kuboresha kwa sababu sasa shule za *primary* zimeishakuwa nyingi na wanafunzi wamejiandikisha kwa wingi na wengi wanafaulu sasa wataenda wapi inabidi waende shule za sekondari na wakishaenda sekondari wataenda wapi. Hilo ni jambo la kujiuliza wakishamaliza sekondari wataenda wapi? Sawa watakuwa kwenye umri wa kuajiriwa kwa sababu watakuwa na miaka 18. Ningeshauri Wizara zingine ambazo zinatakiwa kupokea wanafunzi kama hawa sasa

nazo ziwe ni Askari wa Miavuli kwa sababu wakishasoma ina maana wanatakiwa wakalime, wanatakiwa wakafanye kazi maofisini na wanatakiwa wafanye shughuli mbalimbali. Sasa zile Wizara zingine zikilala ina maana kwamba Wizara nyingine itafanya kazi na nyingine itakuwa inamwumiza mwingine. Ni sawasawa na kufunga *spare* mpya kwenye sehemu mbovu kwenye gari ile *spare* mpya nayo itakufa. Kwa hiyo, Wizara zingine kama Kilimo zijitahidi nazo kuwa Askari wa Miavuli ili hawa wanaomaliza shule wawe na mahali pa kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilihoji hapa Bungeni tarehe 1 Aprili, 2003 kuhusu mishahara ya walimu na Mheshimiwa Waziri alinijibu sina haja ya kunukuu kwa sababu ipo, kama nitatakiwa kunukuu nitalinukuu. Lakini Mheshimiwa Waziri alinijibu kwamba wamepanga kuwa ni lazima walimu waongezewe mishahara ili wafanane na walimu wanaofundisha *private schools* kwa sababu walimu wanaofundisha *private schools* ilionekana kwamba wanapata mishahara mara mbili kuliko walimu wa shule za Serikali *(Government Secondary Schools).*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri alisema kwamba wamepeleka hiyo hoja kwenye Baraza la Mawaziri, sasa nimeangalia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakuonyesha kama ile hoja imejibiwa namna gani kwenye Baraza la Mawaziri. Kwa sababu tukiongelea ile asilimia 10 ya Waziri wa Utumishi ni ya Watumishi wote Tanzania nzima lakini nilikuwa nimeomba *exceptional* kwa walimu kwa sababu kazi yao ni kubwa sana wanayoifanya toka zamani. Walimu, Madaktari na kadhalika lakini nilizungumzia walimu. Kwa hiyo, naikumbushia tena leo ahadi ya Mheshimiwa Waziri kwamba atalipeleka kwenye Baraza la Mawaziri ili ufumbuzi upatikane ili *at least* wakaribiane karibiane na hao walimu wanaofundisha shule za *Private.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie kwenye shule za sekondari. Baada ya kuona bidii ya Wizara na maelekezo yake kwamba tutengeneze au tusimamie au tuhamasishe sekondari za kata mimi nilikuwa mstari wa mbele na mimi nilikuwa Askari Mwavuli kwa upande wangu. Kwa hiyo, nataka nimweleze Mheshimiwa Waziri juzi hapa kuna mwenzetu mmoja alisema kwamba anajenga shule za sekondari nane na anataka msaada ili amalizie hizo shule za sekondari akapongezwa.

Sasa mimi nasema katika Jimbo langu la Moshi Vijijini na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Wizara kwani tayari shule za sekondari nane zimeishasajiliwa kati ya mwaka jana na mwaka huu zimesajiliwa na zina wanafunzi hivi sasa. Lakini hilo ni katika kuhamasisha na nataka ieleweke hapa kwamba tunafanya kazi Jimboni kuna *Kindi Secondary* imesajiliwa, Mheshimiwa Waziri nilichangia shilingi 400,000/= kutoka mfukoni kwangu na sementi mifuko 10 na imesajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *Somsom Secondary School* ambayo Somsom Sekondari nilichangia shilingi 200,000/= na niliomba *TANAPA* wakatusaidia shilingi milioni 16,500,000/= ile shule umeishaisajili na sasa inafanya kazi na inafundisha wanafunzi.

Kuna shule ambayo inaitwa Sungu Sekondari ya Kibosho Mashariki nayo ilikuwa inasuasua nikaidhamini mahali mkopo wa shilingi milioni 3,300,000/= na mimi mwenyewe nikachangia shilingi 200,000/= ile shule imeshasajiliwa na sasa ina wanafunzi wanasoma na imesajiliwa mwaka huu. Kuna shule ya Mabogini Sekondari ambayo nayo nimechangia mifuko 20 ya sementi na nashukuru Mungu imesajiliwa.

Kuna shule inaitwa Saoni ya Mbokomu na yenyewe nimechangia shilingi 200,000/= na sementi nayo imesajiliwa mwaka huu na imeingiza wanafunzi ni katika Jimbo la Moshi Vijijini. Kuna shule inaitwa Kisarika ya Uhuru na yenyewe imesajiliwa. Kuna shule inaitwa Okaoni sekondari Kata ya Ukaoni na yenyewe nimechangia shilingi 200,000/= na yenyewe imesajiliwa na imechukua wanafunzi mwaka huu. Kwa hiyo, siyo kama nasema shule nane bila kutaja ufafanuzi kwamba shule zenyewe ni zipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo ya ardhi Wilaya ya Moshi Vijijini. Eka moja ya ardhi kule Milimani ni shilingi zaidi ya milioni tano, kwa hiyo sehemu zingine kama Kirima Sekondari au Meli sekondari ya *Old Moshi* au shule ya *Old Moshi* Magharibi ambazo hakuna hizo sekondari za kutwa sasa hivi kumekuwa na tatizo la ardhi.

Kwa hiyo, ile ardhi kidogo iliyopo kama tutasema kwamba kuwe na ulazima wa ekari 15 au eka 10 ndipo shule iweze kusajiliwa kwa kule kwetu ni vigumu kupata. Ningeomba Wizara iangalie *position* ya ardhi kule kwetu ili tuweze kurekebisha angalau kidogo ile *amount* inayotakiwa ili mradi tu vitu vyote ambavyo vinatakiwa viweze kuenea kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hususan shule ya Meli Sekondari ambayo ipo *Old Moshi* Mashariki ambako kuna vijiji vinne vimekuja, hapa kimekuja kijiji cha *Old Moshi* Mashariki, kijiji cha Thuduni, Kidia na Kikarara. Hivyo vijiji tulisaidiana. Aidha kuna shule inaitwa Kidia Sekondari ni shule ya wazazi vilevile ambayo walipewa Dayosisi kama meneja. Kuna ekari 40 na walivyokuja kuomba kupimiwa, kijiji kikasema hapana tuna mpango na hizo eka 10 kwa hiyo mpime eka 30 ndiyo ziwe zenu, eka 10 zitabaki kwa maendeleo ya shule nyingine.

Kwa hiyo, kwa misingi hiyo wananchi wakaelezwa hivyo. Nikiwa Kanisani upande wa *Old Moshi* Mashariki kule kanisani wakatangaza kwamba kesho kutakuwa na harambee ya kujenga shule eneo hilo la eka 10 na mimi nilichukua mifuko 40 ya sementi kwenda kuwaunga mkono maana nilikuwa hapo wakati wanatangaza na tayari tumejenga madarasa matatu katika eneo hilo.

Kuna madarasa matatu katika eneo hilo na wananchi wamejitahidi sana, sasa tunaambiwa kwamba ile ardhi ina *dispute* Mheshimiwa Waziri shule inayojengwa ni ya Serikali na shule iliyopo ni ya Serikali, eka zilizokuwa zimeachwa kwenye shule nyingine ni eka 30! Ni nyingi sana! Hizo eka 10, na shule imekwishajengwa na tayari kuna wanafunzi ambao hawakupata kuendelea na shule wa eneo hilo 120 waliofaulu,

sasa wananchi wana kilio wale wanafunzi wamekaa lakini madarasa wanayaona mimi naomba Mheshimiwa Waziri utusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yapo na wenyewe wamekuja hapa, tena wameniambia nisiingie humu ndani bila maombi maalum ya Kichaga wamenipa *isale* hili *(isale ni jani la tambiko kwa mila za Kichaga)* wako huko nje wamesema nimwombe Mheshimiwa Waziri! Watoto wao hawakwenda shule.

Kwa hiyo, ninaomba hili jani kwetu walikuwa wanapelekewa machifu hapo zamani, kwa maombi maalum. Sasa nimekuja nalo hapa ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, hapa atamke kwamba wanafunzi wale waingie pale kwenye shule kwani yale madarasa yamekaa peke yake namna ile. Kwa hiyo, ni ombi kwa Wizara na Serikali. Njoo mtoto umpelekee Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, hebu kaa chini kwanza. Kwa sababu hilo dudu hatuna uhakika nalo na sisi hatulijui, naomba ukae nalo kwanza mpeane huko nje. Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, naomba ukae chini tena. Kwa sababu hili dudu ni la Utamaduni wa huko ambapo Bunge hili hawalijui. Hatujui unavyolipeleka. unalipeleka peleka kwa misingi gani. Sasa kaa nalo mkapeane kienyeji huko nje ua Ukumbi huu. Endelee na hotuba yako. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Lakini nitampa kama walivyokuwa wamenituma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine ndogo ndogo. Kuna hoja ambazo wanauliza wananchi kwamba kuna mitihani ilivuja kwenye shule za *St. Mathew* na *South Highlands* ya Mbeya na Mkuranga ikaundwa Tume. Tulikuwa tunatarajia labda katika Bajeti hii Mheshimiwa Waziri angetueleza matokeo ya ile Tume imekuwaje kwa sababu wanafunzi wamekaa hawajapata matokeo kwamba waendelee na shule au wasiendelee au ni kitu gani kinachoendelea. Ningeomba kupata ufafanuzi wakati Mheshimiwa Waziri anahimitisha hoja yake, kama hiyo Tume imemaliza kazi au bado inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachotaka kitekelezwe hapa ni kwamba kulingana na Serikali inavyokwenda na sisi Waheshimiwa Wabunge ndiyo wahamasishaji ningetegemea kwamba mwaka kesho kila Kata ya Jimbo la Moshi Vijijini iwe na shule ya sekondari ya kutwa na uwezo huo upo kwa sababu zimebaki Kata 4 tu katika Jimbo langu zingine zote tayari zinazo shule za sekondari na zimeishasajiliwa.

Ningeomba kwa bidii hiyo basi Serikali inipe moyo kwamba kweli kule Thomas Ngawaiya anajitahidi na anafanya bidii na litakuwa ni Jimbo la mfano katika Majimbo yote ya Tanzania kuweza kuonyesha kwamba kila Kata imekuwa na shule ya sekondari ya kutwa ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo baada ya kusema hayo, narudia tena kusema kwamba naomba Mheshimiwa Waziri kuhusu ile mishahara kwa kweli tuangalie walimu

ni kazi kubwa wanafanya na hilo ombi la *isale* nitamkabidhi huku nje na hayo maombi mengine ya kusaidia mtu anayejitahidi na Serikali inasema ukijitahidi na sisi tutakusaidia. Kwa hiyo mimi ninayejitahidi naomba sasa Serikali inisaidie zaidi. Nashukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote napenda kupongeza vile vile hotuba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni na mikakati yake alivyoiweka, kwa kweli inaleta matumaini makubwa. Tatizo lake tunachomuomba Mheshimiwa Waziri ni kwamba afanye kazi kama alivyopanga ili tuweze kupata matunda ya hiyo kazi. Tunaomba vile vile Bajeti inayopita basi isibadilishwe kati kati ili aweze kutekeleza majukumu aliyojiwekea kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kumpongeza kwa *African Union* kuanza kutumia Kiswahili. Hii ni hatua kubwa sana katika Taifa la kwetu. Kiswahili kinaanza kueleweka katika Afrika na naamini kitaendelea mbele na hivyo tunaweza kupata wakalimani ambao watapata kazi na ajira katika Mashirika ya Kimataifa na hivyo tutakuwa *proud* sisi Watanzania kwa sababu Kiswahili kimeanzia Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nampongeza Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru pamoja na Chifu Kunambi, kwa taarifa waliyoitoa jana katika *television* kuhusu miaka 50 ya *TANU.* Miaka 50 maana yake ni *half century* na *infact* ni *Golden Jubilee* ya tano katika nchi yetu. Historia hii ni ya muhimu na walivyoieleza wameieleza vizuri sana bila kuficha kitu chochote. Kwa hiyo, hiyo ni hongera sana. Maana yake wangeweza kuingia kigugumizi katika kueleza mambo mengine. Kwa hiyo, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, historia hii ilikuwa inafundishwa katika shule za msingi baadaye ikatoka ikapotea. Kwa misingi hiyo naomba historia hiyo iingie katika kufundisha shule za msingi na isiishie kuzungumzia kwamba watu 17 walioanza na *TANU* lakini waandikwe kwa majina. Moja Mwenyekiti ambaye alikuwa Baba wa Taifa, Marehemu Julius Nyerere, Makamu Mwenyekiti, Mzee Rupia na Katibu wao Mkuu ambaye ni baba yangu Mzee Joseph Kassella-Bantu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ni muhimu katika nchi hii kama tunavyoandika historia za David Livingstone, vita ya Majimaji, Chifu Mkwawa mpaka akachukuliwa kichwa chake kwenda Ujerumani na kikarudishwa, Chifu Mirambo na wengine wengi hata katika historia ya upande wa pili...

**MBUNGE FULANI:** Na Mheshimiwa Chifu Fundikira.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Na Fundikira ndio, hasa yule aliyejiua kwa ajili ya kuona hawezi kusimama kwenye kesi kama Chifu ya Wanyamwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo namalizia hapo na naingia sasa katika shughuli yenyewe hasa. Wazazi wenye watoto wanaosoma katika shule za msingi na

wazazi wengi katika Tanzania ni maskini. Tunaelewa hali hiyo na ndiyo maana tulipiga kelele kupata elimu bure ya shule ya msingi. Vile vile baadaye tumeendelea kupiga kelele kupata elimu ya sekondari bure kwa sababu tunajua hali halisi ya wazazi wale. Yule mama au baba mwenye mtoto wa darasa la kwanza anapofika darasa la saba umempa bure. Unapokwenda sekondari unamwambia alipe angalau kwa sababu imepunguzwa shilingi 10,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi 10,000/= kwa sisi tulivyo humu ndani haina tatizo, lakini shilingi 10,000/= kwa mtu wa kawaida, mkulima ambaye anauza mazao yake kwa bei anayopangiwa na watu. Mkulima hajapewa nafasi hata siku moja ya kupanga bei yake kwamba sasa hivi mimi napanga bei yangu ya pamba au ya kahawa ninavyotaka, wanampangia wengine. Ahesabu kwamba fedha hii nimetoa katika mkopo wa madawa, fedha hii nimelima au nimetoa ukulima faida yangu ni kiasi gani. Kwa hiyo, mtu huyu anaendelea kuwa maskini moja kwa moja. Kwa hiyo, ukimwambia shilingi 10,000/= ni tatizo. Kwa misingi hiyo naomba elimu hii iendelee kuwa ya bure mpaka sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kutengeneza shule za sekondari mimi nafikiri nilitoa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, lakini napenda kusisitiza tena kwamba kama wana kijiji au kata wanajenga shule za sekondari, wanajenga darasa moja moja kila mwaka. Kwa mfano, mwaka huu wanaweza kujenga darasa moja la *Form One* ile wanapomaliza darasa la saba wanaingia *Form One* pale pale. Mwaka kesho tena kesho kutwa wanajenga *Form Two.* Kwa hiyo, wale wa *form one* wanaingia *form two* na wengine wanaingia *form one.* Wanaendelea kwa na mtiririko huo huo mpaka wanafika *form four* kwa kujenga. Serikali itoe vile vile mabati kama ilivyo kwenye MMEM. Hivyo tutakuwa tunapata sekondari za kutosha kwa miaka minne mtoto anapotoka darasa la saba anaweza kuendelea mpaka sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikubaliani na wale ambao nusu wanabaki. Kwa sababu kama tunazungumzia haki ya mtoto ni kupata elimu basi watoto wote lazima wapate haki hiyo. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo hasa ukiangalia katika shule za Vijijini kuna darasa moja tu, yaani "A" basi afadhali kule Mjini unaweza kukuta A, B, C. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo watu wanaweza kuendelea mpaka *Form Four* bila wasi wasi. Kwa hiyo, naendelea kusisitiza kwamba ni haki ya mtoto kupata elimu na mtoto ni watoto wote bila kujali itikadi itikadi zao au nini. Kwa hiyo, wote wapate elimu mpaka *secondary school* na elimu hii iwe bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataniuliza nyumba za Walimu zitafanyikaje? Nafikiri nyumba za Walimu vile vile zinaweza kujengwa katika utaratibu huo huo wa wanakijiji au vitongoji wanajenga kama wanavyojenga shule na Serikali inatoa mabati. Ninachotaka kuongeza hapa tusitegemee kufanya *tender* za watu kwa sababu hapo kuna ulaji. Nafikiri na nashauri *VETA* itumike katika ujenzi wa shule hizi za kwetu. Hapo tunawapa vijana wetu ajira ambao waliomaliza na wale ambao bado wanasoma katika vyuo vya *VETA* na wale ambao wako vyuo vingine ambavyo viko chini ya *VETA* watakuwa wanapata *practical* kufanya kazi katika Vijiji vyao vya darasa moja moja au nyumba ya Walimu mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba watasema kuna upungufu wa Walimu baada ya kuingia watu wengi katika shule za sekondari. Kuna vijana wengi sana wanaomaliza chuo kikuu sasa hivi. Hawa vijana hawana kazi kwa hiyo ushauri wangu nilikuwa nafikiria hawa wanaweza kuwa Walimu kama vile ilivyokuwa Cuba. Cuba watu wanaotoka shuleni wanakwenda kufundisha ualimu kwanza kwa miaka mitatu.

Kwa hiyo, kwa nini na sisi tusiige mfano wa Cuba ili watoto wetu, vijana wetu wanapomaliza Chuo Kikuu wawe *compulsory* kufundisha miaka mitatu katika shule za msingi na za sekondari. Hapo tutakuwa hatuna matatizo ya Walimu, tutakuwa na Walimu kibao na watoto wetu watapata elimu wakigawiana elimu hiyo. Tukiwapa vijana wetu ajira wale wa *VETA* pamoja na wa Chuo Kikuu kwa hiyo, tutakuwa na vijana ambao wameshapata ajira kwa hiyo, hatutakuwa na walalamikaji vijana wana *hang hang* wanazunguka mitaani wakiwa na vyeti vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie katika suala la Elimu ya Watu Wazima. Hapo zamani nilipokuwa msichana kijana wa jana nilikuwa nasoma *Tabora Girls* na tulikuwa tunafundisha jioni katika mitaa ya Gongoni pale na mahali pengine mpaka *Mirambo barracks* tulikuwa tunafundisha. Tunafundisha elimu ya watu wazima kusoma na kuandika. Tulipata cheti vile vile ngao kwa ajili ya ushindi huo.

Mimi nafikiri mfano huu uigwe ili vijana wetu wa Sekondari waende wakafundishe watu wazima jioni kama *hobby.* Wawafundishe kusoma na kuandika angalau ili watu wote wajue kusoma na kuandika. Nasema hivyo kwa sababu najua liko tatizo sana kwenye uchaguzi. Mtu anataka kumchagua mtu mwingine lakini kwa sababu hajui kuandika na kusoma anatafuta mtu anampeleka kwenda kumpigia kura kule ndani anasema mfano mimi namtaka Mheshimiwa Teddy Kassella-Bantu. Lakini yule ambaye amemchukua anampigia mtu mwingine ambaye sio Teddy Kassella-Bantu. Kwa matumaini makubwa kwamba yeye anaondoka akiringa akijua kura yake amempigia mtu fulani anayemtaka. Lakini kwa sababu hajui kuandika na kusoma anakuwa ameachwa kwenye mataa. Elimu ya watu wazima ni ya muhimu hasa ya uraia. Angalau waweze kuandika na kusoma ili waweze kutumia haki yao angalau ile ya kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hayo machache naomba nizungumzie kidogo mambo ya shule na walimu. Walimu wana matatizo yao ambayo mara nyingi watu hatuyaoni sasa hivi tunazungumzia kupandisha mishahara yao ambayo ni kweli lazima wapewe mishahara hasa wasichana wanaokwenda kufundisha katika shule za mbali. Kwa sababu bila kuwapa chochote ambayo ni posho yao kwa uhakika wanakuwa kitoweo kwa watu wengine.

Kwa hiyo, naomba wapewe mishahara yao kwa wakati muafaka ili waweze kujikwamua. Kama mtu anataka kutembea na bwana basi atembee kwa kuwa anamtaka yeye sio kwa sababu anataka kushibisha tumbo lake na hapo tutakuwa tumezuia UKIMWI na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna walimu vile vile wanawatumia watoto wa shule kuwatekea maji, kutafuta kuni huko Vijijini na wengine wanawapeleka hata kulima mashamba kwa ajili ya kulipwa kwa ajili ya shule au pengine mashamba yao. Ili ni tatizo mtoto anatakiwa kusoma. Mtoto anakwenda shuleni ili akasome. Kwa hiyo, kama ni somo la kilimo basi liwe wakati wa kipindi cha kilimo tu ni liwe somo lenyewe. Sio mtu anatoka tangu asubuhi anakwenda kulima shamba la Mwalimu kwa manufaa ya Mwalimu au shamba la kulipwa kwa ajili ya manufaa ya chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Kamati za Elimu lakini tatizo lipo wale wanaoingia kwenye Kamati ya Elimu vile vile hawana uelewa zaidi. Kwa hiyo, ninafikiria au nashauri kwamba hawa wapewe semina ili waweze kujua majukumu yao kuangalia watoto wanakwenda kusoma shule wanapomaliza darasa la saba au la kumi na mbili watakuwa na elimu inayotakiwa ya darasa hilo na kiwango hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuhitimisha kwamba tukisomesha watoto wetu mpaka sekondari bure tutakuwa na raia wazuri wenye elimu wanaoelewa na wanao upeo. Hawa vijana watakuwa miaka 18 *roughly* au 19 kwa hiyo, wanaweza kujiajiri wenyewe vizuri na wanaweza hata kama kuolewa au kuoa watajua jinsi ya kukaa katika mikakati ya ndoa na vile vile kulea watoto wao na kuzaa kwa mpango kwa sababu wanaelewa. Kuliko mtoto anapokwenda miaka 12 unamwacha au 14 unamwacha ameshamaliza darasa la saba hajui anakokwenda. Kwa hiyo, hata kama atafanya biashara, hata kama ile ya kupiga debe kwa ajili ya wasafiri atafanya katika utaalamu kwa sababu ana elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano atafanya kama vile Bora ilivyokuwepo hapo zamani anaandika Bora kiatu hiki ni shilingi 199/= na hiki ni shilingi 299/=. Sasa wewe unapokwenda kununua ukiona 199/= hujui kama ni shilingi 200/= unaamini kwamba una shilingi 100 na 100 nyingine itabaki. Lakini unapotoa shilingi 200/= unarudishiwa shilingi moja ndiyo unashangaa alah, kumbe ilikuwa 200/=.

Kwa hiyo, *in a trick way* wataweza kufanya biashara zao vizuri na wakajitegemea vizuri. Vile vile hata kama wanapika chapati unaweza kufanya mfuko wa unga wa ngano unahakikisha kwamba unatoa chapati 20. Kwa mfano ukitengeneza chapati 20 pana katika kupika wengine wanaweza kusema zinakuwa nyepesi sana wanasema jamani mbona umetutengenezea chapati nyepesi. Kwa hiyo, kesho unafanya vile vile chapati 20 lakini unahakikisha kwamba zile chapati zinakuwa ndogo na ni nene na nzito. Kwa hiyo, mtu anaona kwamba hii safi. Kwa hiyo, unacheza kwa sababu ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupongeza hiyo hotuba na naomba afanye kama alivyo mtani wangu.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii jioni hii na mimi kuchangia machache kuhusu hotuba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa takwimu nyingi na ma-*graph* ambayo yanapendeza kuona maendeleo na mafanikio ya elimu. Pili, nampongeza kwa kutembelea nchi nzima kwa kuangalia mpango mzima wa MMEM. Kwa hili nampongeza sana awe na moyo kama huu na Mawaziri wengine waige mfano kama huu kutembelea sekta zao wakati ambapo inabidi kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana vizuri na Kamati ya Huduma za Jamii katika wakati wote wa kazi za kujadili Bajeti na wakati wa ziara za Kamati. Kwa kweli kwa hili tunampongeza sana na aongeze bidii hii ili na wale watendaji wao wapate moyo wa kuhakikisha kuwa wanafanya kazi kwa manufaa ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu zaidi utalenga katika taasisi ya Mabaraza ya Elimu. Ukweli usiofichika kuwa Mabaraza yetu au taasisi zetu zinafanya kazi nzuri nchini. Ipo haja ya kuangaliwa vizuri sana hizi taasisi na Mabaraza kulingana na wakati tulionao wa sayansi na teknolojia. Mabaraza yetu kwa kweli hivi sasa yanafanya kazi katika mazingira magumu mno. Ukiangalia kama Baraza la Mitihani. Baraza la Mitihani ni baraza ambalo linafanya kazi ngumu na ya ufanisi katika nchi hii na ndio kioo cha jamii ya Watanzania katika elimu. Lakini ukiangalia baraza hili ukweli lina matatizo mengi ambayo inayoyakabili hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo makubwa yanayowakabili hivi sasa ni ukosefu wa fedha. Wanakabiliwa na ukosefu wa fedha na pesa hizi ni kwa ajili zaidi usafirishaji wa mitihani kufikisha kwenye vituo vya mitihani. Kwa hiyo, ipo haja kuangalia mtizamo huu kuhakikisha kuwa Baraza la Mitihani linapatiwa fedha kuhakikisha kuwa ile mitihani inafika kwa wakati katika vituo ambavyo vinakubalika. Halafu wakati huo huo linafanya kazi katika mazingira magumu. Mashine walizonazo ni chache lakini hata hivyo wanafanyakazi mwaka mzima kuchapisha mitihani ya ngazi tofauti yaani kuanzia darasa la 6, *Form Four, Form Six* na Vyuo vya Ualimu. Wanafanyakazi takribani mwaka mzima bila ya kupumzika. Ipo haja kupatiwa hata nyenzo za kuhakikisha kuwa kazi yao inafanikiwa ipasavyo. Hili sio kama nazungumzia kwa kuliona hasa, kwa kuwa tatizo lipo katika Baraza la Mitihani kuhakikisha kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu ambayo hayana vitendea kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linaikabili katika majengo yale au taasisi ile ni kuhakikisha kuwa wanapatiwa majengo ambayo yanakidhi haja katika wakati huu, kwa sababu majengo waliyonayo hivi sasa kwanza ni machache, halafu hayaendi na wakati tulionao hivi sasa kwa sababu wanatumia vyumba ambavyo havina hewa ya kutosha au mazingira ambayo si ya kuridhisha kwa kufanyia kazi kama kuchapisha au kutumia makaratasi wakati huu wote waliomo mle ndani katika uchapishaji wa mitihani. Kwa hiyo, ipo haja tuliangalie tatizo kama hili ili tuhakikishe kuwa tunawapa au tunawafanyia mazingira mazuri tuhakikishe kuwa wanafanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Halafu suala lingine la Baraza la Mitihani kuwa hivi sasa matatizo ya uvujaji wa mitihani yamedhibitiwa kweli kweli na hakuna uvujaji ambao unatokezea hivi sasa. Lakini kuna tatizo ambalo hivi sasa linaweza likajitokeza la usimamizi wa mitihani. Askari Polisi baada ya kusimamia mitihani wanatumia kama ile nafasi kama ni wakaguzi wa mitihani. Kwa hiyo, ipo haja hili tuliangalie katika baadhi ya vituo sio Tanzania nzima. Kuna baadhi ya sehemu ambayo tatizo hili ni kubwa. Wanaangalia kama ni wakaguzi na wao wasimamizi wa mitihani. Wao ni wasimamizi wa mazingira au kuhakikisha kuwa usalama wa vituo upo lakini sio kusimamia mtihani na kuathiri wanafunzi kisailojia wakati ambapo wanasimamiwa na askari.

Kwa hiyo, ipo haja suala hili liangaliwe kuwa Askari Polisi ni watu ambao wanasimamia usalama wa mazingira au wahakikishe kuwa mitihani inapolala wao ndio wanashughulikia kuhakikisha kuwa usalama wa mahali hapo upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niache hapo niingilie katika taasisi nyingine Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Hii ni taasisi kwa kweli ni ukombozi wa watu wazima wale ambao walikosa elimu hapo mwanzo. Lakini taasisi hii nayo inafanya kazi katika mazingira ambayo hayaridhishi. Ukiiangalia ile taasisi ni taasisi lakini taasisi ambayo hivi sasa inafanya kazi zake karne iliyopita. Nafikiri karne hata siijui mwaka gani unaweza ukasema. Hivi sasa hawana hata kitendea kazi ambacho kinalingana na wakati tuliokuwa nao yaani hawana kompyuta, hawana aina yoyote ambayo inalingana na wakati tulionao hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ipo haja taasisi hii kuangaliwa kwa mtazamo wote yaani hivi sasa mafaili wanaweka katika *shelves* au kwenye makabati au meza. Utashangaa yaani hakuna utaratibu uliowekwa makusudi wa kuhakikisha wanakwenda na wakati. Ni tatizo kubwa sana ambalo wanalo. Kisha mashine walizonazo ni chache vile vile wanachapa vitabu lakini kwa mazingira yaliyo magumu mno utadhani *phrase* ya watu wazima. Kwa hiyo, ipo haja Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla ili waone wale kwa kweli wana hali ngumu na wana mazingira magumu sana ya utendaji wa kazi katika kuhakikisha watu wazima wanapata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu Baraza la Kiswahili la Taifa. Baraza hilo limetengewa fedha nafikiri inatosha kwa wakati huu tulionao kama wataipata kwa wakati na itatumika ipasavyo. Kwa kweli Baraza hili linafanya kazi nzuri ya usanifu wa Kiswahili na usanifu wa maneno, misamiati inayoingia ya sayansi na teknolojia katika Wizara inasaidia sana kuitafsiri na kisha inatoa ushauri wa matumizi mazuri kwa walengwa wote nchini na wanaoingia nchini na taasisi ambazo zinatumia lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini liko tatizo katika taasisi hii au katika Baraza hili nalo linakosa fedha kama alivyosema Mheshimiwa mwenyewe Waziri. Fedha hazitoshi kwa kuhakikisha kufanyia utafiti. Lugha lazima ufanye utafiti na lugha ya Kiswahili haikuja tu hivi hivi lazima ilifanyiwa utafiti, utafiti uliotosha na ikawekwa lugha ya Kiswahili kufanya hivyo. Kwa hiyo, huwezi kukaa kwenye meza au kwenye darasa ukahakikisha kuwa unaisanifu lugha ya Kiswahili. Si kweli kwa sababu utaletewa neno

moja leo utalisanifu leo, lakini mengine ambayo yanatumika sehemu tofauti huwezi kuyapata. Kwa hiyo, lazima uhakikishe kuwa unafanyia utafiti wa hali ya juu au utafiti wa kutosha kuhakikisha kuwa wanafanya kazi ambayo inapaswa kuhakikisha kuwa inaeneza mafanikio na inatumia Watanzania lugha ambayo itakuwa ni sanifu.

Halafu vile vile njia ambayo hivi sasa tunaeneza Kiswahili kwa kweli ni chache ukihakikisha kuwa kuna Vijiji vingine lugha ya Kiswahili haiko kabisa wanatumia mpaka leo lugha za lahaja zao tu au vijilugha ambavyo vimo katika mazingira yao. Kwa hivyo, ipo haja kuwa lazima lugha ya Kiswahili ienee. Sio kuenea Kimataifa tu lakini hata hii Tanzania yenyewe inaonyesha bado lugha ya Kiswahili haijafika ipasavyo. Kwa hivyo, ipo haja kuhakikisha kuwa kazi hii baraza hili linafanya kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inafika.

Halafu vile vile matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu hamna Tanzania. Katika vyombo vya habari hakuna lugha sanifu. Mtangazaji anakaa na kusema kuwa tunawatangazia mpira. Hii ni lugha sijui inatoka wapi? Si lugha sanifu ambayo inatumika katika lugha yetu ya Kiswahili. Waheshimiwa Wabunge humu humu kwenye Bunge mtu anasema "dalasa." Hii kweli ni lugha ya Kiswahili! Lazima tuhakikishe kuwa tunakuwa na matumizi mazuri ya lugha ya Kiswahili. Kama mgeni anasikiliza lugha hiyo ya "dalasa," "ukulasa," kweli hatapata lugha ya Kiswahili sanifu. Hiyo sio kweli lakini lazima tuhakikishe hata sisi Wabunge tunatumia lugha nzuri na sanifu ambayo imesanifiwa na Baraza la Kiswahili sio yale maneno ya kuokota tu tunaleta Bungeni tunawapa wananchi wanayatumia. Lazima tuwe na lugha ambayo kwa kweli inakidhi haja na tunapokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kwa kusema kuwa lazima waandishi hata Wabunge wafanyiwe semina. Wasifanyiwe semina za mambo mengine tuna lugha ya Kiswahili matumizi yake yafanywe. Kwa hiyo, lazima tufanyiwe semina na waandishi wa habari, watangazaji wawekewe mikakati kuhakikisha wanatumia lugha nzuri. Kuna lugha ambazo kwa kweli lazima uzitoe, wasisomeshwe lugha sanifu tu kuitumia lazima utumie na nyenzo zake. Kwa mfano, kama unatumia alama hii unatumia kipasio cha aina gani, kiyayusho cha aina gani, kimadende cha aina gani lazima tuhakikishe kuwa lugha hii inatumika.

Kwa hiyo, mambo haya lazima wale Walimu wetu wanapowasomesha, wawafundishe lugha kama hizi kuhakikisha kuwa lugha hii inatoka wapi. Hii imeanzia wapi au inatokana na lahaja gani waliotumia walianzia wapi. Kwa hiyo, lazima tuwe na suala kama hili tuhakikishe kuwa lugha inakuwa nzuri na sanifu hapa hapa nchini halafu tukiipeleka huko nje ya Mataifa inaboreshwa tu lakini kwanza wenyewe tuwe na matumizi mazuri. Unamwongoza mtalii unamkuta mtalii anamwambia "jambo"? Mswahili anamwambia Mzungu: "jambo," sasa huyo mzungu aitikie vipi? Badala ya kumwambia "hujambo," yeye anamwambia "jambo," yaani unampotosha anachukua lile neno ambalo si zuri kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee katika suala hilo kuhusu Chuo cha Sanaa Bagamoyo. Kwa kweli hiki chuo ni kizuri na kinatoa wasanii wazuri tu lakini kwa kweli

kina matatizo hivi sasa lazima tuhakikishe kuwa Mheshimiwa Waziri anakiangalia kwa jicho la huruma kwa sababu lile jengo ambalo limeungua kweli wametenga fedha za kutosha shilingi milioni 886 si fedha ndogo ambazo zinaweza zikakidhi haja. Kwa hiyo, lazima tufanye ukarabati yale majengo ambayo yameungua na tuhakikishe kuwa tunaongeza na madarasa mengine ambayo hayatoshi kwa hiyo, tuhakikishe kuwa tunayaongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho ni Vyuo vya Walimu. Katika ziara ambayo tumeifanya katika Kamati ya Huduma za Jamii tuliona baadhi ya Vyuo vya Ualimu na matatizo yao ya Vyuo vya Ualimu ni yale yale ya kuhakikisha kuwa wana uchache wa madarasa, mabweni na fedha haitoshi ambayo wanapewa kufanya mazoezi nyenzo au fedha ya kufanyia mazoezi au kufundishia katika wakati wa *field.* Kwa hiyo, ipo haja Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kuwa anawaona katika suala hili. Walipendekeza na wao katika vyuo vyao vya ualimu wahakikishe kuwa wanafanyiwa kama mpango mzima wa MMEM kuhakikisha kuwa na wao wanafuata taratibu kama hizi ili kuhakikisha kuwa Vyuo vya Ualimu vinatanua ile taaluma yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Hoja hii mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Lakini kuna maeneo kidogo ya kuboresha boresha. Kwanza sisi wa Mtwara Vijijini tunaishukuru Serikali kupitia Wizara hii. Kwa kweli shule zinapendeza, hapa tunachoomba ni kutekeleza ile ahadi ya Waziri Mkuu ya kumaliza kabisa madeni ya Walimu na Walimu wapya kutowacheleweshea mishahara yao na maslahi yao na mengine yanayoambatana na hayo ili waweze kutoa huduma ya kuwafundisha vijana wetu kulingana na madarasa yalivyo kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi watu wa Mtwara tulikaa kabisa Mtwara Vijijini siku moja tukajiuliza hili duara la umaskini *(vicioul circle of poverty).* Hili kwetu sisi mbona limetuelemea imekuwa kuwaje hili. Katika kulichambua tukagundua kuna kaufa kwenye elimu kwamba haka kadudu ka umaskini kameingilia hapa kwenye *lack of education.* Kwa kukosa elimu tukagundua uzalishaji wetu unakuwa dhaifu, kwa kukosa elimu vijana wengi wanakimbia kule kuhamia Dar es Salaam tunapunguza nguvu kazi ya kuzalisha. Kwa sababu *productivity* inakuwa ndogo tunakosa uwezo wa kiuchumi wa kuwasomesha vijana wetu, tunakosa uwezo wa kiuchumi kujenga nyumba bora na kuhudumia huduma za afya kwenye familia na mambo mengi tu. Lakini kadudu haka kameingilia kwenye mwanya wa elimu. Tukakubaliana kabisa sasa tumkomeshe kuziba mwanya huu kwa kujenga shule za sekondari, kila kata shule ya sekondari moja ili vijana wasome Wamachinga wasiwe tena wanazagaazagaa iwe ndiyo mwisho wale wale. Sasa hivi tayari tumeshakwisha kufaulu kujenga shule nne.

**WABUNGE FULANI:** Hongera !!!

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Nanyamba, Nanguruwe, Misimbati na Ziwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, nilikwenda kumwonyesha shule moja ya Nanguruwe akaahidi atatoa msaada mpaka leo hatujamwona. Bwana wewe vipi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, tunakuomba ule mpango wa kuongeza mikondo basi uanzie Nanguruwe, Nanyamba, Msimbati na Ziwani kama ulivyopanga kwamba kutakuwa na mpango wa kuongeza mikondo ili kupanua sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo ndizo shule zinazofundisha sasa hivi, lakini tunajenga Kitaya, Mahurunga, Libobe, Mpapura, Nnima, Njengwa, Nitekela, Nantumbuka, Mayanga, Bihimba, hatuna mchezo siku hizi. Sasa tunaiomba Serikali kwa mpango huu wa kusaidia ujenzi wa Shule za Sekondari watukimbilie kule Mtwara, waanze Mtwara. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi maalum ni kwamba, tunaomba kwa sababu mwenzetu Mheshimiwa Thomas Ngawaiya anasema kila Kata wanazo, sisi kila Kata ndiyo tunaanza kujenga sasa. Kwa hiyo, tunaomba msaada safari hii habari hizi zianzie huku Kusini huku kama kawaida yangu ninavyowaelezeni. Ianzie Kusini huku, huku Kaskazini muonyeshe mgongo. Mjifunze kuonyesha mgongo, muanze kuonyesha huku, kibra yenu ya elimu sasa iwe huku. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msaada huu uende pamoja na Walimu na vifaa ili shughuli zitakapoanza basi isiwe kuna kikwazo. Mfano, kunakuwa na shule, lakini hakuna walimu. Hii iende pamoja na walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nilihudhuria mkutano wa Tarafa moja ya Kitaya uliokuwa unazungumzia mambo ya elimu tu. Yaliyojitokeza na niliyotumwa nije nieleze hapa ili Serikali isikie na ikiwezekana Mheshimiwa Rais, Benjamin William Mkapa ayasikie ndiyo haya ninayotaka kusema, kwamba: "Hivi huyu Mheshimiwa Mkapa sisi tumpe nini? Kujenga mashule mazuri namna hii! Bwana huyu barabara safi, zahanati kukarabati, nasikia anataka kuanza mpango mwingine wa Sekondari. Huyu bwana huyu bahashishi ipi? Tunakutuma upitie Wizara ya Elimu na Utamaduni, habari hizi zimfikie Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwamba tunampongeza, lakini ajue kwamba alikuwa ana hiari kuchukua fomu ya kugombea urais ama kuacha. Madhali amechukua, hakuwa na hiari ya sisi kumpa au kutompa, hiari ilihamia kwetu. Kwa hiyo, tukaamua kumpa. Alipopata hiari ikahamia kwake kufanya vizuri au vibaya, lakini amefanya vizuri. Sasa hiari imehamia kwetu ni bahashishi gani tumpe? Hana nafasi ya kuchagua zawadi ya kumpa." *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sema.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Wananiambia niseme. “Tunaamua sisi.” “Enhee, nikasemeje?” Wakasema: “Hatuvunji Katiba, aah, tunaomba tumpe bahashishi bwana huyu kumwongezea hata kama miaka mitatu ili amalizie malizie mambo haya.” Maana kunoga huko kijijini ukienda. “Kamwambie hivyo.” Nikasema: “Jamani eeh, utumwa huu mimi nitapeleka, lakini kuna mambo yatakayojitokeza, kwanza kuna midume inagombea urais, itanitafuna mimi na itanigawanya gawanya wala haitanielewa, lakini nitasema.” Hilo moja. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini la pili, habari hizi akisikia mwenyewe anagoma kweli, kumwambia kumwongezea muda anagoma. Wakasema: “Haya, kama huwezi tupe nafasi tumpeleke mwingine asiyeogopa kugoma. Nikasema: “Eeh, kama ndiyo hivyo nitaenda kusema.” Kwa hiyo, wanaomba wa Mtwara Vijijini kumpa bahshishi ya kumwongezea angalau miaka mitatu, siyo kuvunja Katiba, hapana. Katiba iendelee miaka kumi kumi, ila hii ni bahashishi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakasema: “sasa kama haiwezekani waeleze wale watakaogombea Urais kama wako Bungeni au nje sisi hatujui, wafuate bwana nyayo hizi, wasije wakapata wakaja kuharibu utamu huu. Sisi Watanzania sasa tunajua kwamba inawezekana Watanzania wenyewe wakajenga mashule yao wenyewe bila kutegemea wafadhili. Inawezekana Watanzania wakajenga majosho, wakajenga barabara kwa kutumia fedha zao, sasa wasitudanganye tena. Huyo Rais atakayekuja hatutamuelewa akitudanganya “ooh tuna ukata, utarafa, hakuna!” Kwa hiyo, wafuate nyayo za Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuombe kumwongezea, kama haiwezekani huyo bwana atakayekuwepo tafadhali, maana hatutakuwa na uwezo wa kumueleza hapo baadaye kwa sababu atakuwa mkubwa. Tunamueleza sasa hivi kwamba, bwana wewe hatutakuelewa ukitueleza ukata, utarafa hatukuelewi, mwenzako huyu mbona ukata haupo! Mashule anajenga, anajenga barabara na kadhalika. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwaambia kwamba mimi nitafikisha ujumbe huu lakini aah, midume inayotaka kugombea hiyo itaniletea uhasama. Tafadhali haya si yangu, ni ya wapigakura wangu. Kama nimeenda vibaya nimewaudhi watu tafadhali nisiadhibiwe, mimi nimetumwa na Mbunge ni mshenga. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, lakini Mheshimiwa Waziri, Nanguruwe bwana wanakusubiri ahadi ile. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii. Awali ya yote napenda kumpongeza sana tena sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na wataalam wake kwa namna wanavyoandaa hotuba pamoja na kutusaidia kwa takwimu mbalimbali. Kwa kweli Wizara hii inapofika wakati wake wa kusoma hoja huwa najisikia vizuri sana, kwa sababu kwenye Hotuba ya Wizara huwa kuna kila aina ya takwimu ambayo inakuwezesha kwenda kujibu maswali huko Jimboni. Kwa kweli nawapongeza sana tena sana. *(Makofi)*

Pili, napenda nitoe salaam za rambirambi kwa ndugu yetu aliyetutangulia mbele ya haki, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli katika hoja hii kulikuwa hakuna haja ya kuchangia kwa sababu kila kitu kinajieleza. Lakini haya majibu ambayo yametolewa kwenye takwimu na hoja yenyewe ni majibu ya jumla, huwa kuna matatizo yale yanayotokea kutoka huko kwetu kwenye Majimbo. Kwa hiyo, ndiyo tunayokuja kukuelezeeni. Nakuomba sana tena sana Mheshimiwa Waziri usikilize kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita katika Kitengo cha Ukaguzi. Jambo la ukaguzi kama alivyolielezea Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati inayohusika, ndugu yetu Mheshimiwa Omar Kwaangw', linaeleweka vizuri na imeeleweka siwezi nikarudia, lakini kitengo hiki ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ninapokwenda kuzungumza na Afisa Ukaguzi wa Wilaya nikiingia ofisini kwake kwa kweli huwa napatwa na mshangao mkubwa sana! Unapoingia pale kwanza hakuna kiti cha kukalia mgeni, unasaini ukiwa umesimama na unapotaka kupata taarifa kutoka kwa yule Afisa Mkaguzi unamwuliza maswali kama Mwandishi wa Habari. Hiyo ndiyo Ofisi ya Mkaguzi wa Wilaya. Ofisi yenyewe ina kabati pamoja na meza, samahani kwa kulisema hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo hali halisi. Ni kwamba, ukifika pale ofisini kabati pamoja na meza ni kama vya mtengeneza *chips.* Napenda niliseme hili tu.

Kwa hiyo, naomba kwa namna ya pekee kabisa kwanza tuwawezeshe hawa Wakaguzi wa kila Wilaya tuwapelekee samani ili nao wajisikie kwamba wana ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba, mnapotaka kutatua matatizo yoyote yale yanayohusu kila Sekta hebu fuatilia jiografia ya kila eneo. Huwezi ukampa pikipiki mtu anayeishi Biharamulo ambaye unajua kabisa kwa uhakika kwamba Wilaya ya Biharamulo imezungukwa na mapori na wanyama wakali na ujambazi wa hali ya juu pamoja na wakimbizi. Naomba nitoe mfano, kutoka Makao Makuu ya Wilaya kuna Shule moja ya Msingi inaitwa Kinsabe katika Kata ya Buseresere. Kutoka Makao Makuu ni kilometa 140 na humu katikati mtu anapita ndani ya pori, kuna ujambazi wa kila aina. Huyu unampa pikipiki, hivi unamtakia kheri kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingine ni Shule ya Mavota, kutoka Makao Makuu ni kilometa 103, humo katikati unapita katikati ya pori, hakuna barabara unakwenda kama unakwenda kuwinda. Huyu unamwambia akakague!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara itatue matatizo kwa kufuata jiografia na mazingira ya hali halisi. Tusije tukachukulia kwamba majibu ya matatizo yote yawe ni kama tuliyoletewa na wahisani kwamba mnapaswa mbinafsishe, mnapaswa mpunguze

watumishi ndiyo tuwape misaada. Tunatakiwa kwa namna ya pekee tufuate hali halisi ya mazingira ili tuweze kutatua matatizo. Huwezi kumpa mtu pikipiki anayeishi Biharamulo na ukaja ukampa mtu labda anayeishi Dar es Salaam ile ile pikipiki! Kwa kweli utakuwa unafanya kosa ambalo hatuwezi tukalilinganisha na kitu chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu Walimu. Kuna tatizo kubwa sana la Walimu. Wizara inapotaka kufungua shule inatoa masharti kwa wale waliojenga, kwa wananchi kwamba ili shule hiyo tuisajili mnatakiwa mtimize masharti yafuatayo na wananchi kwa nguvu zao, kwa muda wao wanayatimiza na shule inasajiliwa na inafunguliwa. Lakini Serikali mbona hamtimizi masharti yenu kuleta Walimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano mwingine. Kuna Shule moja ya Nyakabhura ambayo ina *Form One* mpaka *Form Two.* Huu ni mwaka wa pili, ina mikondo minne, lakini mpaka leo ina Walimu wawili tu!

**WABUNGE FULANI:** Eeeh, pole sana.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Leo unasema kwamba tunawaandaa wanafunzi ili waje wajijengee maisha yao ya baadaye na waje wapate namna ya kulipa lile deni ambalo Mheshimiwa Basil Mramba, alilisema kwamba lazima tukopeshe ili baadaye deni lije lilipwe na wajukuu zetu. Kweli huku ndiko kumuandaa mwananchi ili baadaye aje apate uwezo wa namna ya kupata hela ya kulipa? Walimu wawili kwa miaka miwili kwa wanafunzi wote hao! Naomba wakati tutakapotoka hapa nifike nakuta kuna Walimu wa kutosha, upungufu wa Walimu ni Walimu 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingine ni Shule ya *Biharamulo Secondary.* Shule hii ina mikondo minane, kwa kweli ni jambo la ajabu kidogo! Ina mikondo nane, ina wanafunzi 368, ina walimu watano. Ni jambo la kusikitisha. Bahati nzuri nimeshajitahidi sana kuwasiliana na uongozi wa Wizara, nafikiri ambao nimeshazungumza nao wanalielewa hili. Kama hawalielewi, basi hawataki kuelewa, lakini naomba walielewe. Naomba niondoke na walimu 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingine ni Shule ya Kagango ambayo iko katika kitovu cha Mji, ndiyo Shule ya Sekondari ambayo inategemewa karibu na Wilaya nzima. Nafikiri ina miaka zaidi ya 15, lakini mpaka sasa hivi hatujapata mwalimu yeyote anayefundisha hesabu. Ile ni shule ya mchepuo wa biashara, hatuna walimu wa biashara hata mmoja kwa shule nzima!

**WABUNGE FULANI:** Pole sana.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Waziri, kitu ambacho naomba ni kwamba, kwa kweli kadri ninavyokufahamu wewe ni msikivu, wewe ni mtu makini, wewe ni mwangalifu wa hali ya juu, siku zote tumekuwa tukija kukukimbilia na unatusaidia kwa masuala haya, naomba unisaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa tu kuchangia ni kuhusu ubora wa mitaala au aina ya mitaala. Kabla sijachangia kwa haraka haraka naomba niseme *quotation* moja inayosema hivi: *"The best educated human being is the one who understands most about the life in which he is placed."* Hii mitaala ambayo tunaendelea nayo tangu nilipomaliza darasa la saba, nikaenda sekondari, kwa upande wangu naona haimwandai kabisa mwanafunzi au mtu yeyote kwenda kujitegemea huko aendako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mke wangu ni mwalimu. Siku moja nilikwenda nyumbani nikakuta kuna redio ambayo imetengenezwa kwa udongo wa mfinyanzi. Sasa nilipofika pale nyumbani nikamwuliza: "Na hii kitu?" Akasema: "Hizi ni stadi za kazi." Kweli kabisa hili somo la Stadi za Kazi unaweza ukamwandaa mwanafunzi kwenda huko aendako atakapomaliza darasa la saba kwa kutengeneza redio ya udongo wa mfinyanzi na kuweka *aerial* ya nyasi eti unamwandaa ili ajiandae baadaye! Hili ni jambo la ajabu kabisa! Mimi sikuelewa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, safari nyingine nikaona ni kitu cha ajabu wanajifunza namna ya kutengeneza kamba ya kufunga mbuzi, eti hiyo ni stadi za kazi! Tunataka stadi za kazi zimwelekeze katika soko atakapokuwa anatengeneza, maana huwezi ukauza redio ya udongo wa mfinyanzi, utamuuzia nani? Kama ni kamba ile ya mbuzi mtauziana nyinyi kwa ninyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, tutafute walimu ambao tutawapeleka hata nchi zilizoendelea katika masuala ya kazi ya mikono kama China au kama India, ili wakajifunze watengeneze vile vitu ambavyo vitawasaidia huko waendako. Lakini kwa mtaji huu na kwa utaratibu huu mimi nakwambia sote tutakuwa tunabanana kwenye Wizara mbalimbali, kwenye Idara mbalimbali na haya maneno ya kisiasa tunayosema hebu mjiajiri tu, mjiajiri sekta binafsi, wengi wataendelea kubanana hapo Dar es Salaam kwa kuuza soksi, ndiyo kazi maana hujamwandaa hata sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitabu kimoja kinaitwa Mashujaa wa Afrika, nilisoma kulikuwa na malikia mmoja anaitwa Nzinga Mbande wa Matamba. Alipokwenda kuwatembelea Wareno pale Msumbiji, walikataa kumpa kiti. Walipokataa kumpa kiti akamvuta mwanamume mmojawapo aliyekuwa kati ya wale waliokuwa wamembeba akamkalia ndiyo akaanza kuzungumza nao. Hilo somo nafahamu linafundisha ushujaa, linafundisha ujeuri, lakini sasa wanasema kwa shujaa au mjeuri huenda kilio. Kama wewe unafundisha ujeuri kwa utaratibu huo, kweli huko uendako utakuwa shujaa ama utakuwa jeuri? Je, utaishi kwa ujeuri au utaishi kwa ushujaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa hapa ni kwamba, tuhakikishe kwa namna ya pekee kabisa somo hilo la stadi za kazi tunalichukulia maanani maana ndilo somo litakalomsaidia huko anakokwenda. Haya masomo mengine pamoja na hesabu na kujua kusoma na kuandika, hayo yatamsaidia kwa kufanya mengine, lakini namna ya kutengeneza kujitafutia maisha ya kila siku haitawezekana. Tutaendelea kubanana huko

tunakokwenda. Tukimaliza tu Elimu ya Msingi, Dar es Salaam, Arusha, kila Mji tutakwenda na hapa tunaandaa watu ambao huko tuendako ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona niwataje watu wengi ili wajiandae na nikiangalia humu naona wengine hawapo. Sasa baada ya Mheshimiwa Anatory Choya atafuata Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Lekule Laizer na Mheshimiwa Semindu Pawa. Nadhani hao pia waendelee kujiandaa. Sasa namwita Mheshimiwa Raphael Mlolwa.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru sana kwa kuniona na kunitaja kwamba sasa nizungumze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi za dhati sana kwa Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu wake, Katibu Mkuu, Mama Mwantumu Malale, viongozi na watendaji wote wa sekta ya elimu kwa mambo ambayo wanafanya. Kwa kweli sekta ya elimu ni moja ya sekta ambazo zinafanya vizuri. Ni *one of the centres of excellency* katika Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana kwa kuja na kitu kama hiki kilichopo katika hotuba hii kwani kinatoa matumaini makubwa kwa Watanzania wote. Nashangaa sana wale wote ambao huwa wanahoji kwamba hii Serikali ya CCM inafanya nini! Nadhani hili ni jawabu mojawapo kwamba nini CCM inafanya na kwa kutumia fursa hii, napenda kabisa kuwahakikishia Watanzania wote na hasa wanachama wa CCM kwamba watembee kifua mbele kwa sababu Chama chao na Serikali yao vinafanya mambo mazuri kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto moja au mbili katika sekta hii ambazo nashauri Mheshimiwa Joseph Mungai na watendaji wengine wa sekta hii waweze kuzizingatia. Mojawapo na ambayo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameitaja ni jinsi ya kutoa elimu bora itakayotuwezesha sisi Watanzania tuweze kushindana katika soko la ajira la ulimwengu huu wa utandawazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya vigezo muhimu vya elimu hiyo bora ni matumizi ya kompyuta au teknolojia ya mawasiliano kwa ujumla wake. Ilivyokuwa ni kwamba, kwa ujumla wake shule nyingi hapa Tanzania ziko vijijini ambako umeme haupo. Lakini elimu bora sasa hivi katika hii karne ya 21 ya Sayansi na Teknolojia ni lazima kuanza matumizi ya kompyuta kuanzia Elimu ya Msingi. Hii imefanikiwa kwa kiasi fulani katika shule zilizopo katika Miji ambako umeme upo. Kwa hiyo, ninaishauri

sana Serikali ione uwezekano wa kuja na programu ya kusambaza umeme huko vijijini ili shule zote ziwe na elimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyonukuu Ibara moja hapa ya Katiba katika hotuba yake ukurasa wa 11, haya ni malengo maalum ya Elimu ya Sekondari, katika kifungu (d) amesema: "Kutoa Elimu ya Sekondari kwa usawa kwa jinsi zote, Wilaya zote." Kwa kuzingatia maelekezo ya kifungu 11(3) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinachosema: "Serikali itafanya jitihada kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa za kutosha kuwawezesha kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za shule na vyuo vingine vya mafunzo."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napendekeza kabisa kwa nguvu zote kwamba elimu ya matumizi ya kompyuta ifanyike katika shule zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo naliona kidogo linaleta mtafaruku na mkanganyo ni suala zima la *Institutional Rationalization* kuhuisha Taasisi ambazo zinasimamia uboreshaji na uendelezaji wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ambazo zinasimamia maendeleo ya elimu nchini ni tatu. Wizara ya Elimu ya Utamaduni, TAMISEMI na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Wizara hizi pamoja na kwamba zinashughulikia elimu kwa namna moja au nyingine, lakini *mandates* zao zina tofauti kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, binafsi sioni ajabu kwamba wakati mwingine Wizara ya Elimu na Utamaduni ambayo ndiyo inasimamia masuala ya taaluma katika elimu ya msingi na sekondari, inapata *frustration* kuona kwamba usimamizi wa majengo katika Elimu ya Msingi na Sekondari huko vijijini hauendi vizuri. Inapata *frustration* wakati mwingine kuona kwamba zile stahili za walimu wanaofanya kazi kwa kujitolea sana, katika mazingira magumu, haziwafikii kwa nyakati zinazotakiwa. Hii ni kwa sababu zinasimamiwa na Taasisi zingine. Kwa hiyo, pamoja na kwamba Mheshimiwa hapa amezungumzia suala la programu tano za kuhuisha na kuboresha haya, nadhani hili itabidi liangaliwe kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine hapo hapo ni kwamba, kwa upande wa Elimu ya Sekondari ni kweli kabisa hapa Mheshimiwa Waziri leo ametangaza kuanza rasmi mpango wa MMES. Huu ni mpango mahsusi *(very ambitious program),* lakini mafanikio yake yanategemea pia kwa kiwango kikubwa na jinsi gani Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu inafundisha na kutoa wale walimu watakaofundisha katika shule hizi. Kwa hiyo, ni lazima pawepo na ushirikiano wa karibu sana katika Wizara hizi mbili ili waweze kufanikisha hii programu ya MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nadhani linafuata *logically* kutokana na hizi programu mbili za MMEM au MMES ni kwamba, programu ya MMEM imeboresha mazingira ya Elimu ya Msingi kwa ujumla katika nchi yetu yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji huo umeambatana na kupanua Elimu ya Msingi, majengo yamekuwa mengi, Walimu wengi zaidi wameajiriwa, vyuo vimejengwa, vitabu vya kufundishia na vya kujifunzia vimenunuliwa vipo, masuala ambayo yatapelekea kwamba hatimaye vijana wengi zaidi watafaulu mitihani ya kuingia Elimu ya Sekondari.

Sasa ni bahati iliyoje kwamba mpaka hapo Serikali imeona kwamba hii MMEM lazima ipate *support* ambayo inaambatana na hiyo MMES. MMES ni mpango ambao unapokea kutoka programu ya MMEM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kupendekeza ifuatavyo:-

Kwa kuwa nchi yetu ya Tanzania ilikuwa nyuma kielimu huko nyuma, kulinganisha na jirani zetu wa Kenya na Uganda na kwa kuwa MMEM inalenga kupasisha wanafunzi zaidi kuingia elimu ya sekondari na kwa kuwa mazingira ya elimu ya sekondari sasa hivi yataboreshwa vizuri zaidi kutokana na kile ambacho Mheshimiwa Waziri, ametangaza ambapo ni pamoja na kupunguzwa nusu ada za elimu ya sekondari, kuongeza ruzuku zinazokwenda katika kuendesha elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napendekeza kabisa kwamba Serikali ilifikirie kwa uzito stahili wazo la kuwa na elimu ya wote ya sekondari *(Universal Secondary Education -USE).* Hilo litawezesha kabisa kwamba na sisi tuta-*catch up* na wenzetu ambao wameshatangulia. *(Makofi)*

Kwa kuwa tayari nimeshachangia kimaandishi, napenda kumalizia kwa kusema kwamba sisi katika Wilaya ya Kahama kama tulivyomuahidi wakati anatuzindulia programu ya *operation,* elimu ni ufunguo wa maisha na mfumo wa elimu wa Wilaya hapo Kahama mwezi Agosti, 2001, tumemuenzi Mheshimiwa Rais kwa upande wa nyanja ya elimu kwa kuanzisha mashindano ya michezo. Tumeanzisha *league* ya Mkapa nadhani hii itakuwa ni ya kwanza katika Tanzania nzima hii ni kwa ajili ya wanaume. Aidha, tumeanzisha *league* ya Mama Mkapa kwa netiboli kwa ajili ya akinamama. Haya ni mashindano yatakuwa yanafanyika kila mwaka hii ni katika kuuenzi mchango ambao Mheshimiwa Rais, amefanya katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba naunga mkono moja kwa moja hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Elimu wa Utamaduni, ambayo ni hoja muhimu sana. Kwa sababu nilishazungumza na nilishatoa rambirambi, naomba niendelee na mchango wangu.

Kwanza kabisa, naomba niwapongeze Mheshimiwa Joseph Mungai, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote pamoja na watalaam wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo kwa kweli wameionyesha na kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna usemi usemao wengine ni Tomaso hawaamini mpaka watie kidole. Sasa wale ambao ni Matomaso wakatazame nchi hii ilivyojaa shule na elimu inavyozidi kupanda kwa *data* ya kitabu hiki. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ambayo tunaizungumza ni hotuba muhimu kwa sababu tunazungumza kuondoa ujinga na tunazungumzia masuala mazito ya kufanya jamii ya Tanzania ibadilike kabisa kujikwamua na umaskini kwa sababu unaposomesha binadamu maana yake umemwondoa kwenye maradhi pamoja na umaskini. Kwa hiyo, ni kitu muhimu sana.

Naomba nirudie kutoa pongezi zangu kwa wote wanaohusika. Naomba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa watu binafsi ambao wamewekeza kwenye sekta ya elimu kwa sababu kitabu hiki kinaonyesha humu, kuna watu binafsi na taasisi za dini nawapongeza sana kama vile Mchungaji Lwakatare, kwa shule zake nyingi tu ambazo zimefurika Dar es Salaam na wengine wengi tu ambao wameonyeshwa. Ningeomba Watanzania wengi wawekeze kwenye elimu. *(Makofi)*

Pia naomba nitoe pongezi kwa idara ya maendeleo utamaduni kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kwa sababu katika taasisi hii kuna mambo mengi sana kwa kweli wameyafanya. Ukitazama katika muziki, muziki ambao sasa hivi unapigwa Tanzania tumeondokana na *Ndomboloo* sasa hivi tuko kwenye muziki wa Kitanzania. Kwa hiyo, hii inaonyesha jinsi ambavyo idara yetu ya utamaduni inajitahidi sana. Kuna baadhi ya mambo mengi ambayo kwa kweli wanastahili kupongezwa kwa sababu hata kwenye redio sasa miziki ile ya *Ndomboloo* imekwisha tunasikia Mchinga, tunasikia Muumin, tunasikia miziki ya kikabila, Twangapepeta na mingine. Hongereni sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nipongeze kwa dhati kabisa Taasisi ya Kiswahili kwa jinsi ambavyo kipindi cha redio kinavyojaribu kuwaelimisha Watanzania maneno mazuri na jinsi Kiswahili kinavyokuwa. Napenda kuwapongeza kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba katika idara hii ya utamaduni nitoe ushauri kidogo kuna matangazo mengine naomba ikiwezekana Mheshimiwa Waziri yangefutwa kwa sababu yanadhalilisha, hayaendani na mila zetu. Liko tangazo kwa mfano ningeomba lifutwe ikiwezekana, tangazo lile la kudhalilisha mwanaume na mwanamke, mwanaume anatafuta fimbo nzuri ya kumpiga mwanamke, nadhani huwa mnaliona tangazo hilo linatisha, mwanaume anajiandaa kabisa anapiga na mluzi anajiandaa amkung'ute mwanamke, mwanamke anaogopa ili asije akapigwa. Ile haifundishi maadili mazuri kwa Taifa hili. Ningeomba matangazo kama hayo kwa kweli tungeyaondoa kwa sababu yanadhalilisha jamii. *(Makofi)*

Sasa baada ya kupongeza hayo, naomba na mimi mchango wangu niuelekeze kwenye mambo makubwa ya msingi kabisa, kwanza suala ambalo limezungumzwa na wote suala la madeni ya walimu walio chini ya Wizara ya Elimu yenyewe. Wakati

TAMISEMI wakiwa wanajiandaa kuhakiki madeni nilikuwa naomba na Wizara yenyewe kuna madeni ambayo wanahusika wenyewe ndani ya Wizara nao wahakiki ya kwao kwa sababu hawajaanza kufanya hilo. Kwa hiyo, nawaomba wahakiki ya kwao na watafute mkakati wa namna gani watayalipa. Hili ni la kwanza ambalo nilikuwa naliomba ambalo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Lakini la pili, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, kuna walimu ambao waliajiriwa mwezi wa Juni, 2003 ambao mpaka leo wanalipwa posho na wanalipwa posho hawajaingia kwenye *payroll,* hawalipwi mishahara yao wanakaa miezi mitano mpaka sita hawalipwi na ambapo sisi Bunge hapa tulishapitisha fedha walipwe, kulikoni, kuna nini? Walipwe hela zao hawa. Hili ni suala ambalo nilikuwa naliomba sana kwa sababu liko kwenye uwezo wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni urasimu ambao uko Wizarani, katika kutatua matatizo ya walimu kwa kweli kidogo inasikitisha kwa sababu walimu wengi tunapokwenda, wengine sisi wanatupa makabrasha tukawasaidie, lakini wengi wanaacha kufundisha wanakwenda Wizarani na Wizarani kunakuwa na urasimu. Je, Wizara haiwezi kutafuta mkakati wa namna gani wanaweza kutatua matatizo kuliko mtu kwenda Wizarani wakatatua kule kule kuliko kupoteza muda wa masomo na kupoteza muda kwenda Wizarani, hebu litafutieni mkakati hili Mheshimiwa Waziri, uweze kulitafutia namna ya kulitatua, kwa sababu naamini liko kwenye uwezo wa Wizara.

Lingine ambalo naomba nilichangie ni suala la elimu ya awali. Katika utafiti imeonyesha wazi kabisa kwamba watoto wengi ambao wanafanya vizuri katika shule ni wale watoto ambao walikwenda kwenye shule za awali, tunaita shule za chekechekea. Katika kitabu hiki nimeziona zipo. Lakini nilikuwa nashauri kwamba shule hizi ni chache, ziongezwe kwa sababu ndiyo kwenye *base,* samaki mkunje angali mbichi. Unapom-*train* mtoto akiwa mdogo hata akiingia shule ya msingi uwezo wake wa kuelewa unakuwa ni mkubwa na *data* zinatuonyesha hivyo.

Mimi nilikuwa nashauri kwa sababu baadhi ya shule hizi ziko mbali kwenye shule za msingi, Wizara haioni kwamba ingeweza kujenga utaratibu wa kuwa na shule hizi kwenye vijiji vyao, ili kuondoa kero ya mtoto kwenda huko kwa sababu ni vidogo na haviwezi kwenda shuleni. Vitoto hivi ingekuwa kwenye kijiji pale panakuwa na shule ya awali kwa hiyo, ingesaidia kuondoa bugudha ya watoto kupelekwa shuleni, wakajenga utaratibu huo ingetusaidia, wenzetu katika nchi nyingi wanafanya hivyo. Kwa hiyo na mimi ningeona ni suala ambalo lingetusaidia kuanza kujenga *base* ya mtoto kupata elimu akiwa mdogo zaidi. Walimu wa elimu ya awali pia nao waongezwe. *(Makofi)*

Katika elimu ya msingi, mimi mengi tu yameshazungumzwa lakini nataka kujaribu kusisitiza suala moja ambalo ni tatizo, ni zile Kamati za MMEM zimepata mafunzo lakini bado mpaka sasa hivi kuna utata hasa kwenye sekta ya fedha, bado semina zingeendelezwa zaidi.

Mimi nashukuru kwa kweli MMEM katika Wizara kwa maana ya wanaohusika wanajitahidi sana kutoa semina, lakini bado kuna utata ambao upo kwenye utekelezaji.

Sasa kuna baadhi ya madarasa mpaka leo hayajakwisha katika maeneo kwa sababu ya utata wa Mwenyekiti na Kamati au mwalimu mkuu peke yake kufahamu mambo kuliko kamati kutokuelewa baadhi ya mambo. Kwa hiyo, hili nalo tungeliomba litiliwe mkazo kwamba wapate semina za kutosha kwa sababu tunakwenda kwenye MMES lisije likatokea tatizo hili kwenye MMES nako napenda kuhimiza sana hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilikuwa naomba nilichangie kwenye elimu ya sekondari ambalo limezungumzwa sana kwa sababu tunaanza huo mpango wa MMES, ni vizuri ukaendana na ujenzi wa nyumba za walimu. Ndugu yangu, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, alikuwa anatamka shule zilizoko kwenye kata. Tatizo moja la shule nyingi za sekondari zinakosa nyumba za walimu na walimu wanaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vizuri nyumba nazo pia zikatiliwa mkazo, pamoja na kwamba nimeona kwenye *data* nyumba lakini ni vizuri nyumba ikawa ni sehemu mojawapo muhimu sana. Nyumba ziendane na ujenzi wa madarasa. *(Makofi)*

Suala la walimu limezungumzwa, lakini naomba nirudie suala ambalo limezungumzwa la msingi sana ambalo nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri kuna baadhi ya shule ambazo zinapita karibu na umeme, ama ni rahisi kupata umeme, nilikuwa naomba katika huu mpango wa MMES kuwe na programu maalum kabisa ya kuweka hilo, shule ziwe na umeme kwa sababu wananchi hawawezi kuweka umeme kwa sababu gharama ni kubwa sana.

Kwa hiyo, ni vizuri shule hizi ambazo zinapita karibu ziwekewe umeme, iwe ni programu kabisa katika MMES itasaidia sana shule hizi kuweza kupata taalum nzuri na wanafunzi kufundishwa mambo ya kompyuta yatajipa yenyewe. Lakini kusema wanakijiji ama kijiji kiweke umeme ni suala gumu. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, katika kuweka mikakati hili liwekewe.

Mimi nina shule natoa mfano kwa shule za Magoma inapitiwa na umeme hapo jirani lakini kuweka ni vigumu, Shule ya Hale tunazalisha umeme lakini tunashindwa kuweka umeme. Shule ya Semkiwa ni jirani tu hizi zote ni *community base secondary schools* za wananchi, lakini kuweka umeme ni ghali na naomba kabisa Mheshimiwa Waziri, hilo ulione kabisa katika mpango wa MMES suala la umeme liwekewe uzito wa kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala lingine ambalo linatuletea matatizo sana, sijui Mheshimiwa Waziri utatusaidia vipi kwamba tuna matatizo ya Bodi za Shule. Bodi za Shule nazo ni tatizo. Ni vizuri hili nalo ukalitafutia ufumbuzi wa kuwa ni watu gani waingie kwenye bodi kwa sababu tuna watu wengine ni wa ajabu ambao wanaingia kwenye bodi za shule hawaelewi mazingira ya shule ikoje na matatizo ya walimu ni watu tu wanachomekana mle matokeo yake ni kwamba unakuta shule haziendelei, zinakuwa hazipati maendeleo ya aina yoyote. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri utoe mwongozo wa namna gani bodi hizi ziwe ya aina gani na watu wa namna gani wamo mle. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangaa *secondary school* moja inaongozwa na mtu hata *secondary school* hajafika, lakini ndiyo taratibu hizo kama mambo yakiwekwa ovyo ovyo basi unaona ni matatizo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, hilo ulione kwamba bodi ni muhimu kwa sababu ndiyo inayoendesha shule. Idara nyingine ambayo wenzangu wamezungumza na mimi naomba niizungumze kama mwalimu ni kwamba taaluma haiwezi kukua kama hakuna ukaguzi hata siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Wizara ikubali kwamba imetekelekeza ukaguzi. Idara hii ni yatima, idara hii ukitazama hata *data* hapa zinaonyesha wazi kabisa kwamba idara ambayo imeachwa ina matatizo hata huu mpango wa MMEM wakaguzi walikuwa hawapewi fedha za kufanyia kazi. nategemea hata katika MMES inawezekana wasipewe, kwa hiyo, wapewe fedha, wanafanya kazi katika mazingira duni mpaka leo hawana ofisi nzuri, hawana usafiri kama ilivyoonyeshwa, lakini baya zaidi mpaka leo wanatumia *typewriters* kitu ambacho kimepitwa na wakati. Wenzao huku wako kwenye kompyuta wao wanapiga *typewriter* mpaka leo ukienda kwenye maofisi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nenda, ukifika kwa ofisa elimu mambo yake mazuri pale, ana *computer,* ana *funds* hawa hawana. Sasa huwezi kwa kweli taaluma ikapanda kama mwalimu hakaguliwi. Kuna walimu wengine ni wavivu hata kuandaa *lesson notes* hawaandai, hata *scheme of work* hawaifuati. Lakini huyu anapokwenda akitia *ambush* basi unaona walimu wanachachalika, wanapanga watakavyofundisha na wanakuwa na tahadhali kwamba sasa anaingia mkaguzi. *(Makofi)*

Kwa kweli ni idara ambayo naomba muipatie fedha za kutosha hapa hii ripoti yenyewe inajisuta kwa sababu ndiyo ambao wamepata fedha chache zaidi ili waweze kupata uwezo wa kufanya kazi na taaluma iweze kupanda. Unakuta wakaguzi pia hata *promotions* hawapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilikuwa naomba nilizungumzie ni kwamba mishahara ya walimu ina utata kidogo. Sijui inakuwaje, ningepata maelezo, mwalimu anayeingia leo na mwalimu ambaye amekaa miaka mitano nyuma mshahara umelingana. Sasa hili limekuja kujaje? Linakatisha tamaa, walimu ambao miaka kumi walikuwa wanakula chaki, wanakuja wanasema mtu ametoka juzi shuleni anaingizwa kwenye msululu na walimu wa zamani. Kwa kweli hili linakatisha tamaa, naomba hilo nalo lirekebishwe haiwezekani mtu atoke chuoni leo afanane na mtu aliyefundisha miaka kumi nyuma, eti kwa sababu kuna utaratibu, kuna *formula* hizi, *formula* za aina gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, *formula* hiyo hawawezi kutazama mwalimu wa zamani na anayeingia leo ili kummotisha wa zamani ajione kwamba kukaa kwenye ualimu muda mrefu ni sahihi. Hili naomba nalo Mheshimiwa Waziri ungelitazama kwa sababu yako malalamiko kutoka kwa walimu wengi ambao wanashughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa Mheshimiwa Waziri, nikuombe katika Sera, hili nalizungumza miaka yote nakuomba Mheshimiwa Waziri umefanya kazi nzuri sana na wewe ni mwanamichezo naomba ufanye kila njia yaani mkae *Cabinet,*

muone namna gani mtarudisha mashindano ya shule za msingi , ya sekondari (UMISETA).

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo nalizungumza kwa sababu juzi juzi hapa wamekuja wenzetu kutoka Kenya wanataka timu yetu ya *secondary school* iende Kenya. Sisi hatuna *combine,* ikabidi tuokoteze tu lakini kama tungekuwa na mashindano yale kwa kweli tungeweza kuwa timu nzuri. Hili nalisema kwa nia nzuri pamoja na kwamba siku zote unalijibu kwamba watu waendelee kucheza na mimi nauliunga mkono, lakini kukosa *national competition* kwa kweli ni tatizo kubwa na hatuwezi kupata wachezaji wazuri na wenye vipaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa nafasi hii. Lakini naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wameionyesha katika hotuba hii. *(Makofi)*

Hotuba hii ni nzuri sana na ina dira sahihi ya nchi hii. Kwa hiyo, ninaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Kama alivyosema mwenyewe kwamba mambo ambayo ametueleza leo ni baadhi ya yale ambayo hayajawahi kutokea katika Bunge hili na mimi nahakikisha katika miaka minane, tisa niliyokaa humu ndani haijawahi kutokea. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naamini kwamba kwa hoja hii aliyoitoa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni hoja ya kuondoa umaskini katika Taifa hili sasa inazungumzika. Hoja ya kuzungumza mipango ya kuingia katika *globalization process* ya nchi hii sasa inazungumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina imani tunakokwenda tunakwenda kwenyewe. Hebu niwaambieni wenzetu Marekani mwaka huu tarehe 28 Juni, walisema nini. Kule Marekani mwaka huu *Secretary of State* wa Elimu alisema hivi: *"As time will recognize the central cardinal of fact that education is a big business. It is a huge part of our economy, a large segment of our gross national product. Last year as a nation we spent more than half a trillion dollars on get well education, this was only at local state and federal levels. Our nations education effort are the largest financial and ever leveling spending on the defense, agriculture, transportation, telecommunications, entertainment sector and is time we use the little business sense to strengthen our own schools." (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea na sehemu anapozungumzia habari ya *globalization* katika mfumo mpya ambao sisi tunatakiwa twende kisha tuzungumze masuala muhimu ya kwamba na sisi tunajiandaa kweli kwenda huko, maana hamwendi kwenye *globalization,* hamkujiandaa. *Globalization can only be useful if you are prepared.* Kama hauko *prepared* hakuna unachoweza kufanya.

Sasa Wamarekani wenyewe wanasema hivi: *"We may not have much of a choice globalization has made quality education absolutely imperative." Quality education* ndiyo inayozungumziwa hapa siyo blabla! Mimi nasema huko tunakokwenda haya anayoyafanya Waziri jamani tumuunge mkono, tumsaidie na tumpongeze sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, wao Wamarekani katika maelezo ya yule *Secretary of State* wa *Education* anasema: *"In the first, graduating students competed with job seekers in their community country, now our graduate compete globally."* Mnasikia?

*Now our students competes globally, there is no longer a guarantee of employment with high school diploma, even a college diploma may not be a meaningful measure, many employers are now asking for prospective employees. We have ended a new age that in first century is now a service economy dependend on technology, innovation, information and technical skills." (Makofi)*

*We need what are called knowledge workers, and knowledge workers must be well educated. Marginally educated or under educated workers are not in high demand.* Sisi tunataka Watanzania wawe *in high demand.* Maandalizi haya yanatupeleka huko ndiyo maana naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Napongeza sana jitihada zote ambazo zinakuwa zinafanywa na Mheshimiwa Rais kama Mheshimiwa Waziri alivyotueleza asubuhi hii tunampongeza sana Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kazi nzuri ya kuongeza elimu na kuifanya nzuri katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nazungumza na rafiki zangu kutoka *East African Community,* wanasema tukiitwa kwenye *interview* maana ninyi ni Wabunge lakini mtaondoka humu mtaenda kutafuta kazi mtapewa *interview,* wanasema kile kingereza na vitu vingine vinavyotokea vya kujua mambo ya Kimataifa, watoto wetu hawawezi ku-*compete.* Wanasema *East Africa* peke yake kama tunataka kweli ku-*compete* wanachukua *on the bases of quality education* watu wetu hawa-*qualify* hata kupewa kazi. Sasa unaweza kupinga ukasema ahaa, mbona tuko hapa. Lakini ukweli ndiyo huo. Sisi tunataka kweli tushiriki katika hii *process* ya *globalization* na kushiriki huku ni lazima tuwe *broadened* kimawazo tuandaliwe, tukishaandaliwa watu wetu waingie kwenye mambo ya kisayansi ya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Tanzania iko *highly under represented* katika *international organizations.* Leo una watu wanaojua wanaweza mambo lakini ukisema nendeni mkatafute kazi fulani inayoandaliwa ni wachache sana wanaofanana na akina Mchumo wa kuweza kupata kazi za *Common Fund for Commodities* ni wachache. *What we do* ni mlolongo huu anaouanzisha Waziri wa Elimu kwamba *quality education* sasa ndiyo iko njiani na tunaendelea nayo.

Miaka iliyopita nilizungumzia habari ya kuachana na malipo kwa *primary school* nafikiri ni mwaka 1998 iko kwenye *Hansard,* nikasema njia pekee ya kulikomboa Taifa hili ni kuachana na karo ya *primary school* maana watu wetu ni maskini, uwezo hawana, ukienda shule wengine wanaona taabu kubwa kabisa. Leo hii tukitaka kuendelea

tuangalie mifano ya nchi kama India na nchi zingine ambazo zinapenda kuendeleza hii azma tunayoizunguma. Elimu ya *secondary school whatever the level* yote ni bure na sisi tunafiriki tunakwenda huko na aliyeanzisha Mheshimiwa Waziri yanatupeleka huko. *Secondary school education* iwe bure. Iwe bure, watoto wetu wasome na wapewe vitendea kazi vizuri na walimu wafundishe vizuri, waandaliwe na wenyewe kisha maslahi yao yaangaliwe, yakishaangaliwa tutakuwa tunakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana wanasema tumechelewa hapa nikitoa *data* za *East Africa* peke yake sisi tuko nyuma, nikitoa *data* za shule Kenya ulinganishe na zetu tuko nyuma sana. Lakini *I am saying the path is clear, now we are going,* tunatembea, tunakwenda hatujasimama. Lakini jamani tuchokisema hebu nizungumzie *a global aspect* ya *performance* ya Serikali yetu. Nafikiri mwaka 1997 au 1998 nilizungumzia habari ya kila Wizara, Waziri anaingia kwenye Wizara anakuja na dira ya nini anataka kufanya. Wewe Waziri unakuta unasema yasiyoeleweka hapa! Unafikiri tutasema nini? Tutakusifu tu? Tunamsifu mtu anayefanya kazi maana tunapenda maendeleo. *We have seen other people's development.* Mpaka unamfanya yule aliyekuchagua awe na wasiwasi na wewe. *(Makofi)*

Lakini anasema basi tu bwana twende tu hivyo hivyo. Ndiyo haya ni maneno ya kweli, *we must be visionary, we must show the ideals that we believe in,* kama tunaamini mambo ya kwenda tu Mungu nijalie, Mungu hayuko kukujalia tu bila kufanya kazi, *you must show that you can work* na baadaye tutakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usikubali kufanya dhambi kesho ukasema Mungu anasamehe, kumbe wewe ndiyo unarudi nyuma katika hili Mungu ni kweli anasamehe lakini katika hili la utendaji kazi kakupa nguvu kakupa kila kitu wewe unasema Mungu nijalie tu twende hili isikubaliani nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliyoyazungumza ni ya kumsifia Mheshimiwa Waziri. Sasa naomba niseme hivi kule Kasulu tumejitahidi sana kujenga shule na watu ukiisema Serikali bwana wewe hufai.

Kwanza niwaambieni kwangu Upinzani hakuna, maana wengine hasa wapinzani uchwara wamekuwa wanasema eti ohoo, mnaona hizi shule zinajengwa kwa hela zimetoka Washington, mimi kwa kweli huwa ni muwazi na msema ukweli, ninawaambieni hivi ninyi hizi shule mnasema Washington aliyekwenda ni CCM au aliyekwenda ni hicho chama chenu au baba zenu au mama zenu ndiyo walikwenda huko niambieni?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana Chama cha Mapinduzi kimefanya kazi kubwa katika nchi hii na lazima tukipongeze kwa kila hali, haiwezekani mtu anakuja anasema waliofanya hili sijui ni nani? Huko Washington wewe una ndugu yako, una mzee wako yuko huko anakuwakilisha, hakuna. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Niabu Spika, sasa jitihada zinapokuwa zimefanyika basi hizi ziendelee kupongezwa, zipongezwe. Mimi najua ninachotaka kukisema ni kwamba

Ikama ya shule bado ina mapungufu mengi. Haya mapungufu mimi najua tuko njiani, baadhi ya mipango aliyoonyesha Waziri anaonyesha tunakokwenda na mapungufu yatakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kule Kasulu niseme ziko Shule naweza kuzitaja kichwani. Ipo shule ya Kalege kule Tarafa ya Muyam, shule ya Mgera na shule ya Ukererema. Hizi shule zote na nyingine ambazo ziko Tarafa ya Manyovu kama vile Janda, Nyamihanda, Nyangorongo, Buhigwe, Muhinda, Nyaruboza, Mubanda, zina mapungufu makubwa ya walimu. Hii niliyoitaja ya Kalege ina wanafunzi 400, ni shule mpya, lakini *you will be shocked* ina walimu wawili.

Namwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie sana *priority* ya kule kwetu kwa sababu wananchi wamejenga shule kwa nguvu, kwa hiyo naomba sana nipewe walimu. Nikishapewa walimu, kisha *secondary schools* hizi ziangaliwe. Huwezi kuwa na *Headmaster* ambaye hajaona *classroom of the University* ukasema hapa najiridhisha, nakwenda karne ya 21 nikiwa kifua mbele, hapana. Haiwezekani! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale mimi siwaungi mkono kabisa kupewa fedha, hapana. *Their knowledge base* iko chini sana na uwezo wao wa kuendesha mashule haya ni kidogo sana. Shule hizi hazina walimu. Naomba shule yangu ya Mnania ipewe walimu *graduates* kwa sababu ni shule ambayo imetoa matunda mazuri na inafanya kazi nzuri kule Kasulu Magharibi. Naomba pia shule ya sekondari ya Myama nayo ipewe walimu maana hizi ndio shule zenyewe zinafanya kazi kubwa kwa watu ambao walikuwa wanaona elimu hakuna, sasa wamejikomboa, wamejenga *secondary schools* 7 na mwaka kesho tunafungua 9 zaidi. Ni jitihada kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nafikiri tunakwenda kasi sana na ndio maana nasema twende hii karne inayofuata tukiwa kifua mbele maana karne ya 21 tuiite ni karne ya ukombozi na ndipo tutakapofika tukijiamini kama Watanzania. Tusiende na unyonge, haitatusaidia. Ooh, huyo bwana kasema hivi, huyo bwana kafanya hivi hatufiki! Hata wale waliokwenda kwa Yesu, Yesu akawaambia jiaminini kwa hayo mnayofanya. Kama mnayafanya kwa kuamini kwamba ninyi ni Mitume wangu endeleeni kuwa Mitume wangu maana hamtafanya kazi njema. Ndio! *(Kicheko)*

Ninyi mnakumbuka Petro alipokuwa anatembea juu ya maji akaanza kuwa na uwoga akaanza kuzama, aah, Yesu akamwambia mbona wewe mtu wa mashaka mashaka? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naomba madeni ya walimu walioko chini ya Wizara hii pia yalipwe, yafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie Bajeti ya Wizara ya Elimu. Ningependa kusema kwamba naunga mkono Bajeti hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, ningeomba Baraza lake la Mawaziri wapeleke pongezi zetu kwa Mheshimiwa Rais asikie kwamba kwa kweli tunampongeza, sio vizuri kuwa anasikia tu tuhuma, inafaa asikie na mazuri yaliyofanywa na Serikali yake. Kwa kweli tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwapongeza Wizara ya Elimu kwa sababu kwa kweli ni Wizara mojawapo ambayo ukienda na matatizo ya wananchi wa Jimbo lako wanakusikiliza na wanayafanyia kazi. Nawapongeza sana. Kila mara nikienda pale nafurahi tu kwa sababu nitakayoambiwa najua kwamba yatatekelezwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Bajeti hii kuanzia Wizara zilizotangulia mpaka hii, nadhani imeua Upinzani kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Imeua! *(Kicheko)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Kwa kweli nampongeza ndugu yangu mpinzani, aliamka akaipongeza kabisa, amekosa la kusema na nadhani Wizara zote zitakuwa hivi na kama tukiendelea hivi tutakuwa Chama kimoja, hakutakuwa tena na Chama cha Upinzani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema machache ya kuboresha. Nianze na maeneo yaliyoko nyuma ambayo yamechelewa kupata elimu. Katika ukurasa wa 21 katika kitabu cha Waziri ameandika kuhusu kuboresha utoaji wa elimu kwa jamii zilizo nyuma kielimu na zisizofikika kwa urahisi. Hayo maeneo kwa kweli ni maeneo yaliyoko nyuma na nashukuru sana Mheshimiwa Rais alipofanya ziara mwaka 1997 alijionea mwenyewe. Alikwenda Ngorongoro, Monduli, Simanjiro na Kiteto.

Baada ya kuona hali ilivyo akasema kwa kweli tukiacha maeneo haya yakiwa hivi, litatokea tabaka kubwa sana la maeneo yaliyoendelea na yasiyoendelea. Hilo tabaka limekwishaonekana kabisa. Kwa sababu kuna maeneo mengine ambayo ni magumu sana kufikika na ukiangalia hata ukienda *University,* jamii hizo hazipo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ajabu hawafiki hata kumi walioko *University* kati ya wanafunzi 2000 walioko. Hiyo imeshaonesha ni *gap* moja kubwa sana ambayo baadhi ya jamii zimeachwa. Inafaa sasa Mheshimiwa Waziri aangalie. Ameyataja hapa makabila lakini sikuona jitihada zilizoandikwa kwamba watafanyiwa nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo, sio kwamba hizo jamii zilizobaki nyumbani hazitaki elimu siku hizi, wanataka. Lakini kuna mambo ya mazingira. Ukienda katika shule hizo utakuta hawana walimu. Unakuta walimu wawili katika shule moja. Tatizo ni maisha magumu katika maeneo hayo. Mwalimu kutoka katika shule hizo Vijijini kwenda kufuatilia mshahara wake, anatumia nusu ya mshahara, anachukua siku tatu kwenda na kurudi. Anatumia zaidi ya shilingi 30,000/=.

Kwa hiyo, unakuta kwamba maeneo hayo walimu wanakataa kwenda, wanaajiriwa kwa sababu kila Wilaya wanapangiwa walimu, lakini wanakwenda kuona na baada ya kuona tu maisha ya kule hawarudi tena eneo hilo. Kwa hiyo, kuna upungufu mkubwa sana wa walimu, naomba Wizara iangalie na iwasaidie Walimu walioko huko wapate priority, wapate posho yaani ziwe shule maalum kamba walimu walioko huko waangaliwe na wakija kufuatilia matatizo wanakuja kufuatilia mishahara yao wapewe haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi mishahara ya walimu inapitia Benki. Sasa walimu wa kule Vijijini, mwalimu mmoja akienda kuleta mshahara wengine wanaandika barua ili huyo mmoja alete mishahara ya wengine. Siku hizi haiwezekani kwa sababu mishahara inapitia Benki, kila mtu anakwenda kwenye *account* yake kutoa fedha. Sasa unakuta mwalimu mmoja akienda anachukua siku tatu. Kwa hiyo, kama kuna walimu watano katika shule hiyo ni siku 15 walimu hawapo. Sasa ukikadiria kwamba siku 15 walimu hawapo shuleni kwa mwezi mmoja, kwa mwezi mwingine ni hivyo hivyo, unakuta hata *syllabus* nyingine hawatazifikia hata siku moja.

Kwa hiyo, tunaomba tusaidiwe kabisa kujenga nyumba za walimu, tunaomba hao walimu wapatiwe nyongeza ili waweze kukaa huko. Kwa kweli wasipoangaliwa, maeneo hayo yatabaki nyuma na maeneo mengine yataendelea na mengine hayataendelea. Ndio maana wakati ule baada ya Rais kuona hali ilivyo akasema kwamba maeneo haya yajengewe sekondari. Bado tunasubiri tu hiyo ahadi ya Rais, tunakazana wenyewe lakini tunataka Rais alivyosema kwamba tujengewe sekondari, Mheshimiwa Waziri katika Bajeti yake atekeleze hilo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika maeneo yetu, siku hizi tunajaribu sana kuchangia sekondari. Lakini tusipopata msaada kwa kweli hatutaweza kufikia lengo. Mimi nashukuru shule ya sekondari ya Longido tumekubaliwa tufungue *A-Level.* Tunashukuru sana na kuna nyingine iliyoko Monduli, tunaomba mtusaidie tupate na sisi hizo shule mbili ziwe *A-Level* kwa sababu kwanza ni mara ya kwanza kuingia katika Wilaya zetu shule za aina hiyo, wengine wanasema kwamba wanajenga shule kila Kata sekondari moja, bado sisi tunajenga Tarafa yaani Tarafa nzima ndio tunashughulikia sekondari moja, uone tulivyokuwa mbali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atupe msaada mkubwa sana ili na sisi tuangalie kama tutakimbia kuwakuta wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni urasimu uliopo katika Halmashauri walimu wanapokuja kufuatilia mahitaji. Walimu Wakuu wanakuja wanakaa katika Halmashauri zaidi ya siku tatu, yale yaliyowaleta hayatekelezwi yaani hawa Walimu wanazungushwa kana kwamba wamekuja kutafuta mkopo pale, kumbe ni matatizo ya wananchi ndio yamewaleta lakini wanazungushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana huu urasimu ufutwe na uangaliwe. Serikali ikae tena na kuangalia hizi fedha zote zinazopelekwa katika Halmashauri kwa

sababu Wizara ya Elimu na Utamaduni, inapeleka fedha Halmashauri, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Afya, kwa hiyo, unakuta watu wanalundikana pale, inakuwa ni matatizo. Kwa hiyo, walimu wanapata matatizo makubwa sana, ni kero!

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na madeni yao wanayofuatilia, kuna madeni makubwa sana wenzangu wamekwishazungumzia hasa kwa Walimu wapya. Hivi mwalimu ambaye unampeleka Matale, ni wachache wanaofahamu eneo hilo ninalolitaja, ukifika mwenyewe hutaki hata kukaa huko siku mbili. Sasa unampeleka huko hukumpa chochote, atakwendaje kuishi? Walimu walioko huko waangaliwe kwa sababu matatizo ni makubwa.

Kwanza bei ya vyakula kule debe ni shilingi 10,000/= halafu hukumpa chochote atakwenda kuishije? Matatizo ya walimu ni tofauti kabisa kwa walioko Mijini na walioko Vijijini. Ni matatizo makubwa sana! Naomba sana Walimu walioko Vijijini waangaliwe.

Jambo la mwisho ni ada, mmepunguza ada za shule za kutwa, lakini hawa watoto ambao ni wazazi wale wale wa maskini wako bweni, lakini hawakupunguziwa chochote. Hebu muangalie kwa sababu kwa kweli hilo inafaa kabisa tuangalie ada. Ada bado ni kubwa lakini tunashukuru. Kwanza nawashukuru sana mkisema kwamba hizo fedha zitaachwa shuleni, lakini tuangalie kwa sababu watoto wote hawafanani, kuna watoto wa wazazi wasio na uwezo bado wanahitaji kupunguziwa hizo ada.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nisingependa kugongewa kengele tena, ningependa tu kurudia kusema tena kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika nilikuwa nakushukuru wewe kwa kunisimamisha hapa. Kwa hotuba kama hizi ambazo zinapongezwa na Wabunge walio wengi mpaka upande wa Upinzani, inakuwa vigumu sana kuchomekeza mambo ambayo yanaweza yakaleta maudhi katika Bunge hili. Tumesimama tu kupongeza kwa sababu yanaonekana. *(Makofi)*

Sasa kabla sijaanza kuchangia hoja yenyewe iliyoko mbele yetu, naomba kufanya kidogo kama maombi au marekebisho. Ukurasa wa pili kuna majukumu ya Wizara pale. Sasa mimi nimeamua kuwa mchokozi, pale kifungu (e) nimeamua kuweka kiwe cha sanaa, lugha, mila, desturi na ukaguzi wa filamu, nimeongeza na makumbusho ya Taifa. *(Makofi)*

Labda mtanisahihisha kwa sababu makumbusho ni sehemu ya utamaduni sio utalii kwa sababu hayapandwi, ni kumbukumbu za kila siku. Kwa hiyo basi, hayapandwi tukasema kwamba panda, kata mti panda mti. Haya makumbusho ni matukio mbalimbali ya historia ya watu wanaotajwa. Kwa hiyo, sio utalii, ni sehemu ya utamaduni wetu.

Halafu ukurasa wa tatu katika hiyo hiyo, nimeongeza kipengele kingine cha nane pale, *TES* nikaongeza kwamba pamoja na majukumu ya Wizara hii *TES* bado haijafa, bado *TES* ipo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri afuatilie hili suala. Unakuwa *goalkeeper* mzuri, unadaka mpira unarudisha uwanjani, hapo unaudaka tena ndio utakuja. Lakini

usiutupe tu kama hivyo. Andika *TES* ni majukumu ya Wizara isifutike hiyo ikawa *end of the story.*

Masahihisho mengine, sijui Kiswahili nitakuwa sahihi kusema kwamba Waziri wa Elimu na Utamaduni. Hotuba ya Waziri wa Elimu na Utamaduni hapa unasema kimepigwa chapa. Aidha, unaongeza kitabu cha hotuba ya Waziri, halafu kimepigwa chapa au Hotuba ya Waziri imepigwa chapa. Kwa hiyo, unakuta huwezi ukakipiga chapa hotuba ya Waziri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, Tanzania ni moja katika nchi ambazo zinasonga mbele duniani ambazo zimepata Uhuru wake wa kweli kwa mapambano ya kweli kisiasa na nguvu ya hoja ya Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mungu amweke mahali pema peponi, ni kwamba alisaidia Taifa hili pamoja na kwamba sisi tunajidai na kujigamba tunafuata nyayo zake, lakini Nyerere alikuwa na buti kubwa, hatuwezi kuzikanyaga nyayo zake *unless* tunajitahidi kusoma vitabu vyake tuweke kama kumbukumbu tu itusaidie kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba zake ambazo zilikuwa zinaona mbali, zenye *vision,* hazina mfumo wa tochi kumulika mbali kwake giza, kwa hiyo sasa hivi tuzingatie hotuba zake za kila siku, wazo la baba, ngoja tuliwekee wakati, basi hapo tutaweza kuiweka nchi yetu ikaonekana huru.

Pamoja na mafanikio yaliyokuwa yamepatikana, yalikuwa yamesomwa na Waziri kwa mfululizo huo kwamba ukarabati wa shule, nyumba za walimu, kufuta michango ya UPE, kulisha wanafunzi, madarasa mapya, madawati, ukarabati na mambo mengine mengi yaliyojitokeza, hiyo ni shehena peke yake iliyowaridhisha Watanzania kwamba kweli Watanzania wanasonga mbele. Lakini twende mbele pamoja. Kama ninyi nikisema tusonge mbele, Naibu Spika lazima mbele kwenu ni kwetu sisi huku. Sisi tutakuja huko, tutawakanyaga. Twende mbele ya Taifa linakotaka kwa dira ya Taifa, sio mbele anakoelekea mtu binafsi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ni kwamba kuhusu Bajeti, mtiririko wa Wizara ya Elimu, Bajeti yake ni nzuri, sio bajeti mchwa ambazo hushambulia mara kwa mara. Watu walidhani mchwa wana akiba ya kutosha kwa kuona vichuguu, kumbe yale ni majengo yao, ni nyumba zao, chakula hawana. Bajeti hii katika mwaka 1995/1996 mlipata shilingi bilioni 85, mwaka 1999/2000 mkapata shilingi bilioni 141 na mwaka 2004/2005 ni shilingi bilioni 158.

Sasa tunapenda Bajeti ambayo inaendeleza na inatumia kidogo. Kwa mfumo huu tumeona kwamba shilingi bilioni 158 katika hizo shilingi bilioni 105.6 zinatumika kwa maendeleo na shilingi bilioni 52 zinatumika kwa ajili ya *supply vote,* kwa ajili ya kulipia haya. Bajeti hii ni *excellent,* sio bajeti mchwa ya kushambulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa MMEM yako mafanikio makubwa, tumejipima. Lakini sasa hivi tukianza kupima tutajipima urefu wakati tuko shimoni. Tungoje itatokea taarifa mahsusi na itatolewa na Kamati yetu ya Maandalizi ya

Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, hapa utakuta idadi ya madarasa na idadi ya walimu na idadi nyingine. Hapo utapata mafanikio kwenda kuwaambia wananchi kwamba tulikuwa hatuchezi wakati ule, tulikuwa tunatembeza sera zetu. Hapo tutakwenda kifua mbele. Wale wanaodanganya kwamba hii sera ilikuwa imefanywa kwa ajili ya wao, hiyo tabia ya kurumbizi tuache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kurumbizi aliona gogo la mbuyu limeelekea kwenye mto uliofurika, akapanda juu akawa anawadanganya ndege wenzie kwamba nalipeleka, nalipeleka! Kumbe linapelekwa na maji. Hiki ni Chama cha Mapinduzi kinapeleka gogo hilo. Sasa la ajabu ni kwamba gogo hilo likapelekwa likafika mahali penye daraja likanasa, uwezo wa kuligeuza hana, akasema *komredichichi* mampumziko! Kwa sababu alikuwa hana uwezo wa kuligeuza lile gogo, tuwe pamoja. Upande wa Upinzani, Chama Tawala tuwe pamoja kushughulikia Watanzania ili kusudi waelimike. Elimisha wananchi, wape afya, walinde, wakinge, halafu wawezeshe wafanye kazi, Taifa linaendelea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ni kwamba naingia kwenye upande wa wananchi. Hapa ni moyo wa wananchi wa Tanzania ambao wamejitokeza kwa nguvu zote na juhudi zao katika maeneo yao, katika Vijiji vyote tisa na kitu, kwa shule za msingi zilizoko ndani yao ili kujitokeza angalau kuchangia kwa nguvu zao. Hapa natoa pongezi kwa wananchi wa Vijiji vyote Tanzania nzima wakiwemo na wale wa kule Jimboni kwangu. Napenda kutaja na Kijiji cha Ijanija kwa sababu kuna shule ya Ijanija Mzega, wananchi kama wa kule Nyamitwiti, Bunda, kule Jimboni kwangu watu wa Luholole, Changa, Kibwaya, Mfumbwe, Logo, Uponda, Mifuru, Hewe, Bagiro, Nyamigadu, Mkololo, Kumba, Amini, Ludewa, Hurugi, Ng'ala Tarafa ya Ngerengere na Kata ya Mkulazi kule Kata ya Mkulazi.

Sasa najua kabisa walimu walikuwa na matatizo mkija kufuata mishahara yenu mnapita kwa kujia *TAZARA,* sasa nashukuru sana kijana wetu Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na kijana wetu Mheshimiwa John Magufuli, tumepata fedha iliyokuwa ya mwaka jana ambayo ilikuwa haijulikani iko wapi, baada ya kuunda Tume ya Wabunge, barabara ile inatengenezwa. Nimepiga simu kwa *DED, DED* yuko Serembala leo nimepata habari, sasa kutoka Serembala kupita Mkulazi, wiki ijayo Semindu Pawa anakuja kufuatilia hii. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza *World Vision* na *TASAF,* MMEM na Halmashauri za Wilaya kwa kuinua amko hili kwa sababu huwezi ukafanya kazi hii peke yako kwa ushirikiano na watu waliokuwa wanashirikiana. Kwa hiyo, wote ni wadau wa elimu.

Kwa upande wa fedha za MMEM pametolewa mwongozo tu wa kuzitoa fedha hizo, lakini hakuna mwongozo unaodhibiti watu waliokula fedha zile. Kwa sababu yako matokeo kwa Walimu wasiokuwa na uaminifu, wamezitumia vibaya hela hizo na nimekamata barua mbili hapa za Afisa Elimu mmoja akiandikia Kijiji kimoja katika nchi hii kuwaambia kwamba yule mwalimu aliyekula kama laki tatu, aachiwe atakatwa mshahara wake. Barua hiyo iliandikwa mwaka 2002, mpaka leo mwalimu yule

hajakatwa, kwa hiyo, Afisa Mtendaji wa maeneo hayo ameleta barua hizo, sitamkabidhi Mheshimiwa Waziri, hiyo iko ndani ya uwezo wetu, tutalimaliza, tutamchukua kama kipanga, kama mwewe anavyochukua vifaranga vya kuku. Mengine yako ndani ya uwezo wetu. *(Kicheko)*

Lingine kuhusu Tume zinazokusudiwa kuundwa kwa ajili ya kufuatilia mafao ya Walimu na wafanyakazi wengine, inaeleweka kabisa kwamba mfanyakazi fulani *cheque number* fulani, halafu *OC* umepeleka kiasi kadha Wilayani, Wizara ya fedha inajua imepeleka kiasi fulani cha fedha, mwalimu ambaye hajapokea mafao hayo yupo, unaunda Tume ifanye nini? Pale ilikuwa cha msingi ni kwamba kukamata watu wale wote ambao fedha zile wewe una uhakika kwamba zimepelekwa, kwanza utawapa shida Tume, watazongwa kama mpira wa kona. Wakisikia kwamba Pawa yuko kwenye Tume watanifuata tu, watasema unajua mimi kuna Bima na nini na nini, kwa hiyo, utakuwa na *frustration,* madeni yatazidi kuliko hii. Ule uhakika uliofanyika kama Wizara mmefanya, kama hamjafanya, basi ninyi mpewe mpaka tarehe 31, muwe mmelipa kutokana na *consolidated fund.* Kwa sababu Waziri Mkuu akishatamka na Wabunge wakishasema, kinaitwa kilio cha mtu mzima. Mtu mzima akilia kuna jambo.

Kwa hiyo, naomba tafadhali sana mliangalie hili kwa ukamilifu sio kwa njia ya kisiasa. Kwa utaratibu ule ule ambao tumeagiza na sisi Wabunge, ile hoja aliyotoa Waziri Mkuu ni hoja ya Bunge. Kwa hiyo, tutakaporudi Majimboni kwetu kwa sababu kunakuwa na ziara za mrejesho, moja ya hoja za mrejesho ni hii kuuliza, Walimu wangapi katika Jimbo hili ambao wamefanikiwa? Kwa hiyo Walimu tutawaita pamoja na Tume yao ya Wilaya ili kuwauliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, pamoja na kwamba kengele imelia, nilikuwa nasema kwamba kuna shule ambazo haziwezi kuhimili idadi ya watu katika Kijiji. Inatakiwa kila Kijiji kiwe na shule lakini sio kila somo linafundishwa kila wakati na kila mtu. Kwa sababu kwa utaratibu huo kuna shule za msingi ambazo zinaongezwa, wengine wameanzisha mikondo, kwa mfano kule katika Jimbo langu la Morogoro Kusini Mashariki kuna mkondo. Tumefungua shule Kiloka, inaitwa Dioghubha. Ni shule nzuri tu tumepata katika mgao wa fedha. Kuna watu wa miradi mbalimbali ambao wanaleta fedha za madarasa katika mashule ambayo MMEM nayo iko pale pale. Wamepata msaada wa aina tatu katika shule moja. Sasa muweze kutathmini kwamba fedha zile ziingie katika mfuko ule au kuna nyingine zinarudi zikatiwa kinyemela.

Kwa hiyo, tathmini ifanywe kwamba huenda shule moja ikawa na wafadhili kama nane, basi akija MMEM anaonyeshwa darasa hilo hilo, wakija watu kutoka Japan wanaoneshwa darasa hilo hilo, kwa hiyo, inakuwa kama ni kiini macho. Mnauziwa mbuzi kwenye gunia. Kwa hiyo, tafadhali sana, naomba Wizara ifuatilie, fedha hii ni ya walipa kodi wa Tanzania. Kwa hiyo, muwe waangalifu kweli kweli. *(Kicheko/Makofi)*

Mwisho kabisa ni kuhusu lugha. Lugha inaharibiwa kutokana na kuchomekeza baadhi ya majina na maneno ambayo yanajiingiza kinyemela katika Kiswahili. Yapo mambo mengine wakati mwingine unapoingilia, hata mchele unachaguliwa chuya zinaondoka. Unaposhabikia maneno, kwa mfano mtu anasema mambo, anajibiwa poa.

Hizo sio salamu au watu unakuta wanasema kwa mfano mpira umechezwa jana Yanga ameshinda wamecheza na Simba kwa mfano, sasa Simba inakuwa imefungwa na Yanga, wanasema eti Yanga yaichabanga. Neno chabanga nimelitafuta kwenye kamusi hakuna au yairarua au wanatumia neno kwa mfano yaibugiza au yaichapa. Kwa mfano, unasema utafunga magoli, lugha ielekee katika usahihi wa mambo yanavyokwenda. Pamoja na kwamba kwenye mpira goli liko chini lakini watu hupiga mpira juu ni kwa lengo lao kwa sababu kuna baadhi ya watu ukipiga kimo kifupi wanaweza wakaudaka. Kwa hiyo, tunapiga mpira juu sio kwamba tunafuata goli, tunapeleka mpira juu ili uende mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemwambia Mheshimiwa Joseph Mungai, tulipotoka hapo nje kwamba pamoja na hotuba itakuwa nzuri na kuziba kila kitu, lakini kama hata nyumba ukiziba kila kitu useme kisitoke chochote litatokea giza. Pia na yeye mwenyewe akaniambia paka ukimzuia kwa mikono yote ile, atakuparua kwenye macho. Sasa matokeo haya ambayo yametokea, naomba pongezi azipokee lakini mapungufu yajazilizwe. Nakwambia leo vitendo, kesho ndoto, jana historia. Tenda leo kwa sababu kesho haiji, jana haisogeleki na leo haiondoki. Naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu nami nichangie wa mwisho katika hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza naomba nianze kwa kutoa salaam za rambirambi kwa ndugu zetu wa Mbeya kwa kuondokewa na mwenzetu Mheshimiwa Yete Mwalyego. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salaam hizo, napenda nichukue nafasi hii kuishukuru na kuipongeza Wizara ya Elimu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na timu yake ambayo iko pembezoni mwake pale kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati, mengi Mwenyekiti wangu amezungumza, ni kweli kwamba kazi wanayoifanya inaonekana, sidhani kama kuna Hakimu hata wa kukashifu kwamba hii kazi sio nzuri, ni nzuri. Majengo yanaonekana, madarasa yamekuwepo karibu kila kona ya nchi hii, hakuna ambaye hakufaidi matunda haya. Tunashukuru sana kwa mpango wa MMEM jinsi unavyoendelea na unavyoelekea kuishia na tunawapongeza sana kwa kuanzisha mpango wa MMES. Ni utaratibu mzuri kama wenzangu walivyotangulia kusema, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi alivyoielekeza, nafikiri inaonesha wana dira na wana utaratibu wa kuweza kurithishana. Tuna imani hata *University* naona wameanza kugusagusa, nafikiri kutakuwa na mipango mizuri ya namna hiyo ya kuwapokea hawa vijana wengi wanaotarajia kupata hiyo elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasi watu wa Mkoa wa Mwanza-Shinyanga kwa kweli tunashukuru sana. Lakini katika hili miaka ya nyuma tulikuwa nyuma na ndiyo maana kuna hali ya wananchi kwa kutokuwa na elimu tumekuwa na hali ya wazee kuchinjwa, vikongwe wanaonekana ndiyo wachawi hata kama mmekufa kwa UKIMWI. Lakini sasa tumegundua siri kwamba ni kwa sababu hatuna elimu na kwa Wilaya ya Geita kwa kweli

tunapenda tushukuru Wizara ya Elimu na Utamaduni, mwaka 2003 tumefungua shule saba, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005 tunatarajia kufungua shule za sekondari 21. Tunaomba Mheshimiwa Waziri na timu yako mkae na kwa upande wa MMEM, tuna maboma 800. Tulizungumza wakati wa Bajeti ya Wizara ya Fedha, hatukupata jibu. Tuna maboma 800 yako tayari yanasubiri kuezekwa, wananchi wamejitahidi sana. Ni kitu cha ajabu kwa upande wa usukumani kuwa na maboma 800, maboma ya madarasa, wewe Mmasai hujui. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maboma ya madarasa 800. Tunahitaji msaada na nguvu yako. Wananchi wamejitahidi, hivyo tunaomba sana. Tafadhali sana uweze kuwaona, tunaamini wewe ni mnyenyekevu na ni muelewa. Ila tunafikiria kwamba hujafika Wilaya ya Geita. Tunaomba utue kule, wewe tunajua ni askari. Sasa hukuning'inia juu, kuna wengine wamening'inia kwenye mibuyu hawajatua, sasa wewe umetua. Tua na Geita uje uone kazi tunayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule 21 vile vile tumeshatayarisha madarasa manne kwa kila shule. Tunaomba uje Mheshimiwa Waziri uyaone. Ingawa wenzangu wametangaza kusema uanzie Mtwara, Kasulu na wapi, sisi ni shule 21. Sasa uangalie wingi wa shule uanzie wapi.

Hiyo nakutahadharisha tu kwamba sasa hivi kuna haja ya Bajeti yako kuiangalia upya hasa upande wa walimu, tuna tatizo la walimu. Idadi ya walimu ni kidogo kwa shule tulizopewa saba, walimu hawapo. Wastani wa walimu ni watatu. Tunaomba walimu sasa katika Wizara yako jaribu kufanya mipango waweze kuwa wakutosheleza na hili ni tatizo la nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi jaribu kuangalia na Bajeti angalia kila Kata iwe na sekondari, ndiyo bajeti uiweke hivyo, ukiacha sehemu ya ndugu Wamasai ambao bado wanapambana, lakini wengi wanaelekea kwenye Kata na wenzetu wa Kaskazini wako kwenye vijiji. Sasa jaribu kubajeti, walimu wa namna hiyo, ikiwezekana ongeza vyuo. Sisi Geita, kwa kweli ukiangalia Wilaya ya Geita, Sengerema, Kahama, Bukombe, Biharamulo, Kibondo na Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla pale hakuna Chuo cha Ualimu. Tuwe na Chuo cha Ualimu Katoro pale ni katikati. Watoto wetu watasoma, tuwekee Chuo cha Ualimu na sisi tuweze kupata walimu wa kutosha. Tatizo kubwa ninalozungumzia hapa ni idadi ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona tatizo kubwa hapa ni walimu hawatatosha kwa *speed* iliyopo sasa hivi Inawezekana tukakushinda Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada unazozifanya na pamoja na pongezi kubwa na timu yako, nadhani kuna suala la kuangalia maslahi ya walimu hasa zile ambazo ni haki zao za msingi. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimesema kwamba tusiangalie tutajikuta tunalisha pua sio mdomo. Tutakuwa na madarasa mazuri,

madawati mazuri na *computer,* lakini kama walimu hatutawamotisha au kuwapa haki zao za msingi, litabaki kuwa ni tatizo. *(Makofi)*

Mimi sizungumzii kuongeza mshahara, ninachokiangalia ni zile haki zao kwamba anapohamishwa, anapokwenda likizo, kwenye matibabu, analipwa haki zake, kwa kweli inasikitisha sana. Mwaka 2003 tulileta hoja hii, tukaelezwa kwa lugha nzuri namna hii. Tulielezwa vizuri sana ila Mheshimiwa Waziri Mkuu hakusema atazungumza. Safari hii amesema alizungumza, labda mtatekeleza na tulikwenda mpaka kwa Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Madeni ya walimu yamekuwa ni kero. Walimu hawapewi haki zao zile za msingi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anasema pesa anapeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa najiuliza kwamba je, tuwape fedha tena, wakati zile hamjalipa? Mheshimiwa Waziri tunajua wewe ni mnyenyekevu, ni mwelewa, askari wa miamvuli aliyetua. Lakini hapa hujatua. Sasa hivi napata kinoti kwamba hata wewe nilikuwa nafikiri ni salama, hata wewe unadaiwa bilioni 4 na tena hujaanza kuhakiki na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitamka. Sasa kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alitamka wewe hujaanza kuhakiki, sasa mimi Mbunge hivi hivi utahakiki kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika hili nakuomba, hebu liangalie upya. Kuna walimu ambao wanaanza kazi hawa, ambao bado ni wanafunzi, inasikitisha ukienda kuona hali zao. Fikiria kama ni mwanao ameenda ametua mahala fulani kwenye kijiji anakaa miezi sita bila posho. Kama ni mwalimu wa kike au wa kiume hasa wa kike anakaa pale na anatua pale kijiji kinamwona hii ni mali imeingia lakini maskini wa kutupwa.

Mheshimiwa James Musalika, alilizungumzia suala hili kwamba watu wanaolewa na wazee bila utaratibu, mabalozi, wenyeviti wa vijiji. Hiyo hali halisi, walipwe hawa watoto hawa, pesa zao ikiwezekana kama Serikali za Mitaa imeshindwa kuwahudumia basi iwe na *direct contact* na Wizara ya Elimu na Utamaduni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu inaonekana kule ulikowatenga wamekuwa watoto yatima, mtu anakaa muda wote bila kulipwa. Wengine sasa hivi wanajuta kwa nini shule zinafunguliwa kwa sababu anaenda kuingia jehanamu tena. Fedha inawezekana zipo, lakini upelekaji. Naomba nimweleze Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwamba, suala hili inawezekana si lako, lakini kule mwanakijiji hajui mtu wa Serikali za Mitaa kwamba ndiye mhusika, anayekujua ni wewe, basi mwambie mwenzako kwamba unaniangusha. Mimi nimetua wewe mbona hutui? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili kwa kweli nalizungumza kwa uchungu kwa sababu kila mahali kuna tatizo hili. Mimi ni mdhamini wa Chama cha Walimu. Nimekwenda Matundafi, nimekwenda Chunya Juu, nimekwenda kila mahali bahati nzuri na kwenye Kamati ya Maadili nakwenda katika Chama cha Walimu naripoti ni tatizo hilo hilo. Halafu kinachosikitisha ni kwamba baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuzungumza kwamba madeni yalipwe sasa hivi ndiyo ma-*DEO* wanaita walimu kwamba leteni madeni, mnaodai njooni.

Sasa kumbe tuliozungumza hapa ni uongo shilingi bilioni 18 inawezekana ikafika shilingi bilioni 30, kwa sababu sasa ndiyo madeni yanakusanywa na wengine wanaleta sasa hivi. Inawezekana ikawa bilioni 30.

Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyeachiwa basi amwambie kwamba inazidi silingi bilioni 18 na yeye hayupo, lakini wahusika wapo watamweleza, sasa hivi wanakusanya madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Wilaya hakuna *data* zinazoonyesha kweli kwamba hawa wanaweka takwimu au zinaliwa tu. Sasa wanahitaji wa nini tena walimu, taarifa ninazo na ushahidi upo kwamba walimu sasa hivi ndiyo wanaambiwa leta madeni. Kwa kweli inasikitisha hali hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Kweli kabisa, waambie!

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2003 niliuliza suala la *responsibility allowance* kwa viongozi katika Elimu. Nampongeza Mheshimiwa Jackson Makwetta, amezungumzia suala la *REO* awepo, napenda na mimi niseme wawepo. Kwa sababu elimu inapanuka, nilizungumzia suala la *responsibility* ya *REO, Headmaster, Principal,* Afisa Taaluma na wengine wote watendaji wakuu viongozi hata kwenye Wizara. Unakuta *Headmaster* au *REO* walio chini yake au walioanza kazi juzi, wanamzidi mshahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama wanamzidi mshahara hawa watu, utendaji wake wa kazi ni vipi? Kwa nini wasiweze kuwa *motivated,* kwa sababu hata umemshusha madaraka, mshahara wake ni ule ule hakuna hata cha kupoteza hana cha nini. Kwani kosa, niseme kwamba ni kosa, mtu unapofunua faili la mtu wakati wewe anakuzidi mshahara, sijui ni utaratibu gani huo. Wewe ni *junior* halafu unakwenda kuitisha faili lake. *Is that fair? (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona umewaambia ma-*headmaster* wapo hapo juu, lakini *are they fair* kuitisha mafaili ya watu wanaowazidi mishahara na wanaweza kuwa wao wana magredi ya juu? Hamwezi kulifikiria hilo? Lakini vile vile tuliambiwa na jibu lilitolewa kwamba mambo yako kwenye *computer* mpaka sasa hivi. Sasa mimi inanipa wasiwasi je, jibu la sasa hivi litazidi la mwaka 2003 na mwaka 2002, litatekelezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema sasa lipeni. Lakini mimi nakuwa na wasiwasi na inakuwa haileti heshima kwa Serikali. Lakini inapotoa fedha ziende kwa walengwa basi, viishe tujue vimeisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwaambie tena Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwamba kazi wanayoifanya ni nzuri katika hili la walimu tafadhali liangalieni, katika majumuisho tutaelewana kwamba madeni yatalipwa na kwa nini

yaanze kufanyiwa kazi mpaka unapoelezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, *that is not fair*. Kwanza ni kumpa tabu ambayo siyo kazi yake.

**MBUNGE FULANI:** Kweli kabisa.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Wengine wanaomtolea *comment* hata haitolewi na mtu kutoka kwenye ile Wizara kwamba tutajitahidi kufanya kazi. Inaonekana ni la Mheshimiwa Waziri Mkuu hili. Sisi hatukufurahishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kufika hapo tumemaliza shughuli za Bunge kwa leo. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.41 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa tarehe 9 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*